# Nipashe

Alhamisi Desemba 1, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581146

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



AFYA NA MAZINGIRA

Mradi misitu wakikomboa kijiji kilichosaka zahanati miaka 32

Pata umuhimu matunda, mboga kuliwa yakiwa na maganda yake

...zindua jiko 'rafiki wa mazingira'

UKURASA 13


JACKPOT BABA LAO!

TZS. 412,613,570

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**TCRA:** Utapeli 'Tuma kwa namba hii' unavyofanyika

UKURASA 3

# Mlinzi adaiwa kuuawa na bosi akiwa lindoni

UK. 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### MPANGO AIWASHIA MOTO TBA UTENDAJI



MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ametoa maagizo sita kwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ikiwamo kuwabana...

UKURASA WA 4

### FAMILIA ILIYOPOTEZA MAISHA KUAGWA LEO



MIILI ya mama na watoto wake wawili waliofariki katika ajali iliyotokea Jumamosi eneo...

UKURASA WA 7

### MAKALLA AWAGEUKIA MAOFISA MGOGORO ARDHI



MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amesema mgogoro wa ardhi unaoendelea Kimbiji, Manispaa ya...

## Mabalozi EU waridhishwa na juhudi kukabili ukatili kijinsia

UKURASA 3



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akitunukiwa Shahada ya Udaktari wa Falsafa wa Heshima ikiwa ni Shahada ya Udaktari wa Juu katika Humanitia na Sayansi Jamii na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Rais mstaafu, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, katika mahafali ya 52 ya duru ya tano ya chuo hicho jana. **PICHA: IKULU**

# Sababu UDSM kumtunuku Samia udaktari wa heshima

• **Mwenyewe** atoa neno, JK ataka utafiti wanaume wachache udahili vyuo vikuu... *Endelea ukurasa 2*


MICHEZO YANGA SC YAELEZA ILIPOANGUKIA UK.32 KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA



Wafanyabiashara wadogo wakifanya shughuli zao barabarani, eneo la Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mlinzi adaiwa kuuawa na bosi lindoni

**Na Elizabeth Zaya**

MLINZI wa eneo la kuhifadhia mitungi ya gesi eneo la Tegeta Scanska, Kinondoni, Dar es Salaam, Salim Haji, anadaiwa kuuawa kwa kupigwa risasi na mmiliki wa biashara hiyo, kisha mwili wake kuchukuliwa na kupelekwa kusikojulikana usiku.

Mlinzi huyo ambaye ni mwajiriwa wa kampuni ya ulinzi ya Homasa, anadaiwa kuuawa Novemba 20, mwaka huu, akiwa kazini kwa mmoja wa wateja wa kampuni hiyo na mpaka sasa ndugu zake wanatafuta mwili wake na hawajauona.

Kwa mujibu wa mlinzi mwenzake aliyejitaja kwa jina moja la Julius, mwenzake aliuawa akiwa lindoni ndani ya eneo la kazi, kati ya saa 4:00 na saa 5:00 usiku wakati yeye akiimarisha ulinzi getini na mwenzake (anayedaiwa kuuawa) akiimarisha ulinzi kwa ndani.

"Ilikuwa saa tano kama kasoro dakika 10 au 12, waliingia wafanyakazi wa kusambaza mitungi ya gesi wakiwa na usafiri wa pikipiki na baada ya dakika tano, nikasikia geti linavutwa, alikuwa bosi wa hilo eneo la gesi tunapolinda. Alipoingia ndani akaninyooshea bastola akasema anawafuata wale waliorudisha mitungi ya gesi huku akininyooshea bastola," alisema Julius

"Alipowafuata, dakika chache nikasikia milio ya risasi, nikawaona wale wafanyakazi wake waliokuwa wamerudisha gesi wakawa wanakuja wanakimbia. Nilipowauliza, wakaniambia bosi wao anarusha risasi na nilipowauliza sababu ya kufanya hivyo, wakaendelea kukimbia huku wanatoka.

"Mara nikaona anakuja hadi niliko getini, akaniambia niweke silaha chini niondoke la sivyo atanipasua, nikamwambia siondoki, nalinda mali hapa. Akaendelea kunisisitiza nikagoma. Nilipoona hivyo nikageuka kwa nyuma kwa nje hapo hapo getini, akaninyooshea bastola, kidogo akapiga risasi juu. Wakati huo nikaona mke wake anaingia na gari ndani huku akimsisitiza asipige risasi.

"Baada ya kuona anaendelea kupiga risasi juu, mimi nikatoka nikaanza kukimbia ili nikawapigie simu viongozi wangu ambao baada ya dakika 20 wakawa wamefika eneo la tukio. Wakati huo wa purukushani zote hizo zikiendelea, sikumwona askari mwenzangu kutokeza japokuwa yeye ndiye alikuwa kwa ndani zaidi maana ni eneo kubwa.

"Baada ya kiongozi wangu kufika, nilimwambia atanguliе, nikabaki nyuma na alipofika yeye akaona gari imepakiza mtu na imetoka. Baada ya wao kuondoka tukazunguka mle ndani kuanza kumwita mlinzi mwenzangu, hatukumuona. Tulipiga simu yake mwanzoni ilikuwa inapokelewa halafu hakuna anayeongea, kwa hiyo tulichoambulia kuona ni damu zikiwa zimetapakaa chini," alisimulia.

Alisema, majira ya saa 6:00 usiku huo huo, alirudi tena mke wa mmiliki wa gesi akiwa anatembea kwa miguu na walipomuuliza nini kinaendelea kwa mume wake, aliwajibu kiufupi kwamba ni mambo ya dunia.

"Dakika chache, mume wake naye akarudi tena akitembea kwa miguu, ananiambia kwamba nifukie ile damu iliyokuwa imetapakaa pale chini, nikamwambia sifukii mpaka polisi waje wafanye uchunguzi tujue ni ya nini."

Alisema baada ya kumtafuta mwenzake bila mafanikio, walikwenda kituo cha polisi Madale kutoa taarifa na wakapatiwa namba MBD/CID/PE/34/2022.

"Cha kushangaza tulipofika polisi ilikuwa saa 9:30 usiku, tulipoanza kuandikisha maelezo yetu tukamwona yule bosi aliyefanya tukio la kupiga risasi naye amekuja. Tukaenda tena eneo la tukio na polisi wakachukua taarifa na wakafungua jalada letu," alisema.

Alisema tangu kutokea kwa tukio hilo, wamekuwa wakifuatilia polisi kujua upelelezi ulipofikia lakini wanaambiwa bado upelelezi unaendelea.

"Kibaya zaidi wanatuambia hivyo wakati hata hatujui mwenzetu yuko wapi na wakati mwingine tunarushiwa maneno makali na baadhi ya askari jambo ambalo linatutia mashaka. Ndugu nao wanataka mtoto wao," alisema Julius.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Ulinzi ya Homasa, Imani Mileka, alisema alipata taarifa ya kutokea tukio hilo usiku wa Novemba 20 kuamkia Novemba 21 kwamba mteja wake wa mitungi ya gesi (anamtaja jina lake), amefyatua risasi, eneo la tukio kumetapakaa damu na mlinzi mwenzao hayupo.

"Nilipofika pale nilikuta damu na sikujua ni ya nani kwa wakati ule. Kwa kawaida lindo hilo huwa lina walinzi wawili, mmoja anashika silaha na mwingine rungu, kwa hiyo mlinzi Salimu ambaye haonekani mpaka leo yeye ndiye alikuwa anashika rungu kwa ndani ambaye sikumuona nilipofika na mwenzake aliyepona akiwa getini.

"Nilipomuuliza sababu ya kufyatua risasi, alisema eti alipomfukuza mlinzi getini, walikwenda vibaka wakataka kumkata mapanga, kwa hiyo akavunja mguu wa mmoja wapo lakini wakapakizana kwenye boda boda wakakimbia. Na hata tulipomuuliza alipo mlinzi wetu mmoja akawa mkali na kuniambia nimwache," alisema.

Alisema baada ya tukio hilo, mteja wake alivunja mkataba wa kampuni yake kuendelea kufanya kazi nao.

Mjomba wa Mlinzi anayedaiwa kuuawa, Bakari Mdoe, alisema tangu kijana wao alipokwenda kazini Novemba 20 hawakumwona tena.

Nipashe ilimpigia simu Kamanda wa Polisi Kanda maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro ili kujua endapo ana taarifa ya tukio hilo lakini simu zake hazikupokewa.

# Sababu UDSM kumtunuku Samia shahada udaktari

**Na Jenifer Gilla**

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kimeeleza sababu za kumtunuku Rais Samia Suluhu Hassan Shahada ya Heshima ya Udaktari kuwa ni maridhiano, ustahimilivu, mabadiliko na kujenga nchi.

Aidha, chuo hicho kimesema kwa mujibu wa Kanuni za Shahada za Heshima za mwaka 2014, kimesema mtu anatunukiwa akiwa amefikia vigezo mbalimbali kama elimu, kutumia maarifa kutatua changamoto kubwa na mchango mkubwa na uwazi katika kutetea haki za binadamu.

Rais Samia alitunukiwa shahada hiyo na Mkuu wa Chuo hicho, Rais Mstaafu Dk. Jayaka Kikwete, wakati wa Mahafali ya 52 Duru ya Tano ya UDSM, wahitimu 141 shahada za uzamivu (Ph.D) na 1,002 shahada za umahiri (masters).

Akisoma wasifu wa Rais Samia kabla ya kumtunuku, Mwenyekiti wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Prof. Penina Mlama, alisema mwaka 2021 serikali ya Rais huyo ilitia saini mkataba na Shirika la Fedha Duniani (IMF) wa mkopo wa masharti nafuu wa Sh. trilioni 1.3 kwa ajili ya kampeni ya maendeleo ya ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO- 19, zilizoelekezwa kwenye miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa shule, miundombinu ya kielimu tofauti na mataifa mengine ambayo yalielekeza kwenye afya.

Pia alisema serikali hiyo imeongeza bajeti katika fedha za mikopo ya elimu ya juu kwa kiasi kikubwa na kutoa ufadhili kwa wanafunzi watakaofanya vizuri katika mitihani ya kidato cha sita na kuchagua masomo ya sayansi, uhandisi na tiba kwa mwaka 2022/23. Kupitia ufadhili huo, wanafunzi takribani 640 wamedahiliwa katika vyuo vikuu. Prof. Mlama alisema Samia alichukua hatua za kisera na kisheria kuboresha sekta ya elimu na utekelezaji wa mapitio ya Sera ya Elimu ya 2014, hivyo kufanya marekebisho ya mitaala, ili ielekezwe kwenye kutoa elimu ujuzi kulingana na mazingira ya nchi na soko la ajira.

Kwa mujibu wa Prof. Mlama, serikali ya Rais Samia ilitekeleza kwa vitendo dhana ya kuleta maridhiano na kujenga demokrasia na umoja nchini. Alisema Rais alikutana na makundi mbalimbali wakiwamo viongozi wa vyama vya siasa ili kupata maoni yao juu ya mustakabali wa nchi na kuendeleza misingi ya utawala bora, usawa na maendeleo ya uchumi.

Pia alisema alitekeleza ahadi ya kuleta usawa wa kijinsia kwa kuteua wanawake wengi wenye uwezo, ili kujaza nafasi mbalimbali za uongozi, ikiwamo Spika wa Bunge, Katibu wa Bunge ni mwanamke kwa mara ya kwanza, idadi ya wanawake katika baraza la mawaziri ikaongezeka kutoka wanne hadi tisa pamoja na kuteua waziri wa ulinzi mwanamke.

Kwa mujibu wa Prof. Mlama, Rais Samia ni mmoja wa viongozi 100 wenye ushawishi duniani kutoka gazeti la American na ile ya Arican Road Buiders Ndiaye Troupyh kwa uendelezaji miundombinu ya usafirishaji na reli nchini.

"Tangu kuingia madarakani Rais Samia amechukua hatua mbalimbali za kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji na sekta binafsi, ili kuvutia wawekezaji wengi zaidi na kukuza sekta binafsi. Hii ni pamoja na kupunguza vikwazo katika upatikanaji wa vibali, na leseni za biashara na kurekebisha kodi mbalimbali," alisema Profesa Mlama.

**ATOA NENO**

Akizungumza baada ya kutunukiwa, Dk. Samia alisema hakujua kwamba mageuzi aliyofanya katika sekta mbalimbali kwa kipindi kifupi, ili kuendana na mabadiliko ya dunia, ndiyo yaliyompa sifa ya kutunikiwa shahada hiyo.

Alisema katika kuleta mageuzi hayo alitumia dhana za mariadhiano, ustahimilivu, mabadiliko na kujenga upya taifa ambazo inagusa maeneo yote ya maisha ya Mtanzania na kuondoa dhana ya kutumia siasa katika masuala ya maendeleo hasa kujenga uchumi.

"Nikajitizama sikuona kama nina sifa za kupewa shahada hii. Lakini baada ya kusikiliza kwa makini maelezo marefu juu ya wasifu wangu nimepata mwanga wa sababu zilizosukuma UDSM kunitunuku shahada hii, yenye kuhusiana na uwanja mpana wa ubinadamu na utu na hivyo kugusa moja kwa moja maisha ya Mtanzania.

"Nilikuwa naamini kabisa kuwa maendeleo hayawezi kuja bila kuungana na taifa kuwa kitu kimoja, tunaweza kutofautiana kimitazamo lakini sote ni Watanzania wenye lengo la maendeleo ya nchi yetu. Nilikuwa nikiamini kuwa kila kitu kikizidi kina kasoro kwa hiyo nikaona madhara ya kuzigeuza siasa katika kila kitu ikiwa ni pamoja na kuzifanya kuwa njia za uchumi, "alisema. Samia alisema alikuwa akipigania usawa wa kijinsia, ili kuwapa fursa na wajibu sawa wa kulitumikia taifa wanawake na wanaume kwa kuwa anaamini kuwa binadamu wote ni sawa.

Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Kiwete alisema katika udahili wa mwaka huu kuna ongezeko kubwa la wanawake kwa asilimia 53 huku wanaume wakiwa asilimia 47 jambo alilohitaji lifanyiwe utafiti, kubaini sababu za ushiriki wa wanaume katika masomo ya juu kushuka.

"Sasa sijui watoto wa kiume wamekwenda wapi siku hizi. Itabidi suala hili nalo tukae na kulifanyia utafiti. Sijui huko walikokwenda ni wapi ila tunafurahi kwamba sasa wanawake wameongezeka sana. Zamani tulikuwa tunadhani kwamba ni wanaume tu, tena hata kwenye yale masomo ya fizikia, kemia, uhandisi na udakatari wanawake huko ndio wabobezi kabisa," alisema.

## HABARI KITAIFA



Wanafunzi kutoka shule mbalimbali za Wilaya ya Kinondoni na wananchi wakishiriki matembezi ya kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia yaliyoandaliwa na kampuni ya Barrick kwa kushirikiana na Dawati la Jinsia la Jeshi la Polisi, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni maadhimisho ya siku 16 za kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mabalozi EU waridhishwa mapambano ukatili kijinsia

**Na Salome Kitomari**

MABALOZI wa Umoja wa Ulaya (EU), wamesema wanaridhishwa na jitihada za serikali katika kukabili na kumaliza ukatili wa kijinsia kwa makundi yote, huku wakiahidi kuendelea kushirikiana na wadau wote kuutokomeza kwenye jamii. Wakizungumza na waandishi wa habari juzi katika uzinduzi wa siku 16 za harakati kupinga ukatili wa kijinsia, mabalozi hao kutoka nchi za Ufaransa, Ubelgiji, Finland, Ujerumani, Ireland, Italia, Uholanzi, Hispania, Denmark na Sweden, walisema wanaungana na Watanzania kukabili hali hiyo ambayo ni kinyume na haki za binadamu.

Mgeni rasmi katika mkutano huo, alikuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima.

Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui, alisema jitihada za Tanzania ni za kuigwa na dunia kwa kuwa zinaleta suluhisho la kudumu kuanzia ngazi ya kaya hadi taifa.

"Tunafurahi kuwa mambo yamebadilika yako chanja, tunaona Tanzania inakwenda kwenye njia sahihi sana, inastahili kuigwa kwa hatua zinazochukuliwa kuwalinda wasichana na watoto," alisema.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani, Juni mwaka huu alikwenda Paris na kutuma ujumbe mahususi duniani kwamba Tanzania itakuwa na agenda maalum ya kupinga ukatili wa kijinsia, na kwamba wameona utekelezaji kwa vitendo.

Awali, Balozi wa EU, Tanzania Manfredo Fanti, alisema ukatili dhidi ya wanawake na wasichana ni tatizo la duniani na linaathiri maendeleo ya makundi hayo.

Alisema ukatili huo uliongezeka zaidi wakati wa ugonjwa wa COVID-19, kasi ya ukuaji wa mitandao na vita inayoendelea Ukraine ambayo imesababisha wanawake wengi kuingia kwenye kuuza miili yao.

Balozi Fanti alisema sensa ya watu na makazi Tanzania imeonyesha asilimia 49 ni wanaume na asilimia 51 ni wanawake na kwamba sio sahihi kuacha kwenye hatari nusu ya watu.

Alisema ripoti ya taasisi za kijamii na jinsia (SIGI), ya Tanzania imeweka bayana ushahidi kwamba vitendo vyovyote vya ukatili vinawaathiri wanawake kwa zaidi ya asilimia 50 na kwamba inaonyesha bado kuna kazi kubwa ya kufanya.

"Zaidi ya wanawake bilioni 2.5 wanaathiriwa na sheria kandamizi na hawalindwi kisheria kuliko wanaume na wavulana. Wasichana wana wakati mgumu zaidi kupata hati za kusafiria, kurithi mali na kuolewa na mtu wanayempenda au la," alisema na kuongeza:

Waziri Gwajima alisema hakuna aliye na kinga kwa kutenda ukatili na kuna wanaotendewa, ila hawajui kwamba ni ukatili, lakini taratibu za mila na kifamilia zinawafanya wafiche, kutokana na elimu inayotolewa mwamko wa kuripoti umeongezeka.

"Wadau mkiwemo nyie mabalozi mmesaidia sana jitihada za kupinga ukatili, nina uhakika ndani ya miaka mitano tutakuwa mahali pazuri na tutazungumzia mafanikio zaidi kuliko changmoto, jitihada za Rais Samia zitaendelea kuzaa matunda," alisema.

Alisema kuna madawati ya jinsia 420 katika vituo mbalimbali vya polisi kwa ajili ya kesi za ukatili, lakini kwenye Magereza kuna vituo 153 na vituo maalum 21 vya kushughulikia masuala hayo.

Waziri Gwajima alisema kuna kamati 18,186 za kulinda wanawake na watoto nchi nzima kuanzia ngazi ya mtaa na kwamba zina wajibu wa kushughulikia matatizo yote ya ukatili wa kijinsia.

Balozi hizo zitakuwa na matukio mbalimbali kama warsha na midahalo ya kitaalam, msafara wa kupinga ukatili wa kijinsia miaka 12 kwa kuwashirikisha wanaume na wavulana, ziara ya shule salama katika shule mbalimbali, kutoa tuzo kwa wapinga ukatili na kuwaleta pamoja watu kupaza sauti, wanaharakati, washirika na watoa maamuzi kushughulikia GBV.

# TCRA: Utapeli 'Tuma kwa namna hii' unavyofanyika

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imeeleza wahalifu wa mitandao ya simu maarufu kama 'Tuma kwa namba hii' wanavyosajili laini kinyemela kwa kutumia vitambulisho na alama za vidole vya watu, bila wahusika kugundua.

Imesema uhalifu huo hufanywa na mawakala wanaosajili laini za simu mteja anapokwenda kujisajili akiwa na kitambulisho kwa kumtaka kuweka alama za vidole kwenye mashine zaidi ya mara moja kwa kisingizio alama haijasoma.

Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Bidhaa za Mawasiliano TCRA, Thadayo Ringo, alibainisha udanganyifu huo juzi wakati akitoa mafunzo ya kuzijengea uwezo wa kukabiliana na makosa ya mitandaoni Kamati za Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano za mikoa kupitia Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA- CCC).

"Ukienda kusajili laini ukiona umechukuliwa alama za vidole, akaendelea kuingiza taarifa akarudi kukuambia tena alama hazijakubali rudia tena usikubali, anatumia taarifa zako kusajili laini zaidi ya moja na kuwapatia wahalifu," alisema Thadayo.

Alisema wahalifu wa mitandao wamekuwa wakiibuka na mbinu mpya kila mara na TCRA huchunguza na kuzibaini kuhakikisha wanadhibiti uhalifu.

Maelezo hayo yalitokana na swali lililoulizwa na mmoja wa wajumbe hao, Ally Nassoro

kutoka Tanga, aliyetaka kufahamu TCRA inashindwaje kuwakamata wahalifu wanaotumia simu zilizosajiliwa kuomba fedha kwa watu.

Alisema ili kumaliza tatizo hilo, kila mtumiaji wa laini ya simu anatakiwa kupiga namba *106# kutazama idadi ya namba za simu zilizosajiliwa kwa namba yake ya Kitambulisho cha Taifa kinachotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

Alisema baada ya kupiga namba *106# utapewa chaguzi kadhaa namba 1 hadi 5, ukichagua namba 3 utatazama idadi ya namba za simu zilizosajiliwa kwa namba yako ya uraia iliyotolewa na NIDA.

Kwa mujibu wa Thadayo, mtumiaji wa huduma za mawasiliano ya simu za mkononi akibaini namba za ziada, zaidi ya zilizosajiliwa kwa namba yake ya NIDA, atatakiwa kuchukua hatua ya kufika katika dawati la huduma kwa wateja ili kutoa taarifa itakayowezesha kufutwa kwa namba ambazo hakuzitambua.

Alisema hatua hiyo ni muhimu kwa kuwa inamlinda mtumiaji wa huduma za mawasiliano dhidi ya matumizi mabaya ya namba hizo yakiwamo yanayohusisha uhalifu.

Alisema mwakani wataanza kuzifungia lakini zote zisizohakikiwa na zinazomilikiwa nyingi na mtu mmoja.


KNAUF

## PUBLIC TENDER NOTICE

### TENDER NO: MKURANGA II 3652 CONSTRUCTION SERVICE IN DESIGN AND BUILD (EXTENSION) OF EXISTING PLASTERBOARD PRODUCTION LINE.

Knauf international is one of the world's leading manufacturers of modern insulation materials, drylining systems, plasters, thermal insulation composite systems, paints, floor screed, floor systems, construction equipment, tools, and other accessories. Knauf has more than 300 production facilities, with sales organizations in over 90 countries, 40,000 employees worldwide.

**Knauf Gypsum Tanzania Limited** being a part of Knauf international produces German quality drywall products using locally sourced materials. **Knauf Tanzania** is going to extend its plasterboard production line, located at Kisemvule, Mkuranga, Tanzania, from the manufacturing capacity of **15 million square to 40.5 million square.**

**The Company do hereby** invite competitive, reliable, well performing, experienced and eligible **Local Contractors** to tender for the construction service in **Design and Build** of its plasterboard production line based on the description and pre – qualification criteria provided in the table below.

**Description and pre – qualification criteria**

| No | Reference number | Description of work | Pre-qualification criteria |
|---|---|---|---|
| 1 | Mkuranga II 3652 | • Extension of current plant building'<br>• New raw material stock area<br>• New parking area including internal roads.<br>• New social building | Civil and Building works Contractor Class 1 |

If your company meets the pre – qualification criteria you may obtain information from the Procurement & Logistics department at Knauf HQ offices, **Plot 17 Block 186030 14110 • Off Kinondoni Road • Mwindu Lane street, Dar es salaam** from 10:00AM to 16:00PM weekdays only.

A complete set of Tender Documents in English which include tender rules, terms and conditions will be available for physical collection at a fee of Tshs. 100,000/=. Funds must be deposited to the below bank details; (ensure your company details are clearly indicated on the deposit slip when collecting the tender documents for record and reference)

| BANK DETAILS | |
|---|---|
| Bank Name: | CRDB Bank Tanzania Ltd |
| Account Name: | **KNAUF GYPSUM TANZANIA LTD** |
| Account Number | **0150440243800** |
| Branch | Oysterbay Branch |

Submission deadline is **14th December 2022**, Late tenders, partial submission will not be considered.
**ENQUIRIES:** Magretha.VanDerMerwe@knauf.com

**NB: This tender advert does not entail any commitment on the part of Knauf to any applicant. Knauf reserves the right to accept or reject any or all applications without incurring any obligation to inform the applicant (s) of the grounds.**

217172402

## HABARI KITAIFA

# Mpango aiwashia moto TBA utendaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ametoa maagizo sita kwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ikiwamo kuwabana wadaiwa sugu walionunua au kupanga nyumba bila kumwonea aibu mtu hata kama ni kiongozi.

Dk. Mpango alitoa maagizo hayo jana jijini hapa alipokuwa akiweka jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa nyumba 3,500 za watumishi wa umma zinazojengwa eneo la Nzuguni B.

"Kumekuwa na ulegevu kwenye kufuatilia utekelezaji wa mikataba, jambo ambalo limesababisha serikali kupoteza mapato ya kodi. Kupitia hadhara hii, nasisitiza msimamie mikataba yenu kwa karibu zaidi. Hakikisheni pia mnasimamia na kuweka mifumo rafiki ya ukusanyaji wa mapato na kuziba mianya yote ya upotevu wa mapato. Fedha zisiishie mifukoni mwa watu.

"Kuweni wakali na mchukue hatua za kisheria haraka iwezekenavyo kwa wale wote wanaokiuka masharti ya mikataba. Msionee mtu aibu hata kama ni kiongozi,"alisema.

Pia aliagiza wakala kufikiri namna ya kujijenga kibiashara ili kupata mapato zaidi na kujiendesha na kusisitiza kuzingatia ubora na ukisasa kwa gharama nafuu.

"Punguzeni utegemezi wa ruzuku ya serikali kupitia wizara. Serikali ilikwisharuhusu ushirikishaji wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa kuingia ubia. Wizara ya Ujenzi (na Uchukuzi) harakisheni mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Uanzishwaji wa Wakala wa Majengo Tanzania ili taasisi kukamilisha taratibu zote za kuingia ubia na wawekezaji," alisema.

Dk. Mpango alisema kumekuwa na malalamiko mengi kuhusiana na upatikanaji wa maduka, nafasi katika masoko na vizimba kwa ajili ya kufanya biashara kwenye maeneo yenye miradi ya aina hiyo na kuwataka wahusika wote wahakikishe yanapatikana bila upendeleo na kwa uwazi.

Alisema serikali itaendelea kujenga nyumba zaidi ili kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 inayoelekeza TBA kuendeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 10,000 nchini kwa ajili ya viongozi wa serikali na watumishi wa umma.

"Tunatambua kuwa makazi bora ni sehemu ya haki ya msingi ya wafanyakazi. Nchi nzima ina watumishi wa umma 500,000 ambao ndio walengwa wa nyumba za TBA. Hadi sasa wakala ina jumla ya nyumba 7,116 tu nchi nzima zikijumuishwa pia nyumba za viongozi. Hii inaonyesha ni kwa kiasi gani uhitaji wa nyumba kwa watumishi wa umma bado ni mkubwa sana," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Selemani Kakoso, aliomba serikali kulipa madeni ya TBA yanayotokana na kodi za nyumba na kazi inazopewa kusimamia.

Naye Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa alisema mradi huo unasaidia wataalamu wazawa wa fani za ujenzi kujengewa uwezo wa taaluma kwa vitendo pamoja na kusaidia kuendelea kukua kwa kasi kwa Jiji la Dodoma.

Awali, Mtendaji Mkuu wa TBA, Daud Kondoro, alisema kutokana na utafiti uliofanyika, Dodoma kuna uhitaji wa zaidi ya nyumba 2,000 kwa ajili ya watumishi wa umma.

Kandoro alisema katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi huo ambao nyumba 150 zimejengwa, Sh. bilioni 14.3 zimetolewa pamoja na kutoa Sh. bilioni moja katika mwaka wa fedha 2022/23 kwa ajili ya awamu ya pili na maandalizi yameanza.



Mkurugenzi wa Oryx Gas Tanzania Ltd, Araman Benoite (kushoto), akikabidhi moja kati ya majiko ya gesi 600 kwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea Vijijini, Menasi Komba (kulia), kwa ajili ya wanawake wa viongozi wa halmashauri hiyo jana, ikiwa ni mkakati wa kuhamasisha nishati safi ya kupikia hatua ya kukabiliana na uharibifu wa mazingira. Katikati ni Mbunge wa Jimbo la Peramiho ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Moshi,**
**S.L.P. 2888,**
**40470DODOMA,**
**Tarehe 02/12/2022**

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe **02-12-2022** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **DODOMA**, gari hilo lenye namba za usajili:

Gari hizo zenye namba za usajili:
**T 175 DFN / T 168 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 18.00, Upana - mita 2.80, Kimo - mita 5.00**

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM** hadi **DODOMA** kupitia **MOROGORO**.
Gari itasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

17172002

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Barua Pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Mtumba,**
**S.L.P. 2888,**
**40470DODOMA,**
**Tarehe 30/11/2022**

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe **02/12/2022** kampuni ya **AFRICA WAKAWAKA LOGISTICS CO. LTD** itasafirisha mzigo mkubwa kutoka Dar es Salaam kuelekeaa Kigoma kupitia Dodoma.

Gari hizo zenye namba za usajili:
1. **T236DXJ / T676DYK**
2. **T273DYD / T788DXH**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu-22m Upana -4.5 m Kimo-5,**
**Urefu-22m Upana -4.5 m Kimo-5**

Gari litasafiri mzigo kuanzia saa **12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

17172602

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**


## Familia iliyopoteza maisha kuagwa leo

**Na Romana Mallya**

MIILI ya mama na watoto wake wawili waliofariki katika ajali iliyotokea Jumamosi eneo la Kibamba Hospitali mkoani Dar es Salaam, inatarajiwa kuagwa leo katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Magengeni.

Waliofariki dunia katika ajali hiyo ni Immaculata Byemerwa (mama) na watoto wake, Janeth Byemerwa aliyekuwa mwaka wa tatu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), akisomea Uhandisi Ujenzi (Bsc.Civil Engineering) na Jollister Byemerwa, aliyehitimu kidato cha nne mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, kaka wa marehemu Immaculata, Patrick Mpocholwa alisema kuwa miili hiyo itaagwa leo kanisani hapo na baadae jioni maziko yatafanyika Kibaha kwa Mwendapole mkoani Pwani.

Pia, alisema majeruhi, Albert Mrema ambaye amelazwa Hospitali ya Mlongazila katika Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU), aliyekuwa akiendesha gari T 597 BWU, aina ya Toyota Prado, ambayo lilisababisha vifo hivyo, anaendelea vizuri.

Familia hiyo ilipoteza maisha siku hiyo baada ya gari waliyokuwa wakisafiria kutoka kwenye mahafali ya Jollister aliyemaliza kidato cha nne, katika Shule ya Sekondari Gili iliyopo Kibaha, kuacha njia na kuingia bondeni eneo la Kibamba Hospitali.



## TANGAZO


A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
KILIMANJARO
DRINKING WATER
FURAHIA MAISHA NA MAJI ASILIA
500ml
1000ml
1500ml
6L
12L
18.9L
+255 659 536 937, +255 758 979 641, +255 659 785 276
kdw@bbl.co.tz
kilimanjarodrinkingwater
kilimanjaro_drinking_water
61707202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TRA iweke mazingira bora kuimarisha ulipaji wa kodi

**SERIKALI** imekuwa ikitekeleza miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali kama vile elimu, afya, miundombinu pamoja na shughuli za uendeshaji na utawala katika wizara na idara zinazojitegemea. Utekelezaji wa miradi hiyo hutegemea makusanyo ya kodi mbalimbali, mapato ya ndani katika halmashauri, misaada na mikopo kutoka nchi wahisani na mashirika ya kimataifa.

Pamoja na vyanzo hivyo, ili kujiendesha kwa ufanisi, serikali inapaswa kuimarisha mifumo ya ndani katika ukusanyaji mapato hasa yale yatokanayo na kodi kama vile za mapato, ushuru wa forodha na bidhaa na za mishahara ya watumishi wa umma na wafanyakazi wa sekta binafsi.

Kwa kufanya hivyo, serikali inaweza kupunguza utegemezi wa misaada na mikopo kutoka nje ambayo wakati mwingine huchelewa na pia huwapatia mzigo wananchi wake kulipa fedha hizo ambazo hivi sasa zinasababisha deni la taifa kuongezeka.

Ili makusanyo ya serikali yapatikane na hatimaye kuelekezwa katika miradi ya maendeleo, serikali ilianzisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kwa ajili ya kubuni vyanzo vya mapato na kuvisimamia kikamilifu. Ndiyo maana kila mwezi TRA imekuwa ikitangaza kiasi cha fedha kilichokusanywa kutoka katika vyanzo vilivyoainishwa.

Katika kuhakikisha fedha zinakusanywa, TRA imekuwa ikitumia njia mbalimbali kuwafuatilia walipakodi kutekeleza wajibu wao na wakati mwingine hutoza faini kwa wale wanaochelewa. Kuna wakati pia mamlaka hiyo imekuwa ikitumia hata vikosi kazi vinavyohusisha polisi katika kudai kodi kwa wale wanaoshindwa kutekeleza wajibu wao kama ilivyoainishwa kwenye sheria.

Kuna wakati mamlaka hiyo imekuwa ikilalamikiwa juu ya matumizi ya nguvu katika kudai kodi pamoja na baadhi ya maofisa wake kuwabambikia kodi wafanyabiashara hatua ambayo hutengeneza mazingira ya rushwa kwa watumishi hao wa taasisi nyeti kwa maendeleo ya taifa. Hata hivyo kuna habari njema kwamba hivi karibuni ilitangaza kuacha kutumia vikosi kazi katika kukusanya kodi.

Pamoja na mambo hayo, kumekuwa na malalamiko kutokana na mfumo wa TRA kuwatoza kodi watu wanaoanza kufanya biashara kuwa hatua hiyo ni kuchukua sehemu ya mtaji wa kuanzisha shughuli. Jambo hilo pia lilijitokeza katika ziara ya Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana mkoani Mbeya baada ya wajasiriamali kulalamikia hilo.

Ni dhahiri kwamba kunapokuwa na mazingira rafiki katika jambo lolote lile kunakuwa na mafanikio, ikiwamo makusanyo ya serikali kama TRA itakuwa na uhusiano mzuri na walipakodi.

Kwa mantiki hiyo, TRA inapaswa kuwalinda wafanyabiashara kwa kuweka mazingira bora na rafiki ili wafanye shughuli zao na hatimaye kukuza biashara ambazo zitawezesha kuwapo kwa makusanyo mengi.

TRA, kwa mantiki hiyo, inapaswa kukaa na wadau kama vile sekta binafsi kupitia Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye viwanda na Kilimo (TCCIA), Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TaBWA) na kuainisha mambo ambayo ni kikwazo katika ulipaji kodi na ufanyaji biashara kwa ujumla.

Jambo la msingi ni kwamba TRA isikilize kero za wadau na kuzifanyia kazi. Mazingira bora na rafiki yatawezesha kupatikana kwa makusanyo ya kutosha yatokanayo na serikali na hatimaye miradi mingi ya maendeleo kutekelezwa kwa kasi zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Halfani Chusi

## Muungwana Lazima Nilonge

# Uchafuzi mitaro unaofanywa makusudi ni wakati sasa udhibitiwe kwa nguvu zote

**JIJI** la Dar es Salaam na mikoa mingine, kumefanyika ukarabati wa barabara na kwa kiasi kikubwa, ni pamoja na kuweka mitaro kwenye barabara.

Ni jambo zuri na kitu kinachovuta taswira halisi ya namna barabara zinavyotakiwa kuwa hii si kwa Tanzania pekee, bali hata nchi za nje pia wanatumia mfumo huo.

Mfumo huo ni mahususi kabisa kwa kupitisha maji yanayotokana na mvua na wakati mwingine shughuli za kibinadamu kama kumwaga maji taka ili yapite humo kwenda mahali husika.

Katika uchunguzi nabaini baadhi ya wakazi wamekuwa wakichafua mitaro hiyo, kitu ambacho kimetajwa kuwa ndio sababu ya kuongezeka ya mbu na kuiweka jamii katika hatari ya kupata magonjwa mbalimbali yanayotokana na uchafuzi wa mitaro.

Uchafuzi unaofanywa na wakazi kama ulivyonaswa na mwandishi wa makala hii unaonyesha baadhi ya wakazi wanatupa vitu visivyo stahiki kwenye mitaro ikiwamo taka ngumu, hali inayosababisha mitaro kushindwa kupitisha maji na kupelekea kutuama.

Wengi wao wanatupa chupa za maji, rambo, pamoja na karatasi za kufungia chipsi kitu ambacho ni hatari kwa uhifadhi wa mitaro ya kupitishia maji kwa sababu vile si vitu vya kuyeyuka na maji.

Maeneo ya Tandale na Manzese kumekuwapo na kasumba hiyo, baadhi ya watu wakilifanya hilo kwa kujua na kutojua hali ambayo wakazi wa mitaa hiyo wanaitaja kuwa ndio sababu ya kuzuka kwa mazalia ya mbu kwa kiasi kikubwa.

Kama ilivyo kawaida mbu hupenda kuzaliana zaidi wanapokuwa kwenye maeneo ambayo kuna madimbwi ya maji, na kwenye mazingira machafu.

Nyumba nyingi maeneo hayo zimejengwa kufuata barabara na mitaro ipo pembezoni ya barabara kwa ajili ya kupitisha majitaka kwa muktadha huo mbu lazima wanapotoka kwenye mitaro wataingia kwenye nyumba.

Lakini kama utunzaji wa mitaro hiyo ungepewa kipaumbele maji yakapita bila kutuama sehemu kusingekuwa na shida kwa sababu mbu wangekosa mahali pakuweka makazi na hivyo kusingekuwa na adha hiyo.

Jamii inapaswa kujikita katika kutunza mitaro kushiriki kuangamiza vyanzo vya mazalia ya mbu ili kuepukana na magonjwa ambayo yanaweza kusababishwa na uchafuzi wa mazingira.

Ikumbukwe kuwa, uchafuzi wa mitaro hausababishi mazalia ya mbu pekee bali ni chanzo cha uchafuzi wa hali ya hewa kwa sababu kama mitaro ikiwa michafu lazima itatoa harufu mbaya.

Pia ni chanzo cha kuficha wadudu hatari kama nyoka na panya, ni dhahiri kwamba wadudu hao ni rafiki wa mazingira machafu nyoka na panya hupendelea kukaa zaidi kwenye mazingira hayo.

Jambo la kuzingatia ni kwamba jukumu la kutunza mazingira si la serikali pekee, hili ni suala mtambuka ambalo jamii kwa ujumla tunapaswa kulibeba watu wengi wamelemaa na kuona kila kitu kinatakiwa kufanywa na serikali kitu ambacho sio kweli.

Jambo la kufurahisha zaidi siku chache zilizopita nimeona serikali kupitia mamlaka husika ikiendelea na kazi ya kusafisha mitaro iliyoko kando ya barabara.

Jambo ambalo walinieleza baadhi ya wasafishaji wa mitaro hiyo ambalo sikufurahiswa nalo, ni ile tabia ya wale wanaotumia mitaro hiyo kupitisha maji taka yaliyo changanyikana na kinyesi, hawa huwa wanategea kipindi cha mvua baada ya hapo wanaelekeza maji taka kwenye mitaro.

Huu wote ni uchafuzi wa mitaro serikali inapaswa kuweka mikakati kuwashughulikia watu wa namna hii, ikiwa ni pamoja na kutoa adhabu kali kwa wote watakao kutwa na hatia hiyo.

# Makalla awageukia maofisa mgogoro ardhi

**Na Faustine Feliciane**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amesema mgogoro wa ardhi unaoendelea Kimbiji, Manispaa ya Kigamboni, umetengenezwa na wataalamu wa ardhi wa manispaa hiyo.

Akizungumza baada ya ziara kukagua maeneo yenye mgogoro wa barabara, Makalla alisema, picha aliyoipata ni wataalamu wa Idara ya Ardhi wahusika waliotoa hati za viwanja kwenye maeneo hayo.

"Kuona ni kuamini nimesikia mengi sana yakisemwa kuhusu mgogoro huu, nimekuja mwenyewe nimejionea, ni wazi baada ya kusikia pande zote na vielelezo wataalamu wetu wa ardhi ndio wametufikisha hapa," alisema Makalla.

Aidha, alisema busara pekee ndio inaweza kuumaliza mgogoro huo uliodumu muda mrefu.

"Atoa siku saba Manispaa mumtafute huyu mwekezaji ASM pamoja na walalamikaji wa hii barabara tukae kikao cha pamoja ambacho mimi mwenyewe nitakiendesha tutafute suluhu ya hili jambo, kwani kuna shida gani huyu ASM akiamua kuvunja ukuta kuruhusu barabara ipite, ni busara tu? Nipo tayari kuvunja ratiba ya siku nzima kukaa kwenye hicho kikao," alisema Makalla.

Mgogoro huo ulioanza mwaka 2015 umetokana na mwekezaji huyo kuziba barabara inayotumiwa na wananchi na wawekezaji wengine kufika kwenye maeneo yao na pwani ya bahari.

ASM anamiliki viwanja viwili pacha vilivyotenganishwa na barabara inayoelekea kwenye viwanja vya wawekezaji wengine.

Kabla ya kufanya ziara kwenye maeneo hayo ya mgogoro, uamuzi uliotolewa na Wizara ya Ardhi kuitaka Manispaa ya Kigamboni kufanya tathmini na kumlipa fidia mwekezaji ASM, ili kuruhusu barabara hiyo kutumika, ASM itakiwa kulipwa Sh. milioni 126.

Hata hivyo, kikao cha kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo kilitoa uamuzi mwingine wa kuchukua sehemu ya viwanja vya wananchi na kuwalipa fidia kupisha barabara mchepuko.

Mmoja wa wakazi ambaye shamba lake linatakiwa kumegwa kwa ajili ya barabara, Mwinyipingu Mbwana, alisema tayari uamuzi wa kumlipa mwekezaji ASM ulishafanyika na tathmini ilifanyika sasa wanashangaa manispaa kuja na uamuzi mpya.

"Tunakushuru sana Mkuu wa mkoa kwa kuja kujionea mwenyewe na bahati nzuri mwenyewe umekiri kuwapo kwa madudu kwa wataalamu wetu, tunaomba kama ulivyoahidi utusaidie kuumaliza mgogoro huu," alisema.

Pia Mwenyekiti wa Kijiji cha Mikenge ulipo mgogoro huo, Lameck Mayala, alisema viongozi wa manispaa hiyo wamechochea kwa kiasi kikubwa kwa kupindisha ukweli juu ya barabara hiyo.

## Polisi atoa ushahidi alivyoshindwa kukipata kisu kilichotumika kuua

**Na Grace Gurisha**

MPELELEZI wa Jeshi la Polisi, Mussa Degesho, ameieleza Mahakama kuwa hadi sasa hajakipata kisu kilichotumiwa na mshtakiwa Silas Tugala, kumuua shemeji yake Peter Elias.

Shahidi huyo wa Jamhuri amedai kuwa sababu ya kutokukipata ni mshtakiwa alipokamatwa alionekana akimpatia mtu ambaye hakufahamika.

Peter anadaiwa kuuawa kwa kuchomwa kisu na shemeji yake, Tugala, wakati alipokwenda kusuluhisha ugomvi wa wanandoa hao nyumbani kwao.

Degesho alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Susan Kihawa wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkuu, wakati akitoa ushahidi dhidi ya Tugala anayedaiwa kumuua Peter Januari 19, 2017 eneo la Mbezi Juu, Dar es Salaam.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Michael Shindai, Degesho alidai wakati anafanya upelelezi alielezwa na mashuhuda kuwa walimwona Tugala akitoka nyumbani kwake akiwa na kisu mkononi baada ya mauaji kufanyika.

Akijibu swali la Shindai kuhusu wapi kisu kiliko, Degesho alidai kuwa kisu hakipo mahakamani wala polisi kwa sababu mshtakiwa baada ya kufanya tukio, alitoka nacho nje. Alidai mshtakiwa alipokamatwa eneo la Hospitali ya Mwananyamala, alikokwenda kupata matibabu baada ya kutokea ugomvi baina yake na mashemeji zake wawili, wakati yuko ndani ya gari alionekana akimpa kisu mtu aliyekaa kiti cha nyuma cha gari.

"Kutokana na mshtakiwa kutokutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi, hatukuweza kumpata mtu ambaye alimpa kisu alichofanyia mauaji kwa sababu yeye ndiye anamfahamu," alidai Degesho.

Degesho alidai kuwa mshtakiwa alipofikishwa kituo cha polisi, inasemekana mtu aliyepewa kisu hakuingia ndani ya kituo bali aliishia nje na kuondoka, hivyo yeye kama mpelelezi hakumpata.

Kutokana na hali hiyo, inadaiwa mshtakiwa baada ya kufanya mauaji hayo eneo la Mbezi Juu ndani ya Wilaya ya Kinondoni, alitoka na kisu hicho hadi Hospitali ya Mwananyamala.

Alidai kuwa wakati anamfanyia mahojiano, mshtakiwa alikataa kufanya tukio hilo lakini kutokana na upelelezi alioufanya na vielelezo alivyokusanya, Tugala ndiye aliyeua.



Mwakilishi wa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ambaye pia ni Mkurugenzi wa TEHAMA, Emmanuel Nnko (kushoto), akikabidhi tuzo ya mshindi wa kwanza wa jumla kwa walipa kodi wa kati wa ndani kwa Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa CPS, Katrin Dietzold, katika hafla ya kuwashukuru walipa kodi mjini Zanzibar jana. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji CPS, Sebastian Dietzold. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mama, watoto wawili wateketea kwa moto wakiwa wamelala

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MAMA na watoto wake wawili, wakazi wa Mtaa wa Igomelo, Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wamefariki dunia kwa kuungua na moto wakiwa wamelala.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo jana majira ya saa 11:00 alfajiri, kwa wanafamilia hiyo kuteketea kwa moto.

Aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Doto Juma (32), na watoto Samson Mathayo (13) mwanafunzi wa darasa la sita na Joseph Samson mwanafunzi wa darasa la pili katika Shule ya Msingi St. Antony of Padua.

Kamanda Magomi alisema chanzo cha moto huo hakijajulikana na kwamba wakati tukio linatokea baba wa familia, Mathayo Samson, hakuwapo.

"Jeshi la Zimamoto (na Uokoaji) lilifika na kushirikiana na polisi pamoja na wananchi kuwaokoa lakini hawakufanikiwa," alisema Magomi.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, alisema wananchi na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilijitihadi kuwaokoa lakini halikufanikiwa kwa kuwa moto ulishawazingira.

## KABWELA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA

## TAARIFA KWA UMMA

### BEI ELEKEZI KWA MBOLEA ZA KUPANDIA NA KUKUZIA KWA MSIMU WA KILIMO 2022/2023

**1.0 UTANGULIZI**
Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (Tanzania Fertilizer Regulatory Authority - TFRA) kwa niaba ya Wizara ya Kilimo ina jukumu la kutoa bei elekezi ya mbolea ambapo wafanyabiashara wa mbolea wanatakiwa kuuza kwa bei elekezi au chini yake. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 4(1)(u) cha Sheria ya Mbolea ya Mwaka 2009 na Kanuni ya 56 ya Kanuni za Mbolea za mwaka 2011 kama zilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2017.

Katika kutekeleza jukumu hilo la kisheria, TFRA imefanya mapitio ya bei elekezi kwa mbolea ya DAP na UREA katika kila kituo cha mauzo ambazo zitaanza kutumika tarehe 01 Desemba, 2022 (Bei zinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Kilimo, tfra na katika ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa Tanzania Bara). Lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha kuwa mbolea inauzwa nchini kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia tasnia ya mbolea.

**2.0 MJENGEKO WA BEI ELEKEZI**
Kwa kuwa mbolea za DAP na Urea zinazotumika nchini huingizwa kutoka nje ya nchi, na kwa kuwa Mamlaka imeratibu uingizaji wa mbolea hizo kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja (BPS), mapitio ya bei elekezi yamezingatia bei za zabuni, gharama za kuondosha mzigo bandarini na kusambaza hadi kumfikia mkulima. Hivyo, gharama za mjengeko wa bei elekezi ni kama ifuatavyo:
-
i. Bei ya kufikisha mbolea hadi bandari ya DSM (CIF);
ii. Tozo za Mamlaka ya Bandari (TPA) na taasisi mbalimbali za udhibiti, gharama za kuondosha mzigo, vifungashio, kufungasha, usafirishaji hadi kwenye ghala la mwingizaji na kuhifadhi;
iii. Gharama za usimamizi na faida ya mwingizaji;
iv. Gharama za usafiri hadi kwa muuzaji wa rejareja na faida ya mfanyabiashara.

**3.0 BEI ZA MBOLEA YA RUZUKU KWA WAKULIMA**
Serikali imeelekeza aina moja ya mbolea kuuzwa kwa bei inayofanana kwa wakulima nchini kote (pan territorial pricing). Hivyo, mapitio ya bei elekezi hayana athari kwenye bei ya mkulima ambapo mbolea ya DAP itaendelea kuuzwa kwa TZS 70,000, na Urea TZS TZS 70,000 baada ya kuweka ruzuku ya Serikali. Aidha, hakuna mfanyabiashara atakeye ruhusiwa kuuza mbolea nje ya mpango wa ruzuku. Hivyo, tofauti kati ya bei elekezi kwa kila eneo na bei ya mkulima italipwa na Serikali kama ruzuku kwa mkulima.

**USIMAMIZI WA BEI ELEKEZI**
Kwa kuwa mbolea zote zinauzwa katika mpango wa ruzuku, Serikali kupitia TFRA imesajili waingizaji na wazalishaji wa mbolea pamoja na mawakala wanaosambaza na kuuza mbolea kwa wakulima na kuwapa namba maalum za utambulisho. Hata hivyo, ili azma ya Serikali itimie ni muhimu kwa Mamlaka zote husika katika ngazi za Mkoa, Wilaya na Halmashauri kuhakikisha kuwa kila duka la pembejeo linabandika namba ya uwakala na bei elekezi sehemu zinazoonekana kwa urahisi kwa wanunuzi. Pia ni vema mamlaka hizo zikasimamia kwa karibu utekelezaji wa mpango wa ruzuku ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kuhusu uzingatiaji wa bei za mbolea ya ruzuku na upatikanaji wa mbolea kwa wakulima katika maeneo husika.

**4.0 UDHIBITI WA UTOROSHWAJI WA MBOLEA NJE YA NCHI**
Pamoja na kwamba mpango wa ruzuku ya mbolea ni neema kwa wakulima, wafanyabiashara wachache wasio waaminifu wanaweza kutumia fursa hiyo kuwalaghai wakulima na kununua mbolea kwa majina yao na baada ya hapo kutorosha mbolea kwenda nchi jirani. Hali hii itahatarisha utoshelevu wa mbolea kwa wakulima wetu na pia kuingizia hasara Serikali katika fedha inazotoa kama ruzuku kwa lengo la kumnufaisha mkulima na kuongeza uzalishaji nchini. Pamoja na uelimishaji ambao Serikali inaendelea kuufanya, ni vyema Mamlaka zote za Serikali zikashirikiana na wadau wote hususan katika mikoa ya mipakani kama Songwe, Rukwa, Katavi, Kigoma, Kagera, Kilimanjaro, Arusha na mikoa mingine kuhakikisha mbolea ya ruzuku haitoroshwi kwenda nchi jirani.

Vilevile, natoa onyo kali kwa wafanyabiashara wachache wenye tabia hizo au mpango wa kutorosha mbolea ya ruzuku kwenda nchi jirani kutothubutu kufanya hivyo kwani hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao pindi itakapothibitika. Aidha, endapo kutakuwa na haja ya wafanyabiashara kuuza mbolea nje ya nchi, basi wafanye hivyo kwa kuzingatia sheria za nchi na sio kutorosha mbolea ya ruzuku.

**5.0 HITIMISHO**
Ni matumaini ya Serikali kuwa, mpango wa ruzuku ya mbolea utawezesha wakulima kutumia mbolea zaidi na hivyo kuongeza uzalishaji na tija kwa ajili ya utoshelevu wa chakula na kuzalisha malighafi ili kuimarisha uchumi wa viwanda. Hivyo, niwakumbushe wataalam na wadau wa kilimo kuendelea kutoa ushirikiano wa dhati katika kuwaelimisha wakulima juu ya matumizi sahihi ya mbolea na pembejeo nyingine za kilimo. Aidha, natoa wito kwa Mamlaka zote katika ngazi za mikoa, Wilaya na Halmashauri kutoa ushirikiano katika usimamizi wa mbolea ya ruzuku ili Serikali ifikie azma yake na pia mkulima aweze kutumia fursa hii kubadilisha maisha yake kupitia kilimo.

**Dkt. Stephan E. Ngailo**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**Novemba 30, 2022**

17173702

# Jaji ataka huduma ziakisi ubora majengo

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

JAJI Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Morogoro, Paul Ngwembe, amewataka watumishi wa mahakama za wilaya 18 zilizopata majengo mapya, kutoa huduma bora kwa weledi na uaminifu ili kuendana na uzuri na hadhi ya majengo yaliyozinduliwa na Jaji Mkuu hivi karibuni.

Akizungumza na watumishi hao juzi, alipokuwa akifungua mafunzo ya huduma kwa mteja kwa watumishi wa mahakama za wilaya mpya 18 kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki, mjini hapo na washiriki wengine kutoka vituo vingine vya Kigoma, Bukoba na Musoma walioshiriki kwa njia ya mtandao, Jaji Ngwembe amesema ni matarajio ya Mahakama ya Tanzania kuwa uboreshaji wa miundombinu ya Mahakama utakwenda sambamba na utoaji huduma bora kwa wananchi.

"Ni matarajio yangu na ya Mahakama kwa ujumla kwamba, baada ya mafunzo haya kila mshiriki atakuwa ameiva kwa kubadilika kifikra, kimtazamo na weledi na hivyo kuachana na utendaji wa kimazoea ambao ulichangia wananchi kukosa imani dhidi ya huduma zetu," alisema.

Jaji Ngwembe aliongeza kuwa kila mtumishi wa mahakama ana wajibu na jukumu la kuunga mkono jitihada kubwa zinazochukuliwa na mahakama katika kuboresha utendaji unaozingatia matokeo katika majengo mapya na mifumo ya TEHAMA iliyosimikwa kwenye miundombinu hiyo ya kisasa.

"Kwa kipindi kirefu mtakumbuka, Mahakama ya Tanzania imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya majengo, ukosefu wa majengo mapya, sambamba na uchakavu mkubwa wa miundombinu ya majengo ya Mahakama iliyoko sasa katika ngazi mbalimbali kote nchini. Ni kutokana na sababu hizo, ndio maana mahakama imejiwekea utaratibu wa kujenga majengo mapya na kukarabati majengo yaliyoko kuanzia mahakama za mwanzo mpaka mahakama kuu, kwa kutumia vizuri fedha tunazopata kutoka serikalini na mikopo ya wafadhili," alisema.

Ngwembe amesema kwamba, mafunzo hayo ni moja ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Mahakama wa mwaka 2020/21 - 2024/25 pamoja na Mpango Maalumu wa Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama wa Miaka Mitano wa mwaka 2021/22 - 2025/26.

Naye Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Beatrice Patrick, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwakumbusha na kuwawezesha watumishi wa mahakama hizo namna bora ya kutoa huduma nzuri kwa wateja wanaofika kupata huduma katika mahakama hizo.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, mafunzo haya yamepangwa kufanyika katika vituo vinne ambavyo vinajumuisha mahakama zilizozinduliwa na ziko karibu karibu ili kupunguza gharama ya kutokulazimika kufika kila kituo. Vituo vitakavyoendesha mafunzo haya ni Morogoro IJC, Kigoma, Musoma na Bukoba.

Novemba 25, mwaka huu, Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, alizindua Mahakama ya Wilaya Busega iliyowakilisha mahakama zingine mpya za wilaya mpya 17.

Mahakama hizo zilizojengwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia ni za Butiama, Rorya, Songwe, Gairo, Mkinga, Mvomero, Kilombero, Mbogwe, Nyang'hwale, Kyerwa, Itilima, Missenyi, Kaliua, Uvinza, Buhingwe, Kakonko na Tanganyika.

## Wahasibu watakiwa kutumia TEHAMA

**Na Joseph Mwendapole**

WAHASIBU na wakaguzi wa hesabu nchini wameshauriwa kuzingatia matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ili kwenda na wakati.

Ushauri huo ulitolewa jana Dar es Salaam na Waziri Nchi Ofisi ya Rais Ikulu Zanzibar, Jamal Kassim Ali, wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka 50 tangu kuanzishwa kwa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA), yaliyofanyika Bunju.

Alisema NBAA imejitahidi kufanya maboresho makubwa ya matumizi ya TEHAMA na ni dalili njema ya matayarisho ya kupokea na kuendeleza matumizi ya teknolojia hiyo ndani ya taaluma hiyo ya uhasibu.

"Kwa dunia ya leo uhasibu bila TEHAMA ni bure ndiyo maana nawapongeza NBAA mwendeleze maboresho haya kwenye mifumo yenu ya usajili na ukusanyaji wa mapato ili kurahisisha utoaji wa huduma na kwenda kisasa zaidi," alisema Waziri.

Aidha, aliitaka NBAA kuwa karibu na serikali hasa uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao (e-GA) ili kuwajengea uwezo wa kutumia viwango na miongozo katika hatua za kupanga, kuanzisha na kutekeleza jitihada za serikali mtandao.

Waziri aliwataka pia wahasibu kuzingatia maadili katika kazi zao za kila siku na kuheshimu taratibu za kihasibu pamoja na kuheshimu sheria za nchi kwa kutambua kuwa miongoni mwa yanayodhoofisha maendeleo ni vitendo vya rushwa, ubadhirifu, uzembe, kutowajibika na ukiukwaji wa maadili.

Waziri alisema taarifa za fedha zimekuwa zikiwasilishwa kwa wakati ikiwa ni miezi mitatu tu baada ya mwaka wa fedha kwisha kwa kufuata sheria ya fedha.

Hata hivyo, alisema kwa sekta ya umma ukaguzi wa ndani haujafanya vizuri kwani kama ukaguzi ungefanywa vizuri kusingekuwa na hoja nyingi za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Aidha, Waziri alisema wakaguzi wa ndani ndio wenye uwezo wa kuzuia wizi na ubadhirifu wa fedha kwasababu ndio wanafanya ukaguzi mara kwa mara tofauti na CAG anayekuja kufanya ukaguzi wakati matukio ya ubadhirifu yameshatokea.

# Wanafunzi waungana kupinga ukatili kijinsia

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WANAFUNZI wa shule za msingi jijini Mbeya, zikiwamo Meta, Simike na Muungano, wameungana na Asasi ya Sauti ya Mama Afrika Foundation (SAMAFO) kupinga ukatili wa kijinsia.

Waliungana na shirika hilo wakati huu wa maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, huku Mkurugenzi Mtendaji wa SAMAFO, Tabitha Bugali, akiitaka jamii kutofumbia macho vitendo hivyo.

Akielezea maadhimisho hayo, Bugali alisema yalianza Novemba 25 na yatahitimishwa Desemba 10, mwaka huu, na kwamba shirika hilo litatoa elimu shuleni pamoja na kushirikisha wanajamii.

Mkurugenzi Mtendaji huyo alisema elimu ya kupinga ukatili huo imeanzia katika shule za msingi na kushirikisha wadau wengine, wakiwamo madereva wa bodaboda, na kwamba wamashaitoa katika shule za msingi Mlimani na Sinde pia itafika sekondari ya Mabatini.

"Huu ni mwendelezo kupinga ukatili waliofanyiwa masista watawa, huko Colombia, mwaka 1960 ambao walikuwa wanaharakati wakipinga vitendo vya ubakaji, waliuawa kikatili," alisema Bugali.

Alisema baadaye mwaka 1999, Umoja wa Mataifa (UN), uliridhia kuwa ni vyema hizo siku zikaendelezwa, na kwamba Tanzania ikaridhia na kufanya maadhimisho hayo kila mwaka.

"Katika harakati hizi, tumebaini vitendo vingi vya ukatili, vinatokea ndani ya familia na kuhusisha ndugu, ila taarifa zinafichwa, ili kuwafanya wahusika wasichukuliwe hatua za kisheria. Hii si sahihi," alisema.

Kwa mujibu wa Bugali, watatumia siku hizo 16 kuhakikisha wanazitumia pia kuelimisha umoja wa wawaendesha vyombo vya usafiri kama vile madereva wa bodaboda, bajaj na hata viongozi wa dini.

"Katika siku 16 tunasema, pinga ukatili okoa maisha. Kila jamii ikatae, kama mimi sipendi mtoto wangu abakwe, alawitiwe, kwa nini nikamfanyie mtoto wa mwenzangu?" Alihoji.

Ofisa Msaidizi wa Kituo cha Msaada wa Sheria cha Mbalizi, Sara Mwanachimbo, alisema elimu hiyo hiyo ya kupinga ukatili wa kijinsia imekuwa ikifika zaidi mijini kuliko vijijini.

Alisema vitendo hivyo vimekithiri zaidi vijijini, na kwamba sababu ni kutowafichua watuhumiwa wa vitendo hivyo ni rushwa ili kumalizana au familia kuogopa suala hilo kufahamika kwenye jamii.

Mwanafunzi wa darasa la tano katika shule ya msingi Muungano, Furaha Mohamed, alisema ukatili ni vitendo vibaya vinavyotakiwa kukemewa, katika jamii na kwamba watoto wanapokumbwa na matukio hayo, watoe taarifa kwa walimu, walezi na wazazi, ili kuondoa matendo hayo kwenye jamii.

# Makinda kutunuku wahitimu 291 Kairuki

**Na Mwandishi Wetu**

SPIKA Mstaafu ambaye ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), Anne Makinda, anatarajiwa kuwatunuku wahitimu 291 wa ngazi mbalimbali kwenye mahafali ya 20 ya chuo hicho.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Yohana Mashalla, alisema jana kuwa mahafali hayo yatakayofanyika Jumamosi na yatatanguliwa na kusanyiko la wahitimu (convocation) kesho na mgeni rasmi atakuwa Balozi wa Marekani nchini.

Alisema kauli mbiu ya kusanyiko la wahitimu mwaka huu ni "Kukuza Ubunifu Katika Kuimarisha Mifumo ya Afya" na kuongeza kuwa kwenye tukio hilo, wanafunzi waliofanya vizuri katika mitihani yao watapewa zawadi mbalimbali.

Kuhusu mahafali, alisema yatahudhuriwa pia na Mwenyekiti wa Mtandao wa Elimu na Afya Kairuki (KHEN), Kokushubira Kairuki na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo cha Kikuu, John Ulanga, viongozi wa serikali katika ngazi mbalimbali, wadau wa maendeleo na wageni waalikwa.

Alisema kwenye mahafali kutakuwa na wahitimu 291 wakiwamo wanawake 170 na wanaume ni 121.

Prof. Mashalla alisema wahitimu 54 watatunukiwa stashahada ya uuguzi, 10 stashahada ya ustawi wa jamii, 38 shahada ya uuguzi na 177 shahada ya udaktari wa binadamu wakiwamo wanawake ni 97 na wanaume ni 80.

Kwa mujibu wa Prof. Mashalla, kwenye mahafali hayo, wahitimu 12 watatunukiwa shahada za uzamili kati yao 10 katika tiba ya binadamu na afya.

Alisema mwanamume mmoja atatunukiwa shahada ya uzamili ya upasuaji na mwanamke mmoja atatunukiwa shahada ya uzamili ya sayansi ya afya ya jamii.

"Nawapongeza wahadhiri, maprofesa pamoja na watumishi wote wa HKMU kwa kazi kubwa na nzuri waliyofanya kuwalea na kuwafundisha wahitimu wote wanaotarajiwa kutunukiwa shahada zao Jumamosi," alisema Prof. Mashalla.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya KCB, John Ulanga (kushoto), akipokea zawadi kutoka kwa Mwanzilishi wa Taasisi ya Pink Hijab Initiative, Khadija Omar, wakati wa kongamano la wanawake lililojadili kuhusu umuhimu wa wanawake kwenye sekta ya utalii nchini, lililojulikana 'Sneakers and Heels', jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# KKKT yawafunda wanaume kuwajibika kifamilia

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WANAUME wilayani Masasi mkoani Mtwara, wamehimizwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu kwa kuthamini, kuheshimu ndoa zao na kutimiza mahitaji ya msingi kama viongozi wa familia.

Wito huo ulitolewa juzi mjini hapo na Msaidizi wa Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kusini Mashariki, Mchungaji Yeriko Ngwema, wakati akizungumza na waumini wa kanisa hilo katika sherehe ya siku ya wanaume.

Alisema vitabu vya Mungu vimemtaja mwanamume kuwa ni nguzo ya familia na ndio kiongozi mkuu katika kuendesha familia na kuipatia mahitaji yote ya msingi ambayo familia inahitaji kuwanayo.

Mchungaji Ngwema alisema uimara wa familia pamoja na ndoa unatokana na ushupavu wa mwanamume katika kuongoza familia yake, ikiwa ni pamoja na kuhudumia mahitaji ya msingi kikamilifu na kwa wakati.

Alisema lengo la kuadhimisha siku ya wanaume wa kanisa hilo ni kuwaunganisha na kuwapa elimu namna ya kutambua kuongoza familia pamoja na kutimiza mahitaji yote ya msingi.

Mchungaji Ngwema alisema siku ya wanaume iwe somo muhimu kwa wanaume wote nchini, ikiwa ni pamoja na kufahamu umuhimu wao ndani ya familia na kuwa na upendo na wake zao hatua hiyo itasaidia kupunguza mtafaruku kwenye ndoa na hatimaye kujenga ndoa yenye upendo.

Kwa mujibu wa mchungaji huyo, iwapo ndani ya familia kukiwa na upendo wa pande zote, baraka za Mungu ndani ya ndoa hiyo inakuwa ni kubwa na maendeleo yanapatikana kwa haraka.

Ngwema alisema kupitia sikukuu hiyo ya wanaume pia wanaume hao wamepata fursa ya kufanya mafunzo ya wiki moja mafunzo yaliyolenga kuwajengea uwezo wa kuwa na upendo na amani katika familia zao.

Alisema upendo ndio nguzo ya amani katika familia na imani, upendo na utulivu vyote vinapaswa kuzingatiwa na mtu pekee ambaye anatakiwa kuonyesha ni mwanamume kwa sababu yeye ndiye kiongozi wa familia.

Mkuu wa Jimbo la Magharibi Masasi, Mchungaji Kastory Kiulaumagulu, aliwapongeza wanaume wa kanisa hilo kwa kufanya sikukuu hiyo ili jamii kuwa na mahusiano mazuri ndani ya familia.

# NIT, DMG zakubaliana kuzalisha wataalamu

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimeingia makubaliano na Kampuni ya Dar es Salaam Merchant Group (DMG) kushirikiana kuzalisha wataalamu wabobezi katika sekta ya usafiri na usafirishaji hususani kwenye eneo la ujenzi na usanifu wa meli.

Wakizungumza na waandishi wa habari baada ya kutia saini makubaliano hayo jijini Dar es Salaam juzi, Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa, na Mkurugenzi Mtendaji wa DMG, Rayton Kwembe, walisema makubaliano hayo yatasaidia kuboresha taaluma katika eneo la uchumi wa buluu.

Prof. Mganilwa alisema kupitia makubaliano hayo, DMG itatoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa NIT, hivyo kuhitimu kama wataalamu wabobezi kwenye sekta nyeti ya usafiri na usafirishaji.

"Madhumuni makuu ya makubaliano haya ni kuimarisha uhusiano kati ya NIT na DMG katika kuboresha ujuzi kwa wanafunzi na wafanyakazi katika maeneo ya usafiri wa maji.

"Tumeingia makubaliano katika maeneo kadhaa yakiwamo mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi, mafunzo kwa wafanyakazi, kubadilishana utaalamu, ziara za mafunzo ama masomo na vilevile kukuza uhusiano kwa wafanyakazi," alisema.

Mkuu wa Chuo aliyataja maeneo mengine ya ushirikiano katika mkataba huo kuwa ni utafiti na ushauri.

"Wataalamu kutoka DMG watashiriki katika programu za mafunzo katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji," alisema.

Kwembe alisema: "Katika makubaliano haya, kampuni yetu imekubali kutoa nafasi za mafunzo kwa vitendo ikiwa ni pamoja na kutoa fursa za ziara za masomo na uhusiano kwa wafanyakazi na wanafunzi. Kwembe aliongezea kuwa makubaliano hayo ni ya miaka mitano na wanafunzi na wakufunzi kutoka NIT watapata fursa ya kujifunza ujenzi wa meli na ukarabati wake.

"Kampuni yetu inafanya miradi mbalimbali ikiwamo ya ujenzi na ukarabati wa meli, hivyo wanafunzi na wakufunzi wataweza kujifunza kwa vitendo jinsi ya kujenga na kukarabati meli," alisema.

Alisema kwa sasa Tanzania haina wataalamu wa kutosha katika ujenzi na ukarabati wa meli, hivyo wataalamu wengi wa eneo hilo wanachukuliwa kutoka Korea na China.

"Tumekuwa tukiajiri wafanyakazi wengi kwenye ujenzi wa meli kutoka nje ya nchi, hii ni kutokana na sababu kubwa ambayo ni ukosefu wa vijana wa kitanzania wenye ujuzi katika eneo hili," alisema. Alisisitiza kuwa kupitia makubaliano hayo, ana imani baada ya miaka michache ijayo, taifa litakuwa na wataalamu wengi wabobezi kwenye eneo hilo.

"Tunataka kuona miradi mingi ya ujenzi na ukarabati wa meli inasimamiwa na Watanzania, hivyo tutaweka juhudi kubwa kuhakikisha mkataba huu tulioingia unakuwa wenye tija kwetu sote na taifa kwa ujumla," alisema.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa kampuni yao inatoa zawadi kwa wanafunzi wa chuo hicho wanaofanya vizuri katika masomo yao na vile vile kuwapa ajira wahitimu hao.

"Kampuni yetu imeingia makubaliano ya ushirikiano na NIT katika maeneo mbalimbali ikiwamo utafiti, mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi na mafunzo ya uwezeshaji kwa watendaji," alisema.

Mkuu wa NIT alisema kuwa makubaliano ambayo taasisi yake imeingia na kampuni hiyo ya jijini Dar es Salaam ni sehemu ya kutimiza malengo ya Mradi wa Kujenga Ujuzi kwa Maendeleo na Uingiliano wa Kikanda katika Afrika Mashariki (EASTRIP).



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya ushauri wa masuala ya kodi ya RSK Consulting, Raymund Kahumba (wa pili kulia), na Mkurugenzi Mwenza wa Kampuni hiyo, Ezekiel Temu (kushoto), akizungumza na baadhi ya washiriki wa warsha kuhusu changamoto za uelewa wa masuala ya kodi kwa taasisi zisizojiendesha kibiashara, iliyoandaliwa na RSK jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanakijiji kukatiwa bima ya afya toka fungu la utunzaji wa misitu

**Na Christina Haule,** LINDI

WAKAZI 1,798 wa Kijiji cha Malolo, Ruangwa mkoani Lindi wanatarajia kukatiwa bima za afya (CHF) kutokana na Sh. milioni 49.8 zilizotolewa kama faida ya usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii (USMJ).

Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Malolo, Abdalah Lyuba, alisema hayo juzi wakati akisoma taarifa ya utekelezaji mradi wa kuhifadhi misitu kwa kuwezesha biashara endelevu ya mazao ya misitu Tanzania (CoForEST) kutoka mwaka 2021 walipoanza hadi mwezi Julai kwa mwaka wa fedha wa 2022/23 na kuuza mbao zilizowezesha kupata Sh. milioni 49.8.

Lyuba alisema kijiji hicho kina mwaka mmoja tangu kipate elimu ya kusimamia na kuhifadhi misitu ya kijiji na kwamba wamejipanga kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwamo ujenzi wa barabara za kuingia kwenye msitu ili kurahisisha biashara ya mbao na mkaa ambayo wakati mwingine hukosa masoko kutokana na jiografia ya kijiji hicho kuwa katika milima.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Wilbert Mwambe, alipongeza Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu (MJUMITA) na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kupitia ufadhili wa Shirika la Maendeleo na Ushirikiano Uswisi (SDC) kwa kuwapelekea mradi huo ambao husaidia kwa mwaka kukusanya mita za ujazo 30 hadi 40 za mbao huku wakiuacha msitu ukiendelea kuwa katika hali salama.

Alisema wanajishughulisha na uhifadhi wa misitu kwa kutumia eneo lenye ukubwa wa ekari 50 kupanda miti. Mwaka 2022 waliotesha miche 640 na kupanda miti 500.

Pia alisema mradi wa CoForEST uliwapatia mafunzo ya GPS ambayo yanawasaidia kuzuia na kuwakamata wahalifu wanaoingia msituni bila kuwa na kibali chochote kwa nia ya kutenda uhalifu.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2022 wamewakamata wahalifu watatu walioingia msituni bila vibali wala leseni za uvunaji mazao ya misitu, hivyo kuwafikisha polisi na hatimaye kupelekwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Naye mjumbe wa kamati ya mbao, Gerald Mwambe, aliziomba TFCG na MJUMITA kuwaongezea mwaka mmoja na kuwapatia elimu ya uvunaji endelevu mazao ya misitu sambamba na elimu ya kuwa na mashamba ya kudumu ili waepukane na kilimo cha kuhamahama kinachoharibu misitu.

Mwambe alisema jiografia ya kijiji hicho ni maeneo ya milimani na mawe yanayopoteza rutuba ya kilimo baada ya miaka mitatu tu ya misimu wa kilimo na kuwafanya kutafuta mashamba mapya ili wapate chakula na mazao ya biashara.

# Benki yadhamini maonyesho utalii

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imedhamini na kushiriki maonyesho ya utalii barani Ulaya yaitwayo My Tanzania Roadshows.

Maonyesho hayo yaliyofanyika kuanzia Novemba 12 -19 katika majiji manne barani Ulaya; Amsterdam (Uholanzi), Paris (Ufaransa), Cologne (Ujerumani) na Brussels (Ubelgiji) yalioandaliwa na kampuni ya KILIFAIR inajiyojishughulisha na uandaaji wa maonyesho na warsha mbalimbali ndani na nje ya mipaka ya Tanzania.

Maonyesho haya yalitoa fursa kwa kampuni za utalii, mamlaka za utalii na wadau wengine nchini kufungua milango ya ubadilishanaji uzoefu, kujifunza tamaduni mpya, kuonyesha bidhaa za kitalii na kutangaza vivutio vinavyopatikana Tanzania.

Akizungumza katika maonyesho hayo, Meneja Mwandamizi Malipo ya Kadi na Kidigitali wa Benki ya CRDB, Victor Makere, alisema kupitia maonyesho haya, benki yao ilitumia fursa hiyo kutoa huduma kwa wateja wake wa diaspora (kampuni na watu binafsi) waliopo barani Ulaya.

Alisema CRDB pia ilitumia jalada lake la wateja wa diaspora kutoa fursa ya kuhudumia wale wenye maono ya kutaka kuwekeza katika sekta ya utalii Tanzania

Makere alisema: "Kupitia maonyesho hayo tumeweza kukutana na wateja wetu katika sekta ya utalii ambao tumewawezesha na kuwajulisha juu ya njia za malipo zinazopatikana katika Benki ya CRDB ili kuwasaidia wateja kufanya malipo kwa urahisi pale wafikapo nchini.

"Kupitia ushiriki wetu katika maonyesho hayo, Benki ya CRDB inaunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kuutangaza utalii wa nchi kwa kusogeza karibu huduma za kibenki zenye mlengo wa kusaidia kufungua njia na kuwarahisishia wawekezaji wa sekta hiyo," alisema.



# RC aagiza kukamatwa wabunge, madiwani wachochezi

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, ameagiza kukamatwa wabunge na madiwani wa mkoa huo, wanaochochea kwa kuwashawishi wananchi kwenda kuvamia mashamba ya wawekezaji na kusababisha migogoro.

Amri ya Makongoro, inaakisi kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoitoa wiki iliyopita akiwa kwenye ziara ya kikazi mkoani humo.

Rais Samia aliwaonya wanasiasa wanaowachochea wananchi, wakihamasisha kuvamia ardhi iliyotengwa kwa ajili ya shughuli za umma, akisema hawana nafasi katika serikali yake.

Akizungumza katika kikao maalum cha kamati ya ushauri ya mkoa huo (RCC), Makongoro alisema anazo taarifa kwamba Diwani wa Maisaika, Wilaya ya Babati, Abdurahman Kololi, kuongoza baadhi ya wananchi kuvamia mashamba hayo, siku moja kabla ya ujio wa Rais Samia mkoani humo.

"RPC George Katabazi, wakamate madiwani na wabunge wanaoongoza makundi ya wananchi wanaovamia mashamba ya wawekezaji na kuwapeleka nahabusu ya magereza moja kwa moja kabla ya kuwafikisha mahakamani na kuwafungulia mashtaka.

"Nilipata taarifa za diwani huyo kwamba alifanya kikao na wananchi wanaodaiwa kuvamia mashamba ya wawekezaji na kuwaahidi kuwa atakutana na Rais (Samia), Novemba 22 jioni na kula naye chakula na atamweleza Mkuu wa Mkoa anavyowazuia kulima maeneo yao. "Tulipompokea Rais Samia Suluhu Hassan pale Bonga, niliongea na mtu wa itifaki nikamwonyesha diwani huyu kuwa akinyoosha mkono ampe kipaza sauti, bahati mbaya hakunyoosha na baadaye niliuliza mbona hukumpa, akaniambia hakunyoosha," alisema Makongoro.

Alisema licha ya Rais Samia na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, kutoa ufafanuzi kuhusu migogoro ya ardhi inavyosababishwa na wanasiasa, Mkuu huyo wa Mkoa, alisema anasikitishwa na namna diwani huyo na Mbunge wa Babati Mjini, Pauline Gekul, kuona wanaungana na wananchi wanaovamia Shamba la Dudumera na kumpiga vita mwekezaji huyo badala ya kufuata utaratibu.

"RPC nakuagiza fanya uchunguzi wako wa kipolisi kwa umakini ila usimuonee mtu kama ni diwani au mbunge, peleka magereza halafu mfungulie mashtaka.

"Tutachagua diwani mwingine hata kama ni Mwenyekiti wa Halmashauri, tutachagua mwingine."




Mratibu wa Mtandao wa vikundi vya wakulima Mkoa wa Manyara (MVIWAMA), Valentine Ngorisa, akizungumza kwenye mkutano mkuu wa 15 wa mtandao huo, Mjini Babati juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wasiojulikana wahujumu miundombinu mradi wa maji

**Na Dege Masoli,** KILINDI

WATU wasiojulikana wamehujumu, miundombinu ya maji ya Mradi wa Mgera AP, uliokuwa ukitekelezwa na Shirika la World Vision Tanzania katika Kata ya Saunyi, Wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga na kusababisha wananchi kukosa huduma hiyo. Mradi huo uliokuwa ukitekelezwa kwa zaidi ya Sh. milioni 300, umeng'olewa mabomba, koki za maji na mita za kuharibiwa, huku ukikosekana usimamizi madhubuti wa kamati iliyopewa jukumu la kuendesha.

Akizungumzia tatizo hilo, Meneja wa Mradi wa Mgera AP, Modest Kessy, alisema watu hao waliharibu miundombinu hiyo baada ya mradi kukabidhiwa serikalini.

"Inasikitisha kwamba mradi umefeli na umeshindwa kuwa na tija iliyotarajiwa ya kuwahudumia wananchi wa Saunyi. Mradi huu ulitumia Sh. milioni 354,200 na ulikamilika mwaka 2018. "Baada ya kukamilika ulikabidhiwa serikalini na ulifanya kazi muda mfupi na kukumbwa na matatizo mbalimbali ikiwamo kuhujumiwa miundombinu yake. Kama tunakwenda kwa mwendo huu, wahisani hawawezi kuleta miradi katika maeneo ambayo yanashindwa kujisimamia."

Mwakilishi wa Meneja wa Kanda wa World Vision Tanzania, Emanuel Laurent, akizungumza na kamati ya uratibu wa miradi ya jamii, alisema walitumia fedha hizo kujenga miundombinu, kutoa mafunzo kwa mafundi, kamati za kusimamia maji na uhamasishaji wa jamii.

Mkuu wa Wilaya ya Kilindi, Anel Busalama, alitoa siku 14 kwa kamati ya maji ya Saunyi, kuhakikisha mradi huo unafanya kazi na kutengeneza mashine iliyoharibika tangu mwaka jana.

"Naagiza kuanzia sasa, hii kamati ya maji isiingiliwe katika uendeshaji wa mradi huu. Mtendaji wa kata uko hapa (Yussuph Machaku), usiwe mbali nao, hakikisha vituo vyote vya maji vinafufuliwa na wananchi wanapata huduma.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Dustan Ntauka, aliunga mkono jitihada za World Vision, kutaka kupatikana kwa ufumbuzi wa tatizo hilo la kuhujumiwa miundombinu ya mradi wa maji.

# Kampeni chanjo dhidi ya polio kwa watoto yaanza

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

SERIKALI imetangaza kwa mara nyingine kuanza kwa kampeni ya nyumba kwa nyumba ya kuwalinda watoto wenye umri miaka mitano dhidi ya mlipuko wa ugonjwa wa polio ili kuhakikisha hakuna kaya yenye mtoto asiye chanjwa chanjo ya ugonjwa huo.

Ofisa Afya wa Mkoa wa Manyara, Suten Mwabulambo, alisema kwa sasa kuna watoto 438,176 ambao hawajafikiwa na wanapaswa kupata chanjo hiyo ili kuwakinga na maambukizi yanayokuwa kwenye vyakula wanavyokula ambavyo vinaweza kuwa virusi vya ugonjwa huo.

Mwabulambo, alisema jana kuwa mkoa huo unakusudia kuanza kampeni ya utoaji wa chanjo hiyo, awamu ya nne kuanzia Desemba 1 hadi 4, mwaka huu.

"Watoto wanaolengwa kupewa chanjo hiyo ni wenye umri kuanzia miaka sifuri hadi mitano, licha ya kwamba ugonjwa wa polio unaathiri watoto kuanzia miaka sifuri hadi 14. Polio ni ugonjwa unaoshambulia mishipa ya fahamu na vile vile, maambukizi yanakuwa kwenye vyakula tunavyokula," alisema Mwabulambo.

Alisema kampeni hiyo kwa kila halmashauri imejiwekea malengo ya idadi ya watoto, ambao itawachanja. Halmashauri ya Wilaya ya Babati, inatarajia kuchanja watoto 86,287, Babati Mjini watoto 22,080, Hanan'g 74,995, Mbulu 96,712, Mbulu Mjini 56,139, Kiteto 31,117 na Simanjiro watoto 70,846.

Katika awamu ya pili ya kampeni hiyo, kwa mujibu wa Mwabulambo, Manyara ililenga kuwachanja watoto 357,807 na kufanikiwa kuchanja 397,849 sawa na asilimia 111. Wakati kampeni ya awamu ya tatu ilikuwa inalenga kuwafikia watoto 397,849, kuchanja 436,087 sawa na asilimia 110.

Ili kuhakikisha kampeni hiyo inamaliza idadi ya watoto waliobaki, ofisa huyo alisisitiza kuwa serikali imepanga kufanya kampeni yake hiyo kwa wataalamu wa afya kupita shuleni, kanisani, misikitini na sokoni wakitoa chanjo hiyo.

Kuhusu mpango kazi wa kampeni hiyo, Mratibu wa Chanjo wa Mkoa Manyara, Suleiman Manoza, alisema kwenye kampeni hiyo wamepanga timu maalumu za kwenda maeneo magumu na watatumia usafiri wa pikipiki.

Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya mwaka 2019, inaeleza kuwa visa vya virusi vya polio, vinavyotokana na chanjo ni vichache, lakini huwaathiri watoto ambao hawachanjwi na waliopata chanjo kidogo.



## Ongezeko tatizo watoto wenye udumavu latajwa

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

ONGEZEKO la idadi ya watoto hasa wanafunzi wanaopata tatizo la udumavu katika Mkoa wa Manyara, linatajwa kuchangiwa na kukosa chakula cha mchana shuleni.

Mkuu wa Mkoa huo, Makongoro Nyerere, alisema kuwa katika wilaya za mkoa huo, bado kuna watoto hawafundishiki kutokana na udumavu.

Alikuwa akizungumza jana katika kikao maalum cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), kilichofanyika Wilaya ya Babati.

"Utoaji chakula shuleni, bado katika mkoa wetu hatufanyi vizuri, wakati kuna uhusiano mkubwa sana kati ya chakula na kufanya vizuri darasani. Nataka kila wilaya muwabane wazazi na walezi wachangie chakula," alisema.

Katika kikao hicho, Mkuu wa Wilaya ya Hanang', Janeth Mayanja, alisema wilaya hiyo ina shule 155, ambazo hazipati chakula.

Hali hiyo inaathiri usikivu, uelewa na ufaulu wa watoto darasani, Mayanja, alisema ni vizuri serikali ikaja na mpango mahususi wa kuwabana wasiochangia chakula shuleni kwa watoto wao, kwa kuwa maeneo mengi waliofanikiwa kielimu wanafunzi wanakula chakula cha mchana.

Katika Wilaya ya Babati, Mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya hiyo, John Noya, alisema kati ya shule 150 ni mbili pekee, hazitoi chakula cha mchana.

Awali, Ofisa Elimu wa mkoa huo, Halfan Masukira alisema: "Mtoto wa namna hii ambaye alikuwa anashinda na njaa mwaka mzima, ndio tunawaona wanamaliza darasa la saba wanakuwa hawaeleweki. Kumbe walikuwa wanakosa chakula cha mchana."

Kwa mujibu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (PJT-MMMAM) iliyozinduliwa Desemba 13, mwaka jana, Taasisi ya Chakula na Lishe iliandaa toleo la kwanza la miongozo ya kitaifa ya lishe nchini, ambayo inajumuisha makundi yote ya watu, wakiwamo watoto wenye umri kuanzia miaka mitano hadi 10.

# M/kiti CCM aahidi kutokata majina uongozi wake

**Na Cynthia Mwilolezi,**
MANYARA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Manyara, Peter Toima, amesema katika kipindi cha uongozi wake, hakutakuwa na mtindo wa kukata majina ovyo ya wagombea kwa kuwaonea hasa unapofika wakati wa uchaguzi.

Toima alitoa ahadi hiyo jana, baada ya kupokewa na wanachama wa CCM wa Kata ya Emboreet, Wilaya ya Simanjiro, ambako ndiko yalipo makazi yake.

"Kwenye kipindi changu cha uongozi nikiwa kama Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Manyara, nitahakikisha kwamba wanachama wanaongozwa kwa kufuata haki, hatutamwonea mtu, hatutakata ovyo majina ya watu, kwa kuwaonea ila tutaongoza kwa haki na kuwapa fursa ya kufurahia haki ya kuchagua na kuchaguliwa ndani ya chama chetu," alisema.

Kauli ya Toima imeungwa mkono na Katibu Mkuu CCM, Daniel Chongolo, ambaye hivi karibuni alitoa onyo kali kuhusu jambo hilo, akisema sio utaratibu unaokubalika na kwamba wanaopaswa kukatwa ni wote wanaoonekana kupanga safu za uongozi.

Chongolo alinukuliwa akisema, CCM inawataka viongozi wanaowajibika, wanaotambua thamani ya watu wanaowaongoza na ambao wanawajibika bila kuwaangusha kwa kuwa kukata majina kunaweza kutengeneza majeraha ya kisiasa yanayoweza kukigharimu.

Wakati wa mapokezi hayo, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Simanjiro, Kiria Laizer, alisema Toima ni kiongozi pekee anayetarajiwa mkoani humo kuponya majeraha yaliyotokana na uchaguzi wa ndani katika chama hicho unaoweza kutumika kuwagawa wana CCM.

Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa kupitia Wilaya ya Simanjiro, Lenganasa Soipey, alisema wajumbe wa wilaya za Simanjiro na Kiteto, wasingeweza kumpitisha Toima bali kwa ushirikiano na wilaya nyingine.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake (UWT) wa Wilaya ya Simanjiro, Anna Shinini, alisema wajumbe waliamua kugawa viongozi ili Mwenyekiti atoke Wilaya ya Simanjiro na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (NEC), Wilaya ya Babati.



Watalii kutoka mataifa mbalimbali duniani wakiwa na wapanda mlima kutoka kampuni mbalimbali za utalii Kilimanjaro na Arusha, katika eneo la mapumziko kambi ya Barranco, kabla ya safari yao ya kuelekea kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro cha Uhuru Peak (5,895 m ASL), kupitia njia ya Machame na Lemosho, jana. **PICHA: JAMES LANKA**

# Wanafunzi wasaidiwa baiskeli kutimiza ndoto kielimu

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WANAFUNZI wanaotoka katika familia maskini katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Shinyanga, ambao waliokuwa wakitembea umbali mrefu kufuata masomo vijiji vya jirani, wameanza kunufaika na mpango wa Shirika lisilo la kiserikali la ABC IMPACT, linalowezesha usafiri wa baiskeli ili kuwapa motisha kutimiza ndoto zao.

Mkurugenzi wa ABC IMPACT, Ayanna Albert, akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa mradi wa ufundi baiskeli na ujasiriamali uliofanyika Kata ya Olasiti jijini hapo, alisema baiskeli zilizotolewa kuanzia mwezi Januari hadi Novemba mwaka huu, kwa ajili ya wanafunzi hao ni 1,003.

"Uwezeshaji huo wa vyombo vya usafiri kwa wanafunzi hao, unalenga kupunguza utoro, kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi na hasa wanafunzi wa kike kuwanasua kwenye tatizo la kuomba lifti kwa waendesha bodaboda, ambao wakati mwingine huwaingiza katika mahusiano ya kimapenzi na kuishia kupata ujauzito. "Tunaamini kwa kuwapa baiskeli hizi ili kuwahi shuleni na kurejea majumbani baada ya masomo jioni, kutawaepusha na udanganyifu unaowasababishia magojnwa ya zinaa, mimba za utotoni na kuolewa katika umri mdogo au kuacha shule kwa sababu ya ugumu wa kuyafikia masomo yao.

"Tunaendelea kufanya utafiti katika maeneo mengine ili tuendelee kutoa msaada huu wa baiskeli, ambao tunaamini utakuwa mwarobaini wa matatizo tunayoyaona au kuyashuhudia katika jamii zetu. Wanafunzi wa kike, wataepuka kubakwa, kupata mimba kwenye umri mdogo na mengine mengi," alisema.

Alisema, wanatarajia kutoa baiskeli nyingine 300, kwa wanafunzi wenye uhitaji maalum mkoani Dodoma ili kuinua kiwango cha elimu katika shule za serikali. "Kupitia mradi huu ambao tumezindua leo tutatoa mafunzo ya ufundi wa baiskeli na ujasiriamali kwa vijana na tutaanza na 25, mafunzo hayo yataanza rasmi mwakani na katika suala zima la ujasiriamali na tutawafundisha namna ya kufanya biashara mtandaoni na namna ya kukua katika biashara hii ya baiskeli na kutumia mitandao ya kidigitali kukuza biashara na ustadi wao," alisema Ayanna.

Vilevile, Kaimu Meneja wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo mkoani Arusha (SIDO), Anita Mero, alisema uamuzi uliofanywa na shirika hilo wa kusaidia wanafunzi na kuzindua mradi huo kinapaswa kuigwa kwa kuwa kwa kufanya hivyo wanaiunga mkono serikali katika shughuli za maendeleo.

ama
ALHAMISI DESEMBA 1, 2022
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**Waziri Mashimba: Nusu ya sangara wametoweka katika Ziwa Victoria**



Ukurasa 16

Mradi misitu wakikomboa kijiji kilichosaka zahanati miaka 32



Ukurasa 20

**Pata umuhimu matunda, mboga kuliwa yakiwa na maganda yake**

MAZINGIRA

# Azindua jiko 'rafiki wa mazingira'

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

UTUNZAJI wa Mazingira unaenda sanjari na upandaji wa miti na kutokata miti ovyo pamoja na kutunza vyanzo vya maji.

Ili hayo yafanikiwe, kila mmoja ana wajibu kusimamia eneo lake ipasavyo, badala ya kusubiri kusukumwa na taasisi na vyombo vya serikali vinavyohusika na sekta hiyo.

Hivi karibuni, kumekuwepo na makongamano mbalimbali yanayohusiana na mambo ya mazingira lengo hasa ikiwa ni kusisitiza kutunza mazingira na upandaji miti kwenye maeneo ya taasisi na nyumba kwa nyumba.

Wananchi wamekuwa wakitumia nishati ya mkaa kwa wingi kuliko nishati ya gesi ambayo imekuwa mbadala wa mkaa na kuondoa ongezeko la ukataji wa miti.

Mikoa mbalimbali imeathirika na hali hii lakini kubwa ni katika Mkoa wa Pwani ambao mkaa unaovunwa ni kwa ajili ya wakazi wa mkoa huo pamoja na mkoa wa jirani wa Dar es Salaam.

Viongozi wa Mkoa wa Pwani wamekuwa wakikemea hali hiyo iliyokithiri bila mafanikio kwani wafanyabiashara wa mazao ya misitu wakibaini uwepo wa doria wanaamua kutumia njia za panya kuvuka katika mkoa huo.

Hata hivyo wapo wenye vibali vya kuvuna mazao ya misitu ambao idadi yake ni ndogo ukilinganisha na ambao hawana vibali.

Mkaa unatumika kupikia na kutengenezea bidhaa mbalimbali na sasa ni wakati muafaka kwa watumiaji kubadilika na kuanza kutumia nishati mbadala katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Pamoja na mambo mengine lakini ukataji miti ni moja ya sababu ya ukame, ambao unachangia uhaba wa maji na kukosekana kwa mvua kulingana na majira.




Jiko aina mpya linalotumia gesi, rafiki wa mazingira wakati lilipozinduliwa. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

Hivi karibuni mjasiriamali na Mkurugenzi wa Asasi ya Batiki, Rose Urio, alizindua jiko linalotumia nishati safi ya gesi ambalo litawaondoa watengenezaji wa batiki kwenye matumizi ya mkaa.

Rose anasema jiko hili litaenda kuwapa ahueni wazalishaji wa batiki kiafya kutokana na muundo wake na kujiepusha na magonjwa zaidi ya 200 yanayotokana na kuni.

Ni jiko ambalo tunaamini linaenda kuleta mapinduzi makubwa katika utengenezaji wa batiki, linaenda kuwasaidia kiuchumi kwa sababu muda mwingi wataenda kutumia kuzalisha kwa hiyo faida itaongezeka"

"Mazingira ya nchi yetu yanaenda kuboreka kwa sababu ukataji wa miti utapungua na kuunga mkono jitihada za serikali katika kutunza mazingira" anasema Rose.

Anasema kwenye suala la mazingira wajasiriamali hao walikuwa waharibifu wa mazingira lakini kupitia jiko hilo watakuwa mabalozi wazuri wa kutumia nishati safi kwenye kutengeneza batiki.

Rose anaeleza kuwa jiko hilo lina matumizi mengi, wengine pia wataliona na kuanza kulitumia kwa matumizi mengine tofauti na kutengenezea batiki.

"Jiko letu linalotumia nishati safi ya gesi, linatajwa kuwa mkombozi kwa wanawake wajasiriamali wa uzalishaji wa batiki nchini" amesema Mkurugenzi wa Mradi wa Batiki, Rose Urio.

"Sisi kina mama zaidi ya 200 wajasiriamali wa utengenezaji wa batiki tumekuwa tukipata faida kwa kuharibu mazingira, jiko hili litakuwa suluhisho," anasema Rose .

Jiko hilo la gesi asilia linalenga kupunguza kasi ya matumizi ya mkaa na kuni wakati wa utengenezaji wa batiki.

Rose katika uzinduzi wa jiko hilo alifanikiwa kufanya harambee kwa ajili ya kumnunulia jiko mjasiriamali wa batiki mwenye ulemavu anayeishi Bukoba ili kumuwezesha kufanya shughuli zake kwa urahisi.

MAZINGIRA

# Waziri Mashimba: Nusu ya sangara wametoweka katika Ziwa Victoria

**Na Rose Jacob,** MWANZA

ZIWA Victoria linajulikana kuwa tegemeo la taifa na zaidi ya nchi za Afrika Mashariki, lakini uendelezaji wake una matatizo, hasa kupitia uvuvi haramu, kukosekana maadili, sasa ikizaa hali ya tishio

Ziwa Victoria lina ukubwa wa kilomita za mraba 68,000 huku hadi mwaka 2021 inatajwa lilikuwa na wananchi wanaojishughulisha nalo wapatao 102,779 na taarifa za kiserikali zinasema, mwaka jana jumla ya wananchi 194,804 wanaojishughulisha na shughuli za uvuvi nchini, nusu yao (asilimia 53) ni kutoka Ziwa Victoria.



Wavuvi wa Ziwa Victoria, jijini Mwanza wakinadi samaki. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**WIZARA YANENA.**

Mashimba Ndaki, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, anasema baadhi ya wadau wasio waaminifu wameendelea kutumia njia zisizoruhusiwa kisheria kuvua, hata kuathiri shughuli endelevu mahali hapo, ikiwamo uvuvi haramu hususani ndani ya Ziwa Victoria.

"Utafiti uliofanywa mwaka 2021 na Taasisi ya Uvuvi ya Ziwa Victoria (Lake Victoria Fisheries Organization LVFO), unaonyesha katika Ziwa Victoria samaki aina ya sangara wamepungua kutoka tani 1,024,623 mwaka 2020 hadi tani 499,398 kwa mwaka 2021 sawa na upungufu wa asilimia 50," anasema Mashimba.

Anataja samaki walio katika hatari kutoweka kutokana na uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira, baadhi yao ni Ningu (Labeo Victorianus), Soga (Alestopetersius leopoldims), Kuyu (Barbus acuticeps) na Domodomo (Petrocephalis catostoma)

Waziri Mashimba, anasema hadi sasa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, inakabiliwa na matatizo saba yanayokwamisha utendaji wenye tija katika sekta hiyo, akizitaja kuwa ni: Ushiriki duni wa taasisi za kiserikali, hususani Ofisi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI) hasa katika eneo la ushirikiano.

Anautaja umasikini wa wananchi unachangia kuwepo uvuvi haramu, pia kukosekana uzalendo kwa umma, miundombinu duni, kukithiri rushwa kwa watendaji serikalini, hususani wa ngazi ya chini watumiao taa.

**MWELEKEO WA SASA**

Anasema katika kuendeleza wavuvi, serikali imetenga Sh. milioni 60, kuwawezesha wavuvi na wakuza viumbe majini, kununua boti na injini zake za wavuvi, ili kuimarisha ufugaji samaki kwenye vizimba, kuwa na miundombinu bora ya uhifadhi mazao ya uvuvi, ujenzi wa mialo mitatu na masoko saba, mitambo ya kuzalishia barafu na vichanja vya kukaushia dagaa.

> **Kwa sasa sekta ya uvuvi imetoa ajira kwa Watanzania takribani milioni 4.5 katika mnyororo mzima wa thamani, kuongeza usalama wa chakula na lishe kwa asilimia 30 ya protini.**



Mashimba Ndaki, Waziri wa Mifugo na Uvuvi

Anasema kwa sasa sekta ya uvuvi imetoa ajira kwa Watanzania takribani milioni 4.5 katika mnyororo mzima wa thamani, kuongeza usalama wa chakula na lishe kwa asilimia 30 ya protini.

**SAUTI YA WAVUVI**

Wakati serikali ikiendelea kuumiza vichwa juu ya suala zima la uvuvi haramu hata kutoweka samaki aina ya sangara kwa asilimia 50 sasa, wadau nao wana maoni yao, ikiwamo kwa serikali kuchukua jukumu kufanyika doria ya kiulinzi.

Majuta Simwene anafafanua kwamba, wananchi wa Kanda ya Ziwa, watakuwa na ongezeko kubwa la umasikini wa kipato na mlo, iwapo uharibifu utaendelezwa zaidi.

Mvuvi Kimasi Agustino, anasema kila ifikapo kati ya mwezi Septemba hadi Februari kila mwaka, bei ya sangara hushuka, hapo akiomba serikali itafiti bidhaa za samaki hao, mabondo, ngozi, minofu, mafuta ya samaki na mabaki yake (mapanki).

"Tunaiomba serikali itupunguzie kodi katika uvuvi, ununuzi wa vifaa vya uvuvi ikiwamo na kutupatia ruzuku zaidi ya mafuta tunayotumia kuendesha boti za injini, kama ilivyo kwa wakulima na wafugaji,"anasema Kimasi Agustino kwa niaba ya wavuvi wenzake.

Aidha, Kimasi anasema, siyo wavuvi wote wanajikita katika uvuvi haramu, wengi wanafuata sheria za nchi, ila kuna wasiopenda kuwekeza fedha zao katika mitaji ya uvuvi, wanaamua kutumia njia haramu kuvua.

Mwenyekiti wa Chama Cha Wavuvi Tanzania (TAFU), Bakari Kadabi, anaiomba serikali iwasaidie kupambana na wavuvi haramu, akidokeza baadhi ya wanaotenda hayo ni watumishi wa umma.

Pia, Kadabi anaishauri serikali iwashirikishe katika utungaji sera, ili kupunguza migogoro ya kila mara na wavuvi, salamu anayoielekeza vilevile kuimarisha doria kudhibiti ujangili wa uvuvi ndani ya Ziwa Victoria.

**WAZIRI MKUU**

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, katika suala hilo la kukabili ujangili baharini, akatoa maagizo 21 kwa sekta ya uvuvi, mwezi huu akisema ni hali inayotishia kuumiza sekta ya uvuvi nchini, picha halisi ikionyeshwa katika samaki aina ya sangara.

Majaliwa anasema hayo, katika hotuba yake iliyowasilishwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba, katika Mkutano wa Waziri Mkuu na viongozi wa serikali, pia wadau wa sekta ya uvuvi, Kanda ya Ziwa Victoria, uliokuwa na kaulimbiu 'Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Majini kwa Ukuaji wa Uchumi wa Buluu.'

Waziri Mkuu anafafanua: "Kwa kuzingatia umuhimu wa suala hili kupitia mkutano huu, ninatoa maelekezo kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, mamlaka za serikali za mitaa (TAMISEMI) na sekta binafsi, kwa maana ya wavuvi, wenye viwanda, wafanyabiashara ya samaki, mazao ya samaki na zana mbalimbali za uvuvi."

**MAAGIZO WIZARANI**

Maagizo kwenda Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anafafanua:

- Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ihakikishe inasimamia na kutekeleza masuala yafuatayo, kuandaa mikutano ya mara kwa mara itakayokutanisha wadau wote muhimu wa uvuvi, kwa lengo la kubadilishana mawazo, kuhusu changamoto za sekta ya uvuvi na kuzitatua hususani uvuvi haramu.
- Kuimarisha utoaji elimu kuhusu matumizi sahihi ya rasilimali za uvuvi kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano, ili kuwaongezea uelewa kuhusu madhara ya uvuvi haramu, kuwezesha kujenga uendelevu katika shughuli zao za uvuvi.
- Kufanya tathimini ya utekelezaji maelekezo ya matumizi ya nyavu na zana nyingine za kuvulia samaki, ili kujiridhisha endapo wavuvi wa maeneo mbalimbali nchini wanafuata miongozo iliyopo na kutumia zana sahihi.
- Maofisa uvuvi watekeleze wajibu wao kikamilifu ikiwemo kuwatembelea, kutoa elimu kwa wafugaji wa samaki, wavuvi pamoja na kudhibiti uvuvi haramu.
- Kushirikiana na sekta binafsi katika kuhakikisha viwanda vya uzalishaji zana za uvuvi hapa nchini vinaimarishwa, sambamba na kudhibiti uingizaji wa nyavu au zana haramu.

INAENDELEA UK.15

AFYA

# Siku Chuo Kikuu Bugando-Mwanza kilipomwaga wataalamu hospitali

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

NI tarehe njema katika shamrashamra kwenye viunga vya Chuo Kikuu cha Kikatoliki Cha Sayansi za Afya (CUHAS- Bugando) jijini hapa, ikiwahusu wadau 790 wa hospitalini.

Wote walikuwa katika mahafali ya kutunukiwa vyeti vyao katika fani na ngazi tofauti, kijinsia wanaume 436 na kinamama, 364.

Ni mazingira ambayo hospitalini kukatajirishwa na ugeni wa madaktari katika timu yao wakiwa 189, aliyekabidhiwa jukumu hilo la kuwatunuku akiwa Askofu Method Kilaini, Mwangalizi wa Kitume Jimbo la Bukoba.

Aidha, ni orodha yenye wahitimu 120 waliofuzu ngazi ya Stashahada ya Sayansi za Ufundi Maabara ya Tiba na waliopata shahada kwa fani hiyo wako 45; wanafunzi 98 wametunukiwa Stashahada ya Radiografia ya Uchunguzi wa Magonjwa; 143 wamepata Stashahada ya Famasia; huku waliopata Shahada ya Famasia wako 55.



Wahitimu wa Chuo Kikuu Cha Kikatoliki Cha Sayansi za Afya (CUHAS), wakiwa katika maandamano ya mahafali, viwanja vya Hospitali Bugando. **PICHA: ANHTONY GERVAS**

Wengine 79 wametunukiwa Shahada ya Uuguzi, wawili Shahada ya Ualimu wa Uuguzi; waliopata Shahada ya sayansi za ufundi maabara ya tiba wakiwa 45.

Pia, wapo waliotunukiwa stashahada na shahada za fani mbalimbali katika mahafali ya 15 ya chuo hicho yaliyofanyika viwanja vya Hospitali ya Kanda Bugando jijini Mwanza.

Kwa ngazi ya uzamili, wapo 21 waliotunukiwa Shahada ya Uzamili ya Afya ya Jamii (MPH); Shahada ya Uzamili ya Sayansi za Vimelea na Vinasaba wapo wanne; huku 32 wakipatiwa Shahada ya Uzamili wa Magonjwa ya Binadamu; na Shahada ya Uzamivu ikiwa na wahitimu wawili.

Aidha, Askofu Severine anasema ukosefu wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu katika chuo kikuu hicho,ni ajenda wanayoipigania kukipeleka kilio chao kwa serikali, ili kipatiwe ufumbuzi.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo wa Baraza la CUHAS, changamoto za wanafunzi zinajumuisha ulipaji ada, kutokana na viwango vinavyotolewa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na baadhi ya wanafunzi katika chuo hicho hawana uwezo wa kujilipia ada wanapokosa mikopo hiyo.

Rai yake ni kwamba uwekezaji unaoendelea kufanywa na serikali kwenye sekta ya afya, unakuwa na tija zaidi pale wataalamu wake wanaozalishwa wanatumika vilivyo.

Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha CUHAS, Profesa Peter Rambau, anabainisha kuwa chuo hicho mwaka huu kinadahili wanafunzi 1,023, ilhali waliohitimu mwaka jana kwa ngazi ya stashahada mbalimbali ni 2291,shahada za kwanza 425;shahada za uzamili wahitimu 26 na mmoja akatunukiwa PhD

Anasema wanachuo wanakwamishwa na ukosefu wa ada kupitia mikopo, kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na familia zao zinashindwa kumudu gharama za kuwasomesha, akisema ni changamoto inayovikabili takribani vyuo vyote nchini.

**UJUMBE MAMBO MATANO**

Askofu Kilaini anawapa neno wahitimu wa fani ya tiba kutoka Bugando, kwamba ana ujumbe katika mambo matano, akinza na; kutimiza wajibu wa kazi kwa kutumia ujuzi, maarifa waliyoyapata chuoni, maana ndiyo msingi wa taaluma zao,wasiache ujuzi wa kitaaluma na kutumia maarifa mengine nje ya utaratibu wa kitaaluma katika utekelezaji wa majukumu yao.

Pili, Askofu Kilaini anasema haja ya kutumia vizuri nafasi za kazi watakazopata ikiwa ndio hatua sahihi ya kuitumia jamii, iwe katika sekta rasmi au isiyo rasmi.

> **Wengine 79 wametunukiwa Shahada ya Uuguzi, wawili Shahada ya Ualimu wa Uuguzi; waliopata Shahada ya sayansi za ufundi maabara ya tiba wakiwa 45.**

Tatu; taaluma walizosomea zinahusu uhai wa mwanadamu, hivyo kila uamuzi watakaofanya wazingatie maisha ya binadamu na utu wakifanya kazi kwa uadilifu na nidhamu, ili kujijengea jina zuri katika jamii na sehemu yao ya kazi.

Nne; wasiwe wabinafsi katika nafasi na maeneo ya kazi watakayochagua katika kukuza ujuzi na maarifa ya wataalamu walio chini yao katika kujiendeleza kiuchumi wanapojitegemea, wahakikishe haiwi mateso kwa watu wengine.

Mwisho; anawataka wajiwekee malengo ya kitaaluma baada ya kufanikiwa kufuata maudhui hayo machache, hivyo jamii ya Watanzania itafaidika nao kwa namna tofauti.

## Waziri Mashimba: Nusu ya sangara wametoweka Ziwa Victoria

**INATOKA UK.14**

• Kamati za Ulinzi za Vijiji, Wilaya na Mikoa zishirikiane na Wizara ya Mifugo kufanya doria mara kwa mara, ili kuwabaini wavuvi haramu na kuwachukulia hatua za kisheria.

• Kusimamia kikamilifu maeneo yenye rasilimali za uvuvi zilizopo kwenye maeneo hayo pamoja na biashara ya mazao ya uvuvi, viwanda vya samaki viendelee kuimarishwa, sambamba na kuongeza upatikanaji malighafi.

• Wakurugenzi wa halmashauri wahakikishe wanatenga na kurudisha asilimia tano ya mapato yatokanayo na Sekta ya Uvuvi, ili kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi, kulingana na miongozo iliyopo, wakuu wa mikoa, makatibu tawala na wakuu wa wilaya, wahakikishe agizo hili linatekelezwa ipasavyo.

• Ufanyike uhamasishaji wa uwekezaji kwa wale wenye viwanda vikubwa vya uvuvi na ufugaji wa samaki ili, kuimarisha upatikanaji wa samaki nchini sambamba na kukidhi mahitaji ya viwanda.

VIWANDA VYA SAMAKI.

Wenye viwanda waepuke kuchakata samaki wachanga aina ya sangara,kwani kufanya hivyo kunaathiri upatikanaji wa samaki, hasa kwa siku za usoni,kujihusisha na utoroshaji wa mazao ya uvuvi nje ya nchi bila kulipia ushuru wa serikali.

Wafanyabiashara wa samaki wafuate taratibu zilizopo, ikiwemo kuuza, kununua samaki katika maeneo rasmi badala ya kutorosha nje ya nchi.

Kamati za ulinzi za vijiji,wilaya na mikoa zishirikiane na wizara ya Mifugo na Uvuvi kufanya doria za mara kwa mara, ili kuwabaini wavuvi haramu na kuchukua hatua za kisheria bila kupepesa macho.

SEKTA BINAFSI

• Wavuvi, wafanyabiashara na wenye viwanda vya samaki na mazao mengine ya uvuvi, watambue kuwa hakuna haki isiyoambatana na wajibu, kwa misingi hiyo katika uvuvi wanao wajibu.

• Pia, inatakiwa ihakikishe kuendesha shughuli zao kwa kuzingatia sheria na kanuni za uvuvi pamoja sheria za nchi, waache tabia ya kutengeneza na kutumia nyavu zisizokidhi vigezo ikiwemo nyavu aina ya timba.

• Wavuvi wajiunge kwenye vikundi ili iwe rahisi kutatua changamoto zinazo wakabili, ikiwamo kushirikiana na serikali kuimarisha Sekta ya Uvuvi, wafanyabiashara waone umuhimu wa kulipa tozo zinazostahili bila kushurutishwa, waagize nyavu zinazokubalika kisheria.

AFYA

# Mradi misitu wakikomboa kijiji kilichosaka zahanati miaka 32

**Na Christina Haule,** LIWALE

HALMASHAURI ya Kijiji cha Nambinda wilayani Liwale mkoa wa Lindi, inatarajia kukamilisha ujenzi wa zahanati itakayogharimu kiasi cha Sh. milioni 125, ikiwa ni historia miaka 32 tangu kianzishwe.

Ni ahadi ya fedha kutoka Mradi wa Kuhifadhi Misitu kwa Kuwezesha Biashara endelevu ya Mazao ya Misitu Tanzania (CoForEST), kunusuru jamii hiyo inayofedheheka kwa kukosa huduma ya afya karibu.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Saidi Kowe, amesema hayo katika mjumuiko wa Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu (MJUMITA) na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) walipotembelea vijiji vya mradi huo. Kijiji Nambunda kilianzishwa mwaka 1991.

Kowe anasema kukosekana huduma za afya kijijini hapo, kunawalazimu wanakijiji kusafiri umbali wa kilomita nane kufuata huduma hiyo kijiji jirani cha Mlembwe, wengi wakitumia baiskeli na pikipiki, hali inayozua madhara zaidi kwa wajawazito na watoto wachanga.

Ujio huo wa mafanikio ni baada ya kupata mradi huo mwaka juzi, 2020 na kuanza kufanyika shughuli za kuhakiki mipaka ya kijiji, kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, mengine yanayofanyika ni usimamizi shirikishi wa misitu, kuandaa vikundi vya uvunaji mkaa na mbao kwa njia endelevu, pia mafunzo ya kupambana na rushwa kijijini, utunzaji kumbukumbu na kuanza uvunaji mbao kwa namna endelevu.

Kowe anasema katika mwaka uliopita wa fedha, hadi mwaka uliopo, kijiji kimepata mita za ujazo 209 za mbao na kupata kiasi cha shilingi milioni 62, mapato ambayo hawajawahi kuyafikia tangu kijiji kianzishwe.

Mwenyekiti ameyagawa mapato hayo, kwa taratibu zilizopo, akitaja asilimia saba ambayo ni shilingi milioni 4.3 ilipelekwa MJUMITA kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uhifadhi, pia shilingi milioni sita, ambayo ni asilimia 10 zilipelekwa kwenye halmashauri.

Vilevile anasema, asilimia 35 ambayo ni sawa na shilingi milioni 21.8, zilihifadhiwa benki kwenye akaunti ya kijiji, kikilenga mustakabali wa maendeleo yao; uendelezaji usimamizi shirikishi wa misitu ukatengewa shilingi milioni 29.9, ikiwa ina lengo mahsusi kujenga zahanati yao.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, kabla ya mradi huo wa misitu, awali hawakuwa na ndoto ya mradi wa maendeleo na ujenzi wa zahanati kijijini, lakini baada ya mradi kuonyesha mapato, wakakubaliana kujenga zahanati itakayowasaidia huduma za afya jirani na makazi yao.



Katibu wa kamati ya Kijiji Cha Nandimba, Saidi Barabara akiwa na viongozi wenzie wa kijiji wakati akisoma taarifa ya mradi wa mkaa endelevu mbele ya waandishi wa habari (hawapo pichani).

> “Sasa anaiomba serikali kuu iwasaidie kukamilisha ujenzi wa zahanati hiyo, ili ianze kutumika. Hadi sasa imeshatumika shilingi milioni 36.5 kufikia hatua ya rinta.



Mwenyekiti wa kijiji cha Nambinda Saidi Kowe akielezea maendeleo ya ujenzi wa Zahanati ya Kijiji hicho (nyuma yake) itakayowasaidia wakazi hao waliokosa huduma hiyo kwa muda wa miaka 32. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE, LIWALE**

### MWENYEKITI KIJIJI

Mwenyekiti Kowe, anasema ni hatua inayowapa hadhi hata mbele ya vijiji vingine, akijisifu kuwa na uwezo wa kusaidia vijiji katika mambo mbalimbali, ikiwemo kulipia chakula cha kuendesha mikutano, michango ikiwemo ya ujenzi wa shule ya sekondari kata.

Sasa anaiomba serikali kuu iwasaidie kukamilisha ujenzi wa zahanati hiyo, ili ianze kutumika. Hadi sasa imeshatumika shilingi milioni 36.5 kufikia hatua ya rinta.

Anasema, kijiji hicho kina jumla ya wakazi 1,280 kulingana na Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, ukubwa wa hekta 11,224.2 shughuli kubwa ya wakazi ni kilimo na cha mazao ya chakula, ikiwamo mahindi na kunde na biashara mzao biashara ni ufuta na korosho.

Hapo anawataja wateja wakubwa wa biashara zao ni wageni wafikao kijijini, ambao baada ya kufuata taratibu za kisheria wanafanya manunuzi ya mbao kutoka serikali ya kijiji.

### KAMATI MALIASILI

Katibu wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji, Saidi Barabara, anaiomba Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, kutenga fedha za kukamilisha ujenzi wa zahanati, kukiwa na matarajio zaidi kuimarishwa kufikia hadhi ya kituo cha afya.

Anasema katika maboresho hayo, wako katika dira na mchakato kujenga jengo la huduma za wazazi kwenye eneo la zahanati yao ya kijijini na tayari wameshatenga eneo mahsusi, azma ni kuwaondolea kero wajawazito kukosa chumba cha kujifungua, pia huduma za upasuaji kwa wahitaji.

Barabara anaiomba serikali kupendekeza baioanuai zilizopo kijijini, ikiwamo kijiji hicho ikiwemo mabonde mazuri, mabwawa yenye mamba, viboko na ndege weupe ambao ni adimu duniani.

Vilevile, anataja haja ya kuwapo mito mikubwa, kwa kuwa sehemu ya vivutio vya utalii, ili kuongeza mapato kwa Kijiji hicho na kuendeleza shughuli za maendeleo.

Anasema wameanza na ujenzi wa zahanati, lakini bado wanakabiliwa na ukosefu wa ofisi ya kijiji ambayo ni muhimu kutunza kumbukumbu za kijiji. Mpaka sasa hakuna sehemu sahihi za kuhifadhiwa.

### WADAU WAKUU

Mwanamke kijijini, Yanini Makanga, anasema wanapata adha kubwa ya matibabu, hasa pale wanapotaka kujifungua na kulazimika kubebwa na baiskeli au pikipiki kupelekwa zahanati ya kijiji jirani wakapata huduma.

Ana ushuhuda namna umbali wa kupata huduma za afya, umechukua uhai wa baadhi ya kinamama kijijini, akitoa mfano wa mwanamke mwenzake waliojikita wote katika usimamizi shirikishi wa misitu, aliyefariki yeye na mtoto wakiwa njiani kwenda kujifungua.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, Tina Sekambo, anaishukuru TFCG na MJUMITA kwa hatua nzuri waliyofikia kwa shughuli za Usimamizi Shirikishi wa Mazao ya Misitu (USMJ), hata kuvipatia uwezo vijiji kutenga bajeti za kufanya shughuli zao za maendeleo.

Anasema Halmashauri ya Wilaya Liwale, imekuwa ikitenga bajeti ya shilingi milioni 80 kila mwaka, kusaidia uhifadhi misitu kwenye vijiji vya wilaya hiyo, ikiwemo kuondoa wahalifu, kwa sababu zaidi ya robo tatu ya vijiji vya wilaya hiyo wanahifadhi misitu.

Kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack, Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Hassan Ngoma, anaahidi serikali itaendelea kusimamia miongozo yake ya kumalizia miradi inayofikia ngazi ya 'rinta' inayoanzishwa na wanavijiji, ikitoa fedha shilingi milioni 50 kumalizia, zikiwemo zahanati, shule na madarasa.

Anasema katika mwaka wa fedha uliopita, zilitolewa fedha kwa vijiji vya Mkaranga, Mvumi na Miyeo kukamilisha miundombinu waliyoianzisha.

Ofisa Mawasiliano wa TFCG, Betty Luwuge, anasema wote kwa pamoja wanatekeleza Sera ya Misitu ya Mwaka 1998 na Sheria ya Misitu ya Mwaka 2002, inayoelekeza miongozo na kanuni za kusimamia misitu na kufanya Watanzania kufurahia matunda ya kuhifadhi misitu inayowazunguka.

Mkoani Lindi, mradi wa CoForEST unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo na ushirikiano Uswiss (SDC), unatekelezwa katika vijiji vitano vya wilaya za Ruangwa kijiji cha Malolo, Liwale (Nambinda); Nachingwea vijiji vya Lihonja, Mbondo na Nahimba.

AFYA

# Kampeni ya kudhibiti zebaki kwenye dawa meno bado, mlo, rangi ukutani

Na Mary Geofrey

WIKI ya Tiba ya Meno bila zebaki barani Afrika, huadhimishwa kila siku ya Oktoba 13 hadi 20 ya mwaka, hatua hiyo ikifanywa na asasi iitwayo Agenda, inayojihusisha na utunzaji mazingira, pia maendeleo, ikiungana na mashirika mengine.

Mashirika hayo na mengine yasiyo ya kiserikali yako zaidi ya 50 barani Afrika na yanaadhimisha siku hiyo muhimu ya kujikinga dhidi ya madhara yatokanayo na matumizi ya dawa yenye zebaki kutibu meno.

Ni maadhimisho yenye wadau kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Baraza la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) walikutana kujadili na kujipanga kumaliza tatizo hilo nchini.

Tukio hilo lililofanyika katika ofisi zao jijini Dar es Salaam, Ofisa Programu Mwandamizi wa asasi ya Ajenda, Dorah Swai, anasema ni mara ya tisa tangu kuzinduliwa tukio hilo nchini mwaka 2014.

Anaeleza: "Kaulimbiu ya mwaka huu inasema 'tekeleza marekebisho ya mkataba wa minamata ya kupiga marufuku matumizi ya dawa yenye zebaki kutibu meno kwa watoto na wanawake wa umri wa kuzaa ifikapo 2023."

Dorah anatoa wito kwa serikali na nchi nyinginezo Afrika, kuchukua hatua za kuwalinda watu wao, hasa watoto na kinamama, kama inavyotakiwa na marekebisho ya mkataba unaolenga kupiga marufuku matumizi ya dawa hiyo ya meno kwa watoto chini ya miaka 15.

Anasema, pia dawa hizo hazitakiwi kwa wanawake wenye umri wa kuzaa ifikapo mwisho wa 2023, kama inavyotakiwa katika Kanuni za Zebaki Tanzania (2020) na mwongozo wa utoaji huduma za afya ya kinywa Tanzania mwaka 2020.

Mdau huyo anatoa rai kwa serikali, kuhakikisha kliniki za meno nchini zinatii zuio la matumizi ya dawa hiyo, kwa kuwa dawa mbadala za kuziba meno zisizo na zebaki zinapatikana na zimetumika kwa miongo kadhaa nchini Tanzania na kwingine Afrika.

Aidha, anaiomba serikali kutoa uthabiti wa kiwango cha risasi katika rangi kilichopitishwa mwaka 2017 akiwa na rai serikali ifanye utafiti mpya ufahamu hali ya rangi nchini, baada ya kiwango cha kitaifa kuidhinishwa miaka mitano awali.

" Tunahimiza watengenezaji wa rangi, waagizaji na wasambazaji waunge mkono juhudi za serikali kwa kushughulika na rangi isiyo na risasi pekee.

"Hilo linawezekana na tayari baadhi ya watengenezaji rangi wamekuwa wakitengeneza rangi isiyo na risasi kwa zaidi ya miaka mitano," anasema.



Mtu akitumia dawa ya meno. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Madhara ya zebaki katika ukuaji ubongo yanaweza kuwa na athari mbaya katika kiwango cha ufahamu wa mtoto na kufanya ashindwe kujifunza na kuelewa mambo ipasavyo na hatimaye kudumaza maendeleo katika siku za usoni.**



Dawa ya meno inayotajwa kubeba madini zebaki.

### RANGI MAJUMBANI

Ofisa Programu Mkuu wa asasi Agenda, Silvani Mng'anya, anasema tangu mwaka 2009, asasi na mashirika wanachama yamefanya tafiti zaidi ya 100 kwenye rangi zaidi ya 4,000 kutoka nchi 59, ikiwamo Tanzania.

Anasema wameshiriki utafiti wa mwisho mwaka 2017 unaoeleza kuwa asilimia 46 ya rangi za mafuta zinazotumika kupamba majengo nchini, zina kiwango cha madini risasi zaidi ya sehemu 90.

Sylvan anasema, uwekaji chujio la dawa hiyo ya kuziba meno kwenye kliniki za meno ni gharama kubwa na ngumu kutekeleza, kwa kuwa taka anazozitaja kwa jina 'amalgamu' zilizonaswa ndani yake zinapopajaa inakuwa tatizo.

Hapo anasisitiza ulazima wa kuwapo chujio.

Mng'anya anasema, badala ya kutumia njia hizo ngumu wamiliki na waendeshaji wa kliniki za meno umma na binafsi, wanapaswa kuelekeza juhudi zao kuhimiza matumizi ya dawa za kuziba meno zisizo na zebaki, ambazo ni bora zaidi na hazina hatari kiafya pia zisizochafua mazingira.

### MADINI AMALGAMU

Anafafanua kuwa madini amalgamu ni mchanganyiko wa zebaki, madini fedha, bati, shaba na chuma, akiendelea Mng'anya anaeleza kuwa zebaki inapokuwa mwilini hasa kwa mjamzito, athari zake zinamuangukia mama na mimba yake, hata watoto nao wanaweza kuathiriwa kupitia maziwa ya mama, hali inayozuru ukuaji ubongo wa watoto husika.

### VYANZO VYAKE

Mng'anya anasema athari kama hizo zinaweza kusababishwa na kula samaki ambao wameathiriwa na zebaki kutoka kwa maji yaliyochafuliwa na zebaki iliyotokana na amalgamu.

"Ndio maana mkataba wa kimataifa unaojulikana kama Mkataba wa Minamata wa Zebaki ulipitishwa Oktoba 10 mwaka 2013 huko Kumato, Japan na kutiwa saini na serikali ikiwamo ya Tanzania.

"Mkataba unazitaka serikali kupunguza na hatimaye kusitisha matumizi ya amalgamu katika tiba ya meno," anasisitiza Mng'anya.

Anataja mkataba huo ulianza kutumika kisheria Agosti 16 mwaka 2017, baada ya kuridhiwa na nchi 50 Tanzania ikiwa ni miongoni mwao mwaka 2019 na hadi kufikia Oktoba 12 mwaka huu, nchi zilizoridhia zilikuwa 138.

"Madhara ya zebaki katika ukuaji ubongo yanaweza kuwa na athari mbaya katika kiwango cha ufahamu wa mtoto na kufanya ashindwe kujifunza na kuelewa mambo ipasavyo na hatimaye kudumaza maendeleo katika siku za usoni," anasema Mng'anya.

Pia, anataja madhara mengine ni kwamba zebaki inaweza kuharibu mfumo wa fahamu, figo, mapafu, kinga, macho, fizi na ngozi ya mwanadamu.

"Zebaki inaweza kuwa na madhara hasi ya uzazi kama vile kuharibu mbegu za kiume, kasoro za kuzaliwa, matatizo ya uzazi," anatamka, huku akitaja dalili za madhara yake ni mhusika anatetemeka, haoni vizuri, anapooza, kukosa usingizi na kukosa utulivu wa kihisia.

Anasema barani Afrika, nchi zake ziliridhia mkataba wa Minamata katika mkutano wake wa nne uliofanyika nchini Indonesia, Machi mwaka huu, walirekebisha mkataba wakiafikiana kudhibiti matumizi ya madini amalgamu kwa watoto, wanawake wajawazito na wanaonyonyesha.

Anafafanua kuwa, Umoja wa Ulaya, pia nchi za Nigeria, Mauritius na Zambia, tayari zimeshaondoa matumizi ya amalgamu ya meno kwa watoto, wajawazito na wanaonyonyesha, huku nchi za Cameroon, Madagascar na Benin zinaondoa matumizi ya amalgamu katika hospitali zote.

"Ni wakati wa nchi zinazosalia za Kiafrika kuchukua hatua kama hizo," anasisitiza Mng'anya.

### MKEMIA MKUU

Mratibu wa Kituo cha Taifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa serikali (GCLA), Yohana Goshashy, anasema elimu inahitajika kwa jamii kuhusu kuacha matumizi hayo ya zebaki, kwa sababu ya madhara yaliyotajwa.

Anasema, hadi sasa wananchi hawana elimu ya kutosha kuhusu madini ya risasi kwenye rangi za mafuta, kwa sababu hayaonekani kwa urahisi.

Yohana anahimiza elimu zaidi kwa umma kuhusu kuepuka matumizi ya sumu hizo ili kuepuka madhara makubwa zaidi kwa jamii.

AFYA

# Wenye ulemavu wakombolewa kwa vitanda maalum kujifungua hospitali

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KUNA makundi katika jamii yanapopata ujauzito, yanakabiliwa na unyanyapaa, ugumu, pia ubaguzi unowafikishia kukosa huduma ya afya ya uzazi kipindi chote, kwa kutohudhuria kliniki na hata wakajifungua majumbani.

Pia, katika baadhi ya maeneo, hata kwa wale wenye uthubutu wanapofika katika hospitali jirani yao, hakuna mazingira rafiki, ikiwamo vitanda maalum kwa walemavu kujifungua vituoni humo.

Halmashauri za Msalala na Manispaa Kahama, mkoani Shinyanga, kwa kushirikiana na wadau binafsi imeona hilo na kutaka mageuzi, ya kuwapa wajawazito wenye ulemavu mazingira mazuri ya kujifungulia, huku wakiwa wadau hai wa kliniki kipindi chote.

Kwa sasa kumeanza kutolewa kitanda maalumu cha kujifungulia wanawake hao, katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama, inayoongoza kuhudumia wagonjwa kutoka halmashauri jirani za Msalala na Ushetu, na siku wagonjwa 1,000 likiwemo kundi hilo tajwa.



Watoto wenye ulemavu wakiwa wamekaa katika viti vitatu kati ya vitano vilivyotolewa na wafadhili. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA**

### MBUNGE IKUPA

Stella Ikupa, Mbunge wa Viti Maalumu, akitokea kundi la wenye ulemavu, ambaye pia ni Mkurugenzi wa asasi Ikupa Trust Fund, anasema maungo ya wenye ulemavu hususani wanawake, yako tofauti na wengine, hali inayotoa uhitaji maalum kipindi cha kujifungua.

Anasema vituo vya afya, hospitali za wilaya na mikoa zinatakiwa na kuwa na chumba maalumu cha wajawazito wenye ulemavu, kwa ajili ya kuwasitiri, kutokana na upekee wao.

"Tukipata tu ujauzito jamii inatushangaa na kutuona watu wa ajabu kupata ujauzito, huku tukiwa na ulemavu. Je, wakiona maumbile yetu wakati wa kujifungua huoni kama watatuona kituko? Tunaomba kutengewa wodi ili tufiche maungo yetu," anasema Ikupa.

Aidha, anasema suala la kuoa na kuolewa kwa watu wenye ulemavu, linachukuliwa tofauti kwenye jamii na pale mtu anapooa au kuolewa na mwenye hali hiyo, anachekwa na kuonekana hana maana kwani nao wana haki kama yalivyo makundi mengine katika jamii.

Wakati anapokea msaada wa Dola za Marekani 10,000 (Sh. milioni 236) Ikupa anasema asasi yake Ikupa Trust Fund, kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za wanawake na ufadhili kutoka nje ya nchi.

Mbunge Ikupa anafafanua kwamba wafadhili hao wanatambua mchango wa wenye ulemavu katika jamii, ikiwamo kufanya biashara na kulipa kodi za serikali, hivyo ni muhimu wapate huduma kama yalivyo makundi mengine ya kijamii.

> "Tukipata tu ujauzito jamii inatushangaa na kutuona watu wa ajabu kupata ujauzito, huku tukiwa na ulemavu. Je, wakiona maumbile yetu wakati wa kujifungua huoni kama watatuona kituko?



Mbunge wa Viti Maalumu, Stella Ikupa, akimkabidhi Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama, Dk. Deo Nyaga (aliyeshikana naye mkono), kitanda cha kujifungulia watu wenye ulemavu.

Anasema, wameshakabidhi kitanda kimoja cha kujifungua wajawazito hao na baiskeli tano kwa watoto wanafunzi walemavu vyenye thamani ya Sh. milioni 3.1 katika Hospitali ya Manispaa Kahama.

"Tunaungana na mama yetu Mama Samia, ambaye amekuwa akisisitiza kuwepo vyumba maalumu vya kujifungulia kwa watu wenye ulemavu. Sie tunahitaji usiri na miundombinu rafiki wakati wa kujifungua ndiyo maana tumeona umuhimu wa kuleta kitanda cha kujifungulia hapa Manispaa (Kahama)," anasema mtetezi huyo wa wenye ulemavu.

### WADAU JIRANI

Kaimu Meneja Uhusiano wa Jamii kutoka mgodi wa Barrick Bulyanhulu, Zuwena Senkondo, anasema

wametoa viti vitano kwa ajili ya watoto wenye ulemavu na kitanda kimoja maalumu cha kujifungua wenye ulemavu, ikiwa ni sehemu ya kuungana nao.

Pia, Mwenyekiti wa Wanawake na Wenye Ulemavu Manispaa ya Kahama, Rehema Joshua, anasema kitanda cha kujifungulia walichopokea kitawasaidia kupata mazingira rafiki wakati wa kujifungua, ikilinganishwa na halisi iliyoko sasa wodini, akiamini wengi watajitokeza kujifungulia hospitalini.

Anaorodhesha sababu kuwa; wajawazito wengi wenye ulemavu walishindwa kujitokeza kujifungulia katika vituo vya afya, kutokana na mazingira ambayo hayakuwa rafiki kwao, ikiwemo kuchanganywa wodi moja na wajawazito wasiokuwa walemavu, hali inayowafedhehesha, hata wengine kujifungulia majumbani na kuhatarisha usalama wao.

Elizabeth Samweli, mkazi wa Mtaa wa Shunu, Manispaa ya Kahama, anasimulia namna mwanawe alijifungua hospitalini, lakini baadaye alishangaa akidhihakiwa kwa kuchekwa mtaani na hata alipodadisi kulikoni, ikagundulika faragha ya wakati wa kujifungua, imehamishiwa mitaani.

Anasema, baada ya hapo mama huyo akalazimika kujifungua nyumbani, kila pale alipopata ujauzito mara kadhaa akitumia wataalamu wa asili, hali ambayo ni hatari katika huduma hiyo.

Vilevile, mkazi Edward Charles, anasema kitanda hicho kipya kitawasaidia wajawazito wenye ulemavu kujifungua hospitali, tofauti na ilivyokuwa awali. Anaiomba serikali, baada ya kumaliza kutenga wodi maalumu ya watu hao, iwapatie watoa huduma maalum kama wanavyofanya wazee.

### MGANGA MFAWIDHI

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama Dk. Deo Nyaga, akipokea msaada huo, anasema wamekuwa wakipokea kinamama wenye ulemavu na wanawahudumia kulingana na mazingira na vifaa vilivyopo, hivyo kupatikana kwa kitanda hicho kutaondoa changamoto za kuhudumia sehemu hiyo ya jamii.

Anasema, suala la kutenga chumba kwa ajili ya wajawazito wenye ulemavu linashughulikiwa na uongozi katika manispaa yao na kuna jengo sasa linaendelea kujengwa mahsusi kwa ajili ya kinamama, watoto na wajawazito wenye ulemavu.

Mganga huyo anashauri kwamba, wakati wakiendelea kutatua changamoto hizo, ni vyema iangaliwe namna ya kumpata mtoa huduma anayefahamu lugha za alama, ili pale wanapopata mteja mwenye tatizo la namna hiyo, aweze kupata kuwasaidia watoa huduma za tiba.

AFYA

# TRA Katavi ilivyowekeza ‘Wiki ya Mlipa Kodi’ hospitali mkoa

**Na Neema Hussein**



Watumishi wa Mamlaka ya Mapato mkoa wa Katavi, wakifanya usafi katika Hospitali ya Rufani Katavi, mjini Mpanda. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN**

KATIKA kutambua mchango wa walipa kodi na wadau mbalimbali serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani Katavi, iliandaa Wiki ya Mlipa Kodi’ kwa lengo la kuwatambua na kuwashukuru walipa kodi wote kwa mchango wao kwa Taifa.

Siku ya kwanza katika kuadhimisha wiki hiyo, mkoa ulifanya usafi katika Hospitali ya Rufaa mkoa wa Katavi, sambamba na kukabidhi msaada kwa wagonjwa.

Kamishna wa Upelelezi wa Kodi Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Andengenye Mwaipopo. Anaeleza kuwa: “umuhimu mkubwa wa wiki hii ni kuwapongeza walipa kodi wote na kuimarisha mahusiano mazuri kati ya TRA na wananchi ikiwa ni pamoja na kujenga imani na ridhaa kwa walipakodi.

“Katika mkoa wa Katavi tumeadhimisha wiki hii kwa kufanya mambo yafuatayo kwanza tumefanya usafi kwenye hospitali mpya ya mkoa, tumewatembelea wagonjwa katika hospitali ya mkoa, bonanza la michezo litakalo shirikisha wananchi wote wa Katavi.

“Mpira kati ya wafanyakazi wa TRA na wafanyabiashara hiyo yote ni kuwaweka wafanyabiashara karibu na Mamlaka ya Mapato Tanzania, ili wasione kama ni maadui bali ni watu wanaohitaji kufanya kazi pamoja kwa nia njema ya kuendeleza Taifa letu.

“Pia, tumewatembelea walipa kodi nyumba kwa nyumba kwa ajili ya kutoa elimu na kutatua changamoto zao zinazo wakabili kuhusu maswala ya Kodi,” anasema.

Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoa wa kodi Katavi Jacob Mtemang’ombe, anasema walilenga kundi la kina mama waliojifungua wenye watoto wenye umri hadi siku 28 wachanga, kuwapa msaada kwa sababu wao wana mahitaji mengi zaidi.

“Lakini hatukuishia hapo, tulienda pia hadi ya watoto wenye umri wa mwezi mmoja hadi miaka mitano na kutoa msaada kidogo ambao tulikua nao.

“Tulipofika pale tulikutana na jambo ambalo lilituumiza mioyo la mtoto mmoja aliyekuwa amelazwa pale lakini mama yake alikuwa hana uwezo wa aina yoyote na mtu wa kumsaidia, hata kulipia zile dawa, lakini muuguzi wa ile wodi alipotuambia sisi kama jamii na kama wanadamu kwa kweli tulijisikia vibaya. “Ilibidi tufanye harambee palepale tulipokuwepo na kikapatikana kiasi fulani cha fedha na tukamkabidhi yule mama,” anasema Mtemang’ombe.

Ni tukio ambalo siku iliyofuata, liliendana na kukabidhiwa mashine ya kufua hospitalini.

> **“Tulikua tuna mtoto anaitwa Deus tulimpokea siku ya pili sasa ni mtoto ambaye ametokea katika familia duni, mama yake ameachana na mume wake.**



Watumishi wa Mamlaka ya Mapato mjini Mpanda wakitoa msaada kwenye hospitali ya rufani mjini Mpanda, kuadhimisha Wiki ya Mlipa Kodi.

### AFYA BONANZA

Kwa kuzingatia ‘michezo ni afya’ siku iliyofuata kulikuwa na bonanza la michezo mbalimbali kama mpira wa miguu na kwa upande wa wanawake, timu ya wanawake kutoka soko la Mpanda Hoteli, ilicheza na timu ya wanawake kutoka Soko Kubwa.

Pia, wafanyakazi wa TRA kwa upande wa wanaume walicheza na wafanyabiashara, huku waendesha bodaboda wakichuana na madereva wa bajaji.

Timu zote baada ya kucheza mpira pia zilipimana nguvu kwa upande wa kuvuta kamba na kukimbia kwa kutumia magunia na michezo mingine ilifanyika na washindi wote walipewa zawadi.

### DAKTARI WATOTO

Daktari Maria Matei ni Mkuu wa Idara ya watoto hospitali ya mkoa wa Katavi amewashukuru wafanyakazi wa TRA kwa msaada wao.

“Tulikua tuna mtoto anaitwa Deus tulimpokea siku ya pili sasa ni mtoto ambaye ametokea katika familia duni, mama yake ameachana na mume wake.

“Tulipokewa akiwa na shida ya kujaa maji kwenye tumbo na familia yake ikiwa haina chochote tulimuanzishia matibabu, lakini kuna sehemu tulikwama kwa kukosa pesa ambayo alitakiwa atoe huyu mama ili kuendelea kufanya vipimo na kuendelea na matibabu. tunawashukuru TRA,”anasema Dokta Matei.

Elizabeth Januari, ni mama mzazi wa mtoto huyo anashukuru TRA kwa msaada huo, kutokana na fedha walizotoa kuendelea na matibabu hospitalini hapo.

TRA pia imetoa mashine nne za kufulia nguo zenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni sita.

Ofisa Ugavi wa Hospitali ya Rufani Mkoa Katavi anasema “mashine hizi tulizopewa zitatusaidia sana kufua nguo za wagonjwa mashuka pamoja na vitu vingine. Kwa hiyo tunawashukuru sana.”

Pia, TRA ilitumia wiki hiyo kwa kutoa vyeti na tuzo kwa walipakodi bora wa mwaka 2021/2022 kwa makundi matatu ambao ni walipakodi wakubwa,walipa kodi wa kati na walipakodi wadogo.

Na vigezo walivyozingatia katika kutoa vyeti hivyo ni pamoja na ulipaji stahiki wa kodi na kuwasilisha ritani za kodi kwa wakati husika, kulipa kwa wakati kodi zao, na kutopewa onyo lolote kutoka kwa TRA katika utendaji wao wa kazi.

Mbali na wafanya biashara pia Mamlaka hiyo imetoa tuzo kwa idara zilizo isaidia TRA kufikia malengo ya ukusanyaji kodi ambazo ni Ofisi ya Mkuu wa mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoa wa Katavi, Ali Makame na Tobacco Lake Tanganyika.

Mwakilishi wa Mkuu wa mkoa wa Katavi Jamila Yusuf, amewapongeza TRA mkoa wa Katavi kwa kufuata maelekezo yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kukusanya kodi kwa weledi na kuzungumza na wafanyabiashara.

Mwenyekiti wa jumuiya ya wafanyabiashara mkoa wa Katavi, Amani Mahela anasema waligundua kukwepa kodi ni kujikaanga kwa mafuta yao wenyewe.

“Niwaombe ndugu zangu wa TRA wasichoke kutoa elimu kwa sababu sisi wafanyabiashara kila siku tunafilisika na wafanya biashara wapya wanaongezeka hivyo ni jukumu lao TRA kuboresha elimu kwa wafanyabiashara ili nchi yetu iweze kwenda vizuri na tupate maendeleo.

MAZINGIRA

# Pata umuhimu matunda, mboga kuliwa yakiwa na maganda yake



Mboga za aina mbalimbali. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

KUNA watu wengi kila wanapotayarisha matunda na mboga huwa wagumu kukataa hatua ya kutoyamenya.

Daima kibinadamu kuna virutubisho muhimu kwenye maganda ya mboga hizo. Kando na hilo, pia maganda ya matunda na mboga yanayotupwa huchangia mabadiliko ya hali ya hewa.

Matunda na mboga ni vyanzo vikuu vya vitamini, madini, nyuzinyuzi na kemikali nyingi zinazolinda mwili na chembe hai.

Kutokula vyakula hivyo vyenye virutubishi vya kutosha, huwa kunahusishwa na kuongezeka hatari ya kupata magonjwa sugu, moyo, mishipa na kisukari cha aina ya pili.

Mwaka wa 2017, Shirika la Afya Duniani (WHO) limeripoti kwamba, kuna vifo takriban milioni 3.9 mwaka huo, ambavyo vinahusishwa na watu.

Ushauri ulioko ni kwamba, mtu anapokula wastani wa gramu 400 za matunda na mboga kwa siku, kama ilivyopendekezwa na WHO, imekuwa vigumu kwa watu wengi.

Hoja inayojitokeza, je kula matunda na mboga na maganda yake, kunaweza kusaidia kumaliza tatizo hilo kupitia njia ya kuongeza virutubisho muhimu kwenye mlo wa watu?

Bila shaka ni hali inayoweza kuchangia, ikiirejea mfano, kiasi kikubwa cha vitamini kama vile vitamini C na riboflavin na madini kama chuma na zinki, hupatikana kwenye maganda ya aina ya mboga zipatazo saba, ikiwamo karoti mwitu, viazi vitamu, tangawizi na viazi vyeupe.

> **Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Marekani inapendekeza kwamba watu wanawe vizuri katika maji baridi na kusugua kwa brashi ngumu ili kuondoa dawa za kuua wadudu, uchafu, na kemikali.**



Matunda matikiti ambayo ni muhimu kulika.

Idara ya Kilimo ya Marekani inaonyesha kwamba tufaha ambazo hazijatolewa maganda zina asilimia 15 ya vitamini C zaidi, pia vitamini K, ina madini ya calcium na potassium na nyuzinyuzi nyingi, kuliko vile zilizotolewa maganda.

Pia, inatajwa kuna maganda mengi yenye kemikali nyingi za kibaolojia ambazo ni muhimu kwa afya ya mlaji binadamu.

Sababu nyingine ya kutotupa maganda ya matunda na mboga, inaelezwa ni athari yake kwa mazingira, Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) likisema chakula kisicholiwa kwa kujumuisha maganda kinazalisha kati ya asilimia nane na 10 ya gesi chafu duniani, hapo ikijumuisha chakula kinachooza kwenye dampo.

New Zealand, nchi yenye wakazi milioni 5.1 pekee, inaripoti upotevu wa tani 13,658 za maganda ya mboga na tani 986 za maganda ya matunda kila mwaka.

Kwa kuzingatia maudhui ya virutubishi kwenye maganda na mchango wa maganda hayo katika upotevu wa chakula, sasa inahojiwa kwanini watu humenya matunda na mboga?

Ikirejewa kanuni za jumla, matunda na mboga ni lazima zitolewe maganda, kwa vile sehemu za nje haziliwi, hazina ladha nzuri ni ngumu kusafishwa, au kusababisha uharibifu kama vile ndizi, chungwa, tikitimaji, nanasi, embe, parachichi na kitunguu saumu.

Pia, kusafisha kunaweza kuwa sehemu ya lazima ya mapishi kama vile wakati wa kutengeneza viazi vilivyosokotwa. Lakini, maganda mengine kama ya viazi, karoti na tango, yanaweza kuliwa, ingawa watu huyamenya.

**MABAKI YA DAWA**

Baadhi ya watu humenya matunda na mboga, kwa sababu wanahofia mabaki ya dawa za kuua wadudu zilitumiwa wakati wa ukuzaji.

Mabaki ya dawa husalia kwa kiasi kidogo, ingawa hii inatofautiana na spishi za mimea. Hata hivyo, mengi ya mabaki haya yanaweza kuondolewa kwa kuosha.

Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Marekani inapendekeza kwamba watu wanawe vizuri katika maji baridi na kusugua kwa brashi ngumu ili kuondoa dawa za kuua wadudu, uchafu, na kemikali.

Mbinu za mapishi kama vile kuchemsha na kutumia mvuke, zinatajwa kuweza pia kupunguza mabaki ya dawa hizo na ndio sababu watu wanahofia uwezekano wao wa kuathiriwa na dawa za kuulia wadudu, wakiamua kumenya matunda na mboga.

Katika baadhi ya nchi kuna orodha za kiasi cha dawa za kuua wadudu kwenye matunda na mboga, ikitajwa inaweza kusaidia kuamua ni matunda na mboga gani ya kumenya.

• ***Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.***



# TRA yatakiwa kusajili wafanyabiashara matumizi EFD

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), mkoani Mbeya imetakiwa kuandaa mikakati ya wafanyabiashara wote wenye sifa ya kutoa stakabadhi kwa kutumia mashine za kielektroniki (EFD), wanasajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Pia imetakiwa kuhakikisha wafanyabiashara hao wanazitumia mashine hizo kwa mujibu wa sheria ili kuepuka ukwepaji wa kodi kwa baadhi ya wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu.

Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, wakati wa kuhitimisha maadhimisho ya wiki ya shukrani kwa mlipakodi na utoaji tuzo kwa walipakodi bora mkoani humo.

Alisema tatizo hilo la wafanyabiashara kutotoa risiti za EFD linasababisha upotevu wa mapato ya serikali kutokana na ukwepaji kodi wa makusudi.

"Sasa nawaagiza TRA mhakikishe wafanyabiashara wote wanaostahili kutoa risiti hizi wanazitoa ili kudhibiti huu ukwepaji wa kodi, wafanyabiashara ni mawakala wa serikali wa kukusanya kodi," alisema Homera.

Mkurugenzi wa Utafiti na Sera wa TRA kutoka makao makuu, Ephrahim Mdee, alisema kwa mwaka huu wa fedha Mkoa wa Mbeya umepangiwa kukusanya Sh. bilioni 85.

Alisema kila mkoa nchini umepewa lengo la ukusanyaji kulingana na wingi wa vyanzo vya mapato na kwamba serikali itaendelea kufuatilia kila eneo la ukusanyaji wa mapato.

Meneja wa TRA Mkoa wa Mbeya, Shabani Muhibu, alisema tatizo linalowakabili kwa sasa ni biashara za magendo ambazo huwa zinasababisha upotevu wa mapato.

Alisema bidhaa ambazo huwa zinaingizwa nchini kwa njia za magendo huwa zinauzwa kwa bei ya kawaida tofauti na zilizoingizwa kwa kufuata utaratibu.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kiwanda cha Saruji cha Mbeya, Khaled Ghareib (kulia), akitoa maelezo kwa Waziri wa Madini, Dotto Biteko, kuhusu wanavyochimba madini ya kuzalishia saruji kwenye mgodi wa kiwanda hicho, Songwe, mkoani Mbeya juzi. Kushoto ni Meneja wa Kiwanda hicho, Mhandisi Pamphili Mumwi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Serikali yaagiza kiwanda ushirikiano na wananchi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeuagiza uongozi wa Kiwanda cha Saruji cha Mbeya (Mbeya Cement), kuandaa utaratibu wa kushirikiana na wananchi kutekeleza miradi ya maendeleo ili kuendana na sheria za uwekezaji pamoja na kuimarisha uhusiano na wananchi.

Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara katika kiwanda hicho kwa lengo la kuangalia aina ya madini yanayotumika kwenye uzalishaji pamoja na kukagua mgodi wa kiwanda hicho unaozalisha malighafi ya kiwandani.

Waziri Biteko alitoa agizo hilo baada ya Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, kueleza kuwa kiwanda hicho hakina utaratibu mzuri wa kuchangia miradi ya maendeleo (Cooperate Social Responsibility).

Njeza alisema kiwanda hicho kimekuwa kikichangia baadhi ya miradi ya wananchi bila kuishirikisha serikali hali inayosababisha kutokuwapo kwa takwimu sahihi za miradi inayochangiwa kwa wananchi.

"Wamekuwa wakishirikiana vizuri na wananchi isipokuwa michango yao ya CSR haiwi ya wazi, kwa utaratibu ni kwamba CSR ni uwekezaji kwa halmashauri na ilitakiwa iwe inapitia kule ili iwepo kwenye vitabu vya serikali," alisema Njeza.

Alisema wananchi wa eneo hilo walitoa maeneo yao kwa hiari ili kuruhusu kiwanda hicho kupata eneo la kuchimba madini ya kuzalishia saruji na kutakiwa kutoa michango yao kwa uwazi.

Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Khaled Ghareib, alisema kiwanda hicho kimekuwa kikichangia miradi mbalimbali ya wananchi ikiwamo ukarabati wa vyumba vya madarasa pamoja na ununuzi wa madawati 100 yanayotumiwa na wanafunzi 300.

Vilevile, alisema kiwanda hicho kinawasaidia wananchi huduma ya maji ambayo kinazalisha, kuyatibu na kuyasambaza bure kwa wananchi zikiwamo shule za msingi na sekondari zilizoko katika eneo la jirani na kiwanda.

Ghareib alisema kiwanda kimeshiriki kwenye kazi ya utunzaji wa mazingira ikiwamo upandaji wa miti zaidi ya 200 kwa kushirikiana na wananchi wa Bonde la Songwe.

"Kiwanda chetu kimekuwa kikichangia kwa kiasi kikubwa kwenye mapato ya serikali, kila mwezi tunachangia zaidi ya Sh. milioni 40 na tumejitahidi kuzalisha ajira kwa wazawa mpaka sasa tuna wafanyakazi zaidi ya 180, lakini raia wa kigeni ni wawili pekee," alisema Ghareib.

Alisema kiwanda hicho kwa sasa kinazalisha saruji ambayo inauzwa kwenye soko la ndani na nyingine inauzwa kwenye mataifa jirani ikiwamo Malawi, Zambia, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Baada ya maelezo hayo, Waziri Biteko alionyesha kutoridhishwa na uwajibukaji wa kiwanda hicho kwa jamii kwa kusema kuwa michango wanayochangia ni kidogo na akawataka kubuni miradi mipya badala ya kukarabati iliyotekelezwa na wananchi.

Aliwataka kutunza kumbukumbu ya michango wanayochangia kwenye miradi ya wananchi ili serikali inapozihitaji iwe rahisi kuzipata na kuzitumia kwa matumizi yanayokusudiwa.

"Nimekuja hapa kwa ajili ya kujiridhisha na baadhi ya mambo yanayofanywa na kiwanda hiki, sijaridhika na utekelezaji wa CSR, kupanda miti 200 na kukarabati madarasa hiyo ni miradi midogo sana ikilinganishwa na mnachokipata, sasa hebu anzisheni miradi yenu tuione," alisema Waziri Biteko.

Alisema serikali itaendelea na mazungumzo na uongozi wa kiwanda hicho ili kurekebisha baadhi ya mambo ambayo hayako sawa ikiwamo wananchi kuwa na migogoro na kiwanda.

# Wadau waomba vituo malezi ya watoto kufuatiliwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU wa makuzi na malezi ya watoto mkoani hapo, wamewaomba maofisa ustawi wa jamii katika ngazi ya halmashauri kufuatilia utendaji wa vituo vya kulelea watoto kwenye maeneo yao wakieleza kuwa baadhi ya watoto walio kwenye vituo hivyo wanafanyiwa ukatili.

Walitoa ombi hilo kwenye kikao cha tathmini ya makuzi na malezi ya watoto wenye umri wa kati ya miaka sifuri mpaka miaka minane, mkoani hapo.

Mmoja wa wadau hao, Michael Malecela, Kaimu Ofisa Elimu wa Wilaya ya Rungwe, alisema baadhi ya watoto wanaolelewa kwenye vituo hivyo wamekuwa wakinajisiwa na kuhatarisha usalama wa kundi hilo.

Alisema vitendo hivyo vinafanyika kutokana na baadhi ya walezi wa vituo hivyo kutokuwa na maadili ya kazi na kuomba serikali kuchunguza kwa makini ili kubaini wanaotekeleza unyama huo dhidi ya watoto.

"Wote ni mashahidi tumekuwa tukisikia taarifa nyingi za watoto kubakwa na kulawitiwa kwenye hivi vituo, sasa tuwaombe maofisa ustawi wa jamii watusaidie kukabiliana na matatizo haya," alisema Malecela.

Alisema vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto vinasababisha matatizo mbalimbali ikiwamo kuathirika kisaikolojia pamoja na matatizo mengine ya kupata magonjwa ya zinaa.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Mkoa wa Mbeya, Aika Temu, alisema mkoa huo una vituo vya kulelea watoto zaidi ya 200 ambavyo vimesajiliwa kwa mujibu wa sheria na vinafanya kazi.

Alisema wanapobaini ukiukwaji wa maadili kwenye vituo hivyo huwa wanachukua hatua kwa mujibu wa sheria ikiwa ni pamoja na kuvifungia.

"Ni kweli vipo vituo vinakiuka sheria na vingine tumeshavichukulia hatua kwa kuvifungia, vingine tunaendelea kuvisajili na vingine tunavifuatilia ili tukijiridhisha tuvichukulie hatua endapo tutabaini ukiukwaji huo wa sheria," alisema Temu.

Aliwataka wamiliki wa vituo hivyo kufanya kazi kwa kufuata sheria ili kuepuka kukumbwa na mkono wa sheria na kwamba serikali inaendelea kufanya kazi yake kwa kushirikiana na wadau.

Mwakilishi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Leah Mwakasobe, aliwataka maofisa ustawi wa jamii walio kwenye halmashauri kujiridhisha na vigezo kabla ya kusajili vituo hivyo.

Alisema wizara huwa inavisajili vituo hivyo kwa kutegemea mapendekezo ya maofisa ustawi wa jamii na kuwataka kuwa makini kwa kuwa wakitoa maoni hayo wizara huwa haiwezi kubadili mtazamo.

Katibu Tawala Msaidizi Mipango wa Mkoa wa Mbeya, Emmanuel Kilundo, aliwataka wadau wote wanaotekeleza programu hiyo kufanya kazi kwa kushirikiana ili kuhakikisha inatekelezwa kwa ufanisi.



# Serikali kupitia upya sera utaratibu kuasili watoto

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum imesema iko katika mchakato wa kupitia upya sera na taratibu ili kuweka utaratibu mzuri wa kuasili na malezi ya watoto wa kambo nchini.

Akizungumza jana katika kikao kazi cha wadau kutoka wizara za kisekta na taasisi za serikali kilichofanyika jijini hapo, Kamishna wa Ustawi wa Jamii wa wizara hiyo, Dk. Nandera Mhando, aliwaomba wadau hao kuja na mapendekezo ya namna bora za kukabiliana na vikwazo vinavyojitokeza katika mchakato wa kuasili na malezi ya watoto hao.

Dk. Nandera alisema kuna umuhimu wa kupitiwa na kuangaliwa upya kwa sera hiyo ili kuondoa vikwazo vilivyokuwa vinasababisha kuchukua muda mwingi kwa watoto wenye uhitaji wa malezi ya familia kuungana na familia hizo.

"Watoto wapo wengi wenye uhitaji wa kusaidiwa katika jamii zetu hivyo inabidi changamoto zinazokwamisha mchakato wa watoto hao kuasiliwa zitatuliwe ili kurahisisha huduma ya malezi ya kambo na kuasiliwa," alisema.

Naye Kamishna wa Ustawi wa Jamii Msaidizi wa wizara hiyo, Baraka Makona, aliwataka wadau kutoka wizara na taasisi zinazohusika na huduma ya kuasili kubainisha vikwazo vilivyoko katika mchakato huo na njia ya kuzitatua kwa uharaka zaidi.

"Lengo ni kuwasaidia watoto kupata malezi yanayofaa hivyo pale wanapojitokeza watu wanaotaka kuwasaidia kwa kuwaasili au kwa kuwapatia malezi ya kambo pasiwe na kikwazo kitachokwamisha mchakato huo," alisema.

Ofisa Ustawi wa wizara hiyo, Zaka Olais, alitaja vikwazo vinavyokwamisha suala hilo kuwa ni kucheleweshwa kwa uchunguzi kutoka Idara ya Uhamiaji kwa raia wa nje wanaotaka kuasili watoto na kukosekana kwa vigezo maalum vya kuasili watoto wanaoishi katika makao ya kulelea watoto.



Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa, Kenani Kihongosi (katikati), akimkaribisha Naibu Katibu Mkuu mstaafu wa UVCCM Taifa ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, wakati wa uchaguzi mkuu wa 10 wa umoja huo taifa, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# RC azitaka taasisi kutunza mazingira kupanda miti

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amesema taasisi zinazotekeleza miradi jijini Dodoma zinatakiwa kutunza mazingira kwa kupanda miti ili kupendezesha Mji.

Senyamule alitoa kauli hiyo juzi alipotembelea mradi wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Dodoma katika eneo la Nala jijini humo ikiwa ni moja ya miradi mikubwa ya kimkakati inayotekelezwa jijini humo.

Alisema ujenzi wa miradi hiyo uende sambamba na kutunza uoto wa asili na kupendezesha mazingira.

Aidha, alisema ujenzi wa chuo hicho utaongeza nguvu kazi yenye ujuzi na maarifa inayohitajika kwenye uzalishaji katika maeneo mbalimbali nchini.

"Serikali ya awamu ya sita inatekeleza kwa vitendo katika kufikia malengo ya kuwa na wataalamu wenye ujuzi watakaotumika katika uzalishaji."

"Nampongeza Rais kwa maono makubwa aliyonayo anasema uchumi unaotegemea viwanda anaweka muunganiko, anajenga vyuo ili kupata wataalamu hao na nimefarijika kusikia chuo hiki kitatoa fani ya maabara hii itasaidia sana katika hospitali zetu," alisema.

Kadhalika, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, alisema utekelezaji mradi wa ujenzi wa chuo hicho ni juhudi za serikali za kuongeza ujuzi kwa vijana wa kitanzania ili kuutumia ujuzi kwenye soko la ajira hapa nchini na kimataifa kwa kujiajiri na kuajiri wengine.

"Msisitizo wa serikali yetu sasa ni elimu ujuzi, tunapitia mitaala ya shule za msingi, sekondari, vyuo vya ufundi na vyuo vikuu. Hii ni kutokana na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, tunaamini mitaala hiyo itakapokuwa tayari hata majengo yatakuwa tayari ili iweze kutumika kuzalisha ujuzi," alisema.

Prof. Nombo alitoa rai kwa Watanzania kuunga mkono juhudi za serikali kwa kupeleka vijana kusoma katika chuo hicho majengo hayo yatakapokamilika ili kupata ujuzi.

Mshauri elekezi wa chuo hicho, Mhandisi Aliki Nziku kutoka BICO, alisema kinajengwa kwa awamu mbili na utekelezaji wa mradi awamu ya kwanza ulianza Juni 2021, unatakiwa kukamilika Desemba 2022.

Alisema ujenzi unagharimu zaidi ya Shilingi bilioni saba na umefikia asilimia 75.

"Awamu ya kwanza ya mradi ikikamilika chuo kitakuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi 1,500 awamu zote zikikamilika kitadahili 3,000," alisema.

# Kampeni chanjo dhidi ya polio kuanza leo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WATOTO 695,508 mkoani Dodoma, wanatarajiwa kufikiwa na kampeni ya awamu ya nne ya utoaji wa chanjo ya kuzuia ugonjwa wa polio kwa watoto wenye umri kuanzia miaka sifuri hadi mitano inayoanza leo.

Akitoa taarifa ya utoaji wa chanjo hiyo, Ofisa Afya wa Mkoa wa Dodoma, Francis Bujiku, alisema kampeni hiyo itaanza leo hadi Desemba 4, mwaka huu.

"Awamu ya nne itafanyika kwa siku nne kuanzia Desemba 1 hadi 4, mwaka 2022 na itaenda sambamba na utoaji wa huduma zingine ikiwamo elimu ya chanjo. Tumepokea chanjo 765,059 na bajeti ya utoaji chanjo hii kwa ngazi ya mkoa ni Sh. milioni 45.5," alisema Bujiku.

Alisema kuwa ugonjwa huo ni tishio kwa miaka mingi katika nchi nyingi duniani ikiwamo Tanzania.

"Mara ya mwisho nchi yetu ilipata mgonjwa mwezi Julai mwaka 1996, hivi karibuni nchi ya Malawi ilitoa taarifa ya mgonjwa wa polio mnamo Februari 17, mwaka huu katika mji wa Lilongwe hivyo Tanzania ilionekana ni miongoni mwa nchi zilizo katika hatari kubwa ya kupata maambukizi ya ugonjwa huu na ndio sababu serikali kupitia Wizara ya Afya imefikia uamuzi wa kutoa chanjo hii kwa watoto wote wenye umri wa miaka 0-5 nchini," alisema.

Alisema chanjo hiyo kama ilivyokuwa ikitolewa kwenye awamu zilizopita, inatarajiwa kutolewa nyumba kwa nyumba ili kufikia idadi kubwa ya watoto. Aidha, Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, aliwaomba viongozi wa dini kuwatangazia waumini wote kuhakikisha watoto wenye umri huo wanapata chanjo.

"Watoaji wa chanjo watafika maeneo ya ibada hivyo wazazi wachukue fursa hiyo watoto wapate chanjo, kwenye hizo nyumba wataenda Desemba 2 na 4 mwaka huu," alisema.

Alitoa wito kwa wazazi kushiriki kikamilifu kuwatoa watoto wao wapate chanjo.

"Dodoma tumefanya vizuri katika awamu zilizopita na leo tunajadili namna nzuri ya kwenda kutekeleza awamu hii ya nne. Rais ametimiza wajibu wake kwa kutoa fedha na sisi tutekeleze jukumu hili. Nasisitiza chanjo ni salama, wazazi andaeni watoto wote," alisema.



# Watu 150 waokolewa usafirishaji haramu binadamu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Ustawi wa Jamii, Abdallah Saleh Omar, amesema usafirishaji haramu wa binadamu kwa kipindi cha mwaka mmoja Serikali ya Zanzibar imeokoa waathirika zaidi ya 150 waliokamatwa katika Bandari ya Malindi Unguja.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe katika mkutano unaohusu usafirishaji haramu wa binadamu ulioandaliwa na Taasisi ya C-SEMA kupitia mradi wa Jumuiya ya Ulaya, uliofanyika mjini hapo.

Alisema asilimia 90 ya waathirika hao ni watoto na wasichana ambao wanatoka katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na kufika Zanzibar kwa ajili ya kazi za ndani.

Alisema kuna madalali wengi wanawatoa watoto na wasichana hao kuwapeleka Zanzibar kwa ajili ya kazi za ndani na baadhi yao hukumbana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia, mateso na manyanyaso.

Alisema hatua walizozichukua ni kuwaunganisha na jamaa zao na kuwarejesha walipotoka kwa kuwagharamia nauli na chakula wakati wote wa safari.

Ofisa Mwandamizi wa Sekretariati ya kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ahmad Said Mwindat, alisema kwa Tanzania hakuna mkoa ambao upo salama katika usafirishaji huo kutokana na watu wanaokolewa.

Alisema kuna sababu mbalimbali zinazofanya usafirishaji haramu wa binadamu, ikiwamo umaskini na mbinu zinazotumika ni za ulaghai watu kuahidiwa ujira mkubwa wa kazi.

Alisema sababu zingine ni uelewa mdogo kwa jamii kuhusu wa usafirishaji haramu wa binadamu na ndoto ya kubadilisha maisha kwa kutegemea kazi zenye mshahara mkubwa.

Alisema ili kudhibiti hali hiyo lazima jamii ielimishwe na kufahamu mbinu zinazotumika za ulaghai na elimu kwa vyombo vya ulinzi na usalama ili kugundua mitandao ya kihalifu inayojihusisha na biashara hiyo na wanaohusika kukamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mwenyekiti wa Mtandao wa kitaifa wa kuzuia usafirishaji haramu Tanzania, Edwin Mgambila, alisema hali ya usafirishaji haramu nchini sio nzuri kama zilivyo nchi zingine, kuna vitendo vilivyokithiri kwa wasichana wa kazi za ndani kuchukuliwa mkoa mmoja na kwenda mwingine au nje ya nchi. Alisema wasichana hao hupitia katika manyanyaso na mateso makubwa wanapotumikishwa bila ya kupewa ujira na wingine hupoteza maisha, huathirika kiafya na baadhi yao hupata maradhi ya ngono.

Alisema usafirishaji haramu wa ndani ni mkubwa zaidi kuliko wa nje ya nchi na maeneo yanayoongoza ni maeneo ya kazi za ndani, sekta ya ngono kwa kushirikishwa katika kazi za saluni ikiwamo kufanya masaji, sehemu za starehe na sekta za uzalishaji kama sekta ya uvuvi na viwanda.

Alisema sababu kubwa ya biashara hiyo kunawiri duniani ni thamani iliyonayo na takwimu za serikali ya Marekani ya ripoti ya mwaka 2021 inaonesha kuwa biashara ya usafirishaji haramu ya binadamu inawatengenezea wanaofanya biashara hiyo zaidi ya Dola bilioni 150 kwa mwaka.

Alisema serikali imechukua jitihada mbalimbali na kwa sasa sheria ya usafirishaji haramu wa binadamu imepewa meno zaidi na adhabu kali ikiwamo adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela kwa kumsafirisha mtu mzima na kumsafirisha mtoto au mtu mwenye ulemavu ni kifungo cha maisha.

## Mwinyi aenda Makka kutekeleza Ibada ya Umrah

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amewasili katika mji Mtukufu wa Makka Saudi Arabia kwa ajili ya kutekeleza Ibada ya Umrah.

Ibada ya Umrah ni kuizuru ama kuitembelea Nyumba Takatifu (Alkaba) wakati wowote mtu anapotaka, kwa kutekeleza matendo ya ibada maalumu kwa mujibu wa imani ya Dini ya Kiislamu.

Katika ujumbe aliofuatana nao kwa kutekeleza ibada hiyo, Dk. Mwinyi ameambatana na mkewe mama Mariam Mwinyi.

Wengine alioambatana nao ni Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Alhaj Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, Balozi wa Tanzania nchini Saudi Arabia, Ali Mwadini pamoja na viongozi wingine waandamizi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ibada hiyo hufanywa katika Mji Mtakatifu wa Makka pekee ambako ndiko zinakoelekea nyoyo za Waislamu wote popote walipo duniani katika hali ya unyenyekevu.



Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Mifugo, Asha Zahran Mohamed (kulia), akizindua chanjo ya kichaa cha mbwa katika kisiwa cha Uzi, Mkoa wa Kusini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mbwa watakiwa kuchanjwa kudhibiti kichaa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI Idara ya Maendeleo ya Mifugo, Asha Zahran Mohamed, amesema ili kudhibiti athari za kichaa cha mbwa ni lazima wote wachanjwe ili kuepusha maambukizi ya ugonjwa huo.

Aliyasema hayo jana katika uzinduzi wa zoezi la kampeni ya chanjo ya kichaa cha mbwa kwa mbwa wote Zanzibar ambapo uzinduzi huo umefanyika katika Kisiwa cha Uzi Unguja.

Alisema chanjo itadumu kwa muda wa siku 10 hadi Desemba 9, mwaka huu na inatolewa bila ya malipo na kuwataka wafugaji kupeleka mbwa wa kupata chanjo katika kila shehia wataalamu wa afya ya mifugo watawafikia.

Alisema ugonjwa wa kichaa cha mbwa ni hatari na unaathiri pia afya za binadamu endapo mtu atang'atwa na mbwa mwenye kichaa.

Alisema, chanjo hiyo itawasaidia wafugaji na kuwaomba kutodharau chanjo hiyo ambayo itawarahisishia kupata huduma hiyo bila malipo.

"Tumeanza zoezi hili katika kisiwa hichi cha Uzi kwa sababu hufikiwa mara chache kutokana na jiografia yake na zoezi hili tunatarajia kuchanja mbwa 200 kwa kisiwa hiki tu cha Uzi," alisema.

Alisema uwapo wa chanjo hiyo kila mwaka umesaidia kupunguza matokeo ya watu kutafunwa na mbwa wenye kichaa.

Naye Daktari Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Mifugo, Ali Zahran Mohamed, alisema ugojwa huo ni hatari na pia unampata binadamu, atakapong'atwa na mbwa aliyeathirika na ugonjwa huo na kuchelewa kupata tiba husababisha kufariki dunia.

Alisema wafugaji wa mbwa wanatakiwa kuzingatia elimu wanayopewa na athari za ugonjwa huo ili kuutokomeza.


"Lengo letu ni kufikia asilimia 70 ya mbwa wote waliopata chanjo ili kuondosha ugonjwa huo hatari na tunakadiria kuchanja mbwa 11,000 Unguja na Pemba ambapo kwa Pemba ni mbwa 20,00 na unguja 90,00," alisema Dk. Zahran.

Alisema kuna tatizo la mwitikio wa wafugaji kuwa mdogo, lakini kutokana na juhudi za idara ya mifugo kwa kuwashirikisha masheha katika kutangaza kampeni hiyo imesaidia kushajihika na mbwa wao kupata chanjo.

Mjumbe wa sheha ya shehia ya Uzi, Badru Aboudu Salum, alisema wamepata faraja kubwa kufikiwa na madaktari hao ili mbwa wote walioko katika kisiwa hicho wapatiwa chanjo hiyo na kuwakinga wananchi na ugonjwa wa kichaa.

Mfugaji wa mbwa, Abubakar Haroub, aliwataka wafugaji wenzake kutodharau chanjo hiyo ili kuepusha athari.

Chanjo dhidi ya kichaa cha mbwa inatekelezwa na Serikali ya Zanzibar kupitia ufadhili wa Shirika la Kudhibiti ugonjwa hatari wa kichaa cha mbwa duniani.





# Wanafunzi waingiwa hofu wazazi kuwaoza kimya kimya

**Na Shaban Njia,**
SHINYANGA

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Lyamidati, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wameingiwa na hofu ya kushindwa kuhitimu masomo yao baada ya baadhi ya wazazi na walezi wenye tamaa na mali kuanza kuwaozesha kimya kimya kwa wanaume wasiowapenda waishio vijijini pamoja na kata jirani.

Baadhi ya wanafunzi hao walizungumza na gazeti hili, wakati wa utekelezaji wa Mradi wa Sauti za Kaya na vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, unaotekelezwa na SPC kupitia Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Mmoja wa wanafunzi hao wa darasa la sita, Jenifa Samweli alisema, kuna mwanafunzi mwenzake aliacha shule wakiwa darasa la tano na kwenda kuolewa kitongoji jirani cha Mwankulwe na mtu mzima, baada ya wazazi wake kupokea mahali ya ng'ombe hali iliyosababisha kukosa masomo yake mpaka sasa.

Alisema, wengine mapacha wawili walifaulu mtihani wa kuingia kidato cha kwanza mwaka wa masomo 2020, lakini walishindwa kuendelea na masomo na kuolewa na wanaendelea kulea familia zao na kuomba serikali kuingilia kati na kuwachukulia hatua kali za kisheria wazazi wenye tamaa wanaokatisha ndoto za wanafunzi.

Mwanafunzi mwingine Aisha Saidi alisema, kuna wakati wazazi wanawalazimisha kubeba mimba na mwanaume waliomchagua ili akibainika ni mjamzito aache shule na kwenda kuolewa, wanashindwa kutoa taarifa katika uongozi wa shule au ofisi ya mtendaji wa kata kwa kuogopa kupigwa na wazazi.

"Mimi kuna mwanafunzi namfahamu amemaliza mitihani hivi karibuni ya kuhitimu elimu ya msingi akiwa mjamzito, na naingiwa na hofu matokeo yatakapotoka na akabainika amefaulu sijui ataendelea na masomo au ataendelea kulea familia yake."

Naye Diwani wa Kata ya Lyamidati Veronika Nduta, alikiri kuwapo kwa matukio ya ukatili wa kijinsia hususani kwa wanafunzi na wasichana na amekuwa akiyakemea kupitia mikutano ya hadhara anayoifanya, kuwasihi wenyeviti wa vitongoji na vijiji kupitia kikao ya maendeleo ya kata kupinga vikali vitendo hivyo.

Alisema, hivi karibuni kuna binti alibakwa na fundi kinyozi na alipopata taarifa aliingilia kati na kuhakikisha mhusika anachukuliwa hatua za kisheria, licha ya wazazi wake kumtishia, lakini hakukata tamaa, alihakikisha amefikishwa kituo cha polisi kwa hatua nyingine za kisheria.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa kata, Irene Mchuma alisema, wananchi wanashindwa kutoa taarifa ya matukio ya ukatili wanaofanyiwa ndani ya familia kwa kuogopa kutengwa na koo zao na ili kuondoa dhana hiyo wamejiwekea utaratibu wa kupita kila kaya na kuwapatia elimu ya ukatili wa kijinsia.



Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, akikata utepe kuzindua baraza huru litakaloshughulikia malalamiko ya wananchi wanaozunguka mgodi wa Almasi Mwadui. Kushoto ni Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Petra Diamond inayomiliki mgodi huo, Richard Duffy. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mgodi wafungua ukarasa mpya kuimarisha uhusiano

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MGODI wa Almasi wa Mwadui wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga (Williamson Diamond), umeweka mikakati ya kuanza ukurasa mpya wa kuimarisha uhusiano mzuri na wananchi wanaouzunguka mgodi huo, kwa kuwalipa fidia waliopata madhira mbalimbali kupitia mgodi.

Mgodi wa Mwadui kupitia Kampuni ya Petra Diamond Limited ambao kwa sasa ndio wamiliki wake, juzi ulizindua baraza huru ambalo litakuwa likishughulikia malalamiko ya wananchi waliopata madhira ndani ya mgodi huo kwa kuyatafutia ufumbuzi wa njia ya usuluhishi na kulipwa fidia.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alisema wananchi waliopata madhira mbalimbali kupitia mgodi wa Mwadui kilio chao kimesikika na watapata haki zao. "Baraza hili huru la kushughulikia malalamiko ya wananchi wanaozunguka mgodi wa Mwadui, nendeni mkatende haki kwa wananchi juu ya madhira waliyoyapata kupitia mgodi wa Mwadui na kuwapatia haki zao," alisema Mkude.

Mbunge wa Jimbo la Kishapu, Boniphace Butondo, alisema baraza hilo ndio mwisho wa migogoro baina ya wananchi na Mgodi wa Mwadui, litakuwa kiungo cha kuanzisha ukurasa mpya wa kuimarisha uhusiano mzuri na hakutakuwa na masuala ya ukiukaji wa haki za binadamu.

Mwenyekiti wa Baraza hilo Dk. Rugemeleza Nshala, alisema baada ya kukithiri malalamiko ya wananchi dhidi ya Mgodi wa Mwadui ikiwamo vipigo na kukiuka hadi za binadamu, liliundwa Baraza huru ambalo litakuwa likishughulikia malalamiko ya wananchi kwa njia ya usuluhishi na kuwalipa fidia.

Alisema mpaka sasa walishapokea malalamiko 5,575 kutoka kwa wananchi wa vijiji 12 wanaouzunguka mgodi huo kuhusu madhira wanayoyapata kupitia mgodi huo, na wataanza kuyashughulikia moja baada ya jingine kwa njia ya usuluhishi na kupata haki zao kwa kulipwa fidia.

Alisema pia mgodi umeongeza muda wa kupokea malalamiko ya wananchi ambao walipata madhira kupitia mgodi huo, kuanzia watu wa mwaka 2009 hadi Mei 2021 wanaruhusiwa kuwasilisha malalamiko yao.

Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Petra Diamond, Richard Duffy, wamiliki wa Mgodi wa Mwadui kwa sasa, alisema lengo kuu la kuunda baraza hilo huru la kushughulikia malalamiko ya wananchi, ni kufikia maridhiano na kuimarisha uhusiano mzuri baina ya wananchi na mgodi.

## Ujenzi kituo jumuishi taasisi za kisheria kujengwa

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAZIRI wa Sheria na Katiba, Dk. Damas Ndumbaro, ameweka jiwe la msingi kwenye ujenzi wa kituo jumuishi cha taasisi za kisheria za serikali mkoani Mwanza kitakachogharimu Shilingi bilioni 3.8.

Akizungumza katika warsha hiyo alisema lengo la serikali kujenga miundombinu ya vituo jumuishi vya utoaji haki inalenga huduma zote za kisheria kwa wananchi na wadau wengine, kutolewa eneo moja zikiwamo za msaada wa kisheria na ustawi wa jamii matumizi ya huduma mtandao.

Alisema dhima ya wizara ni kutumia katiba na sheria kuleta maendeleo, bila katiba hakuna serikali wala taasisi ambapo kila mtu atafanya yake na kusisitiza wizara na taasisi zake ni kusimamia sheria, kuleta amani na utulivu ili kuleta maendeleo.

Alimwagiza mkandarasi kukamilisha kwa wakati, ufasaha na umakini mradi huo na ajira zitolewe kwa vijana wazawa pia serikali imefanya mambo makubwa yakiwamo kuimarisha na kujenga miundombinu ya utoaji haki na kuwawezesha wananchi kupata huduma kwa karibu na gharama nafuu.

Naye Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dk. Eliezer Feleshi, alisema dhamira ya kusogeza huduma karibu na wananchi na kuziwezesha taasisi za kisheria za serikali na wizara pamoja na wadau muhimu kuwa pamoja na kuongeza tija katika utoaji huduma.

"Mpango huu utafanikisha kazi zinazofanywa na mahakama mtandao pamoja na kuondoa changamoto zinazozikabili ofisi zetu kwa sasa katika maeneo yenye mahakimu wengi kuliko mawakili wa serikali pia mpango huu utawezesha huduma zitolewazo na taasisi zetu kupatikana katika eneo moja," alisema Feleshi. Serikali inajenga vituo jumuishi vya kisheria kuziwezesha taasisi zake za kisheria kuondokana na tatizo la kukosa miundombinu ya ofisi ili kutoa huduma bora kwa umma.

Awali, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria, Khatibu Kazungu, alisema mradi huo umetafsiri kwa vitendo Dira ya Wizara 'Katiba na Sheria Wezeshi kwa Maendeleo ya Taifa' una faida kubwa katika utoaji wa huduma si tu za kisheria, unaongeza ubora, mapato ya serikali, kukuza uhusiano na taasisi zingine na kuwapunguzia umbali wananchi kufuata huduma.

Alisema wizara itatoa ushirikiano mkubwa katika kuhakikisha ujenzi wa jengo hilo unamalizika kwa wakati na huduma zinazotolewa pia wizara wamejipanga kujali taasisi zote zilizoko chini ya wizara inayoiongoza zinatimiza majukumu yake ya kutoa huduma za kisheria kwa ubora unaotakiwa.

"Natoa rai kwa taasisi nyingine zilizoko chini wa wizara kuanzia kufikilia kujenga majengo Jumuishi ya Ofisi ili huduma zote zinazosimamiwa na wizara zipatikane sehemu moja na wakati wanaweka mipango yao ya ujenzi wa ofisi za taasisi zetu ni vyema tukashtakiana katika hatua za awali kabisa," alisema Kazungu.

Akisoma taarifa fupi ya ujenzi huo, Mkurugenzi wa huduma za ushauri TBA, Wencelaus Kiziba, alisema utekelezaji wa mradi huo katika hatua ya ujenzi umefikia asilimia 35 ya kazi zote za mkataba, utekelezaji katika huduma za ushauri elekezi kabla na baada ya mkataba umefikia asilimia 50 pia muda wa mradi uliotumika ni miezi saba kati ya 18 sasa na asilimia 39.

HABARI KIMATAIFA

# Mawaziri NATO waijadili Russia

**BUKAREST, Romania**

MWAZIRI wa Mambo ya Nje wa nchi wanachama wa jumuiya ya kujihami ya NATO, wameanza mkutano wa siku mbili nchini Romania.

Mkutano huo una lengo la kutathmini njia za kuimarisha ulinzi katika mipaka yake ya mashariki, wakati mvutano na Russia ukishamiri.

Katibu Mkuu wa NATO Jens Stoltenbeg, aliuambia mkutano huo kuwa jumuiya hiyo haipaswi kuchoka kuiunga mkono Ukraine.

Mawaziri wanaokutana watazungumzia pia mipango ya dharura ya kuisaidia sekta ya nishati ya umeme kwa Ukraine iliyosambaratishwa na mashambulizi ya Russia. Stoltenberg amesisitiza kuwa nchi hizo tayari zimefanya makubwa katika kuipelekea Ukraine majenereta na vipuri vya kukarabati mitambo yake iliyoharibiwa.

Awali, Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy aliwaweka tayari raia wa nchi yake kujiandaa kwa kipindi kigumu cha majira ya baridi.

Wakati huo huo, Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz, amesifu makubaliano kati ya nchi yake na Qatar kuhusu mauzo ya gesi ya kusindika, akisema yatakuwa msingi wa juhudi za nchi yake kufikia usalama wa nishati. Makubaliano hayo yaliyofikiwa Jumanne yatawezesha usafirishaji wa gesi iliyobadilishwa katika mfumo wa kimiminika kusafirishwa kwa meli kutoka Doha hadi bandari maalumu iliyojengwa kwenye pwani ya kaskazini mwa Ujerumani.

Ujerumani inapambana kutafuta msambazaji mbadala wa gesi baada ya Russia kukatisha usambazaji wa bidhaa hiyo kwa Ujerumani wakati wa vita vya Ukraine vinavyoendelea.

Usambazaji wa gesi hiyo kutoka Qatar utaanza mwaka 2026 ingawa haikutajwa gharama.

Kwa upande mwingine, mfanyabiashara wa Russia, Yevgeny Prigozhin, na mshirika wa karibu wa Rais Vladimir Putin, amesema mwanafunzi wa Zambia aliyefariki nchini Ukraine alikuwa akipigana katika kundi lake la Kijeshi la Wagner.

Awali Zambia ilisema inahitaji kupata taarifa kutoka serikali ya Russia jinsi mwanafunzi huyo, Lemekhani Nyirenda (23), alivyotoka kutumikia kifungo karibu na mji mkuu wa nchi hiyo hadi alipofariki vitani mwezi Septemba.

Baba yake Nyirenda alisema mwanawe alikuwa akitumikia kifungo cha miaka tisa jela nje kidogo ya jiji la Moscow kwa kosa la kutumia dawa za kulevya wakati alipoandikishwa kupigana.

Familia yake ilisema haikuwa wazi jinsi alivyoajiriwa au na nani.

Siku ya Jumanne, kundi la Prigozhin lilisema Nyirenda alikuwa ameajiriwa na Wagner.

Kumekua na madai kuwa Prigozhin na wawakilishi wengine wa Wagner wamezuru magereza ya Russia yanayotoa msamaha kwa wahalifu kujisajili kupigania Russia nchini Ukraine.

"Ndiyo, namkumbuka vizuri mtu huyu," alisema Prigozhin wakati akijibu swali kutoka kwa mwandishi wa habari kama Mzambia huyo alikuwa akipigana na Wagner.

Prigozhin alisema Nyirenda alikufa kama shujaa na kwamba alikuwa mmoja wa watu wa kwanza kuingia kwenye mahandaki ya adui mnamo Septemba 22.

Shirika la habari la Reuters linasema halikuweza kuthibitisha mazingira ya kifo cha Nyirenda au madai ya Prigozhin kwamba alijiunga na Wagner kwa hiari.

***DW***

# Aliyemuua Chris Han achomwa kisu gerezani

**PRETORIA, Afrika Kusini**

JANUSZ Walus, ambaye alishambulia kwa risasi na kumuua mpinga ubaguzi wa rangi nchini Afrika Kusini, Chris Hani, amedungwa kisu akiwa gerezani.

Shambulizi hilo la kisu kwa Walus linakuja siku chache kabla ya kuachiliwa kwa msamaha baada ya takriban miaka 30 akiwa jela.

Inadaiwa alipigwa kisu na mfungwa mwenzake na hali yake inaendelea vizuri.

Walus (69), alimpiga risasi Hani mwaka wa 1993 katika jaribio lililofeli la kuvuruga mpito wa Afrika Kusini kutoka utawala wa wazungu wachache hadi utawala wa kidemokrasia.

Mauaji hayo bado yanaibua hisia kali nchini Afrika Kusini. Hani alichukuliwa kuwa mwanasiasa maarufu zaidi baada ya Rais wa kwanza na mpigania Uhuru Nelson Mandela.

Serikali ya Afrika Kusini na mjane wa Hani Limpho walipinga vikali majaribio ya Walus kuachiliwa huru, lakini katika uamuzi wa tarehe 21 Novemba, mahakama ya juu zaidi ya Afrika Kusini iliamuru kuachiliwa ndani ya siku 10.

Katika taarifa fupi, idara ya magereza ilisema inaweza kuthibitisha kuwepo kwa tukio la bahati mbaya la kuchomwa kisu Walus.

Hata hivyo, maofisa wa afya walikuwa wakimpa huduma muhimu.

BBC ina taarifa kuwa mshambuliaji wake alijaribu kumdunga kisu kwenye moyo ili kumuua.

Shambulio hilo lilijiri baada ya mnara wa kumbukumbu ya Hani kuharibiwa siku ya Jumamosi katika makaburi aliyozikwa.

Chama tawala cha African National Congress (ANC) na washirika wake walilaani tukio hilo na kueleza ni shambulio la uchochezi, na sawa na muendelezo wa mauaji ya Chris Hani kaburini.

Walus alimuua Hani alipokuwa akiokota magazeti nje ya nyumba yake mnamo Aprili 1993 kwa kumpiga risasi kwa kumlenga moja kwa moja.

***BBC***

NELICO

NEW LIGHT CHILDREN CENTRE ORG.

*P.O. Box 160\Geita –Tanzania \Tel: 0800-751030 admin@nelicotz.org\ Web..www.nelicotz.org*

**RFP Title: Procurement of educational subsidies and printing of ART calendars.**
**Tender No: NELICO/ACHIEVE/FY23/01**

**Date of Solicitation: 01/12/2022**
**Closing date and time: 15/12/2022 11:00 am (Geita Tanzania)**
**Questions and clarifications: Due by 12/12/2022**

**1.0 Introduction:**

New Light Children Centre Organization (NELICO) is a non-profit organization registered under the Non-Governmental Organizations Act No. 24 of 2002 on March 28, 2006 and awarded with registration certificate No. 00NGO/0739. NELICO started its operations in Geita Region in March 2004 as an organization focusing on support to Orphans and Most Vulnerable Children. Starting of the organization was motivated with the desire to address the issues of HIV/AIDS, Tuberculosis and orphans in the mining areas of Geita Region.

Up to date, NELICO is implementing programs related to: HIV/AID's prevention, SRHR, GBV and VAC prevention, quality education, disability inclusion, Free Legal Aid, protecting girls against harmful practices and Economic strengthening to communities from the 5 regions of Lake Zone (Geita, Shinyanga, Simiyu and Mwanza). **In October 2022 NELICO** received funding from USAID through PACT partnership to implement ACHIEVE PROJECT in Geita Region covering 6 councils (Geita Tc, Geita Dc, Bukombe Dc, Chato Dc, Mbogwe Dc & Nyang'wale Dc) while 3 councils for Shinyanga Region (Kishapu Dc. Shinyanga Dc and Shinyanga Mc).

Adolescents and Children HIV Incidence Reduction, Empowerment, and Virus Elimination (ACHIEVE) is a five-year global effort to reach and sustain HIV epidemic control among pregnant and breastfeeding(PBF) women, infants, children and youth, as well as to mitigate the impact of HIV/AIDS and prevent HIV transmission among these populations.The project is funded by the U.S. Agency for International Development (USAID) and implemented by a Pact led consortium of top global HIV/AIDS partners, including Jhpiego, Palladium, No Means No Worldwide, and WI-HER

**2.0 Objective of the Assignment**

The overall objective of this assignment is to procure education subsidies (comprised of 5 exercise books, 5 pens, 5 pencils, 1 mathematical set and a small bag) for **14,958 DREAMS** beneficiaries from 2 DREAMS councils and **printing of 6,748 ART Uptake calendars** for monitoring of ART daily uptake for C/ALHIV who are on ART.

**3.0 Items to be supplied**

Items to be supplied are categorized into two lots (2) as below:

**LOTS 1 & 2**

| Item | Description of item | Number of items per kit |
|---|---|---|
| Educational subsidies | To be assessed in the TOR | 14,958 educational subsidies kits |
| ART Calendars | To be assessed in the TOR | 6,748 calendars |

**HOW TO ACCESS MORE INFORMATION ON TOR:**

Interested vendors should download the full Terms of Reference (ToR) through **NELICO** website www.nelicotz.org by assessing the **MORE** section then click **TENDERS** and through **NEWSLETTER** section at the bottom.

All questions and requests for clarifications should be directed procurement@nelicotz.org with the subject line Request for clarifications as per RFP Title.: S***upply Educational subsidies and ART Calendars before 1200hrs on December 12, 2022.***

**Eligibility**

For qualified awarded vendor must currently be legally operating in Tanzania and Quotation must include the following information

- Ability to meet the requirements or technical specifications
- Legally registered in Tanzania
- Ability to deliver items/services on time

**Evaluation criteria**

- Price
- Financial capability
- Experience
- Quality of items to be supplied
- Delivery terms

17173302

**Submission instructions.**

Interested dealers must submit the following information to NELICO:

- Draft inception report detailing the methodology for supplying and distributing of educational subsidies and ART calendars as per LOT 1 and LOT 2 item description including tentative Workplan, for review and approval by NELICO.
- Quote, valid for at least 60 days
- Current company profile.
- Copies of the registration certificate and address of their registered office, valid business license, VAT, TIN certificates and Tax clearance certificate.
- Items specifications are fully addressed in the quotation.
- Current Audited financial statement for two consecutive years.
- Evidence of similar assignments, and at least two (2) PO or contract and names and addresses of clients served.
- Delivery time must be specified.
- Payment's term is 100% after delivery.
- Current Audited financial statement for two consecutive years.
- Artwork on LOT 2 (ART calendars should be requested through inquiries **procurement@nelicotz.org**.

Interested bidders should address their applications.

- **The Tender Committee NELICO Bomani -NELICO Street, P. O. Box 160, Geita, Tanzania**

All quotes must be in Tanzanian Shillings with taxes separately and should be enclosed in a plain sealed envelope since electronic bids will not be accepted. The deadline is **11:00hrs (11:00 am) EAT Thursday 15th December 2022.**

**Note: Shortlisted vendors will be required to submit samples that will be provided upon NELICO confirmation.**

- NELICO will open all bids on **15th December 2022 at 12:30 pm** in the presence of all bidders' representatives at their discretion.

**Please note, each lot that the dealer/vendor is interested in must be a separate submission that includes all the requirements listed above.**

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

PAKEMA INTERNATIONAL LIMITED
Dealers in: General Auctioneers, General Brokers, Count Brokers, Tribunal Brokers, Debt collections, Engineering constructions, cleaning services, Fumigation services, Land developers, Supplies and Manufacturers Representatives.
Head office: Station road, pakemainternational@gmail.com
P.O. Box 3115,
Mob: 0754| 0715 477 982 |
MOROGORO - TANZANIA

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliopewa na Meneja wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) Morogoro. Tutauza vitu/vifaa mbalimbali kwa mnada wa hadhara vilivyotolewa kwa wapangaji walioshindwa kulipa kodi ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) Morogoro vifuatavyo:-

**Kabati za nguo, kitanda , Godoro, Dressing Table, Masanduku ya kuifadhia nguo, ndoo , mtungi wa 6kg, makochi, stuli, Kontena futi 40 na vitu vingine vingi**

Mnada utafanyika kwenye yadi yetu ilioko barabara ya **SUA** maeneo ya Msufini na Hoteli ya Acropal barabara old Dar es salaam Morogoro tarehe 15/12/2022 muda ni kuanzia saa 4.00 asubuhi

**MASHARTI YA MNADA**

* Mnunuzi atalazimika kulipa bei iliyofikiwa papo hapo baada ya nyundo ya dalali kutua
* Endapo mnununzi akishindwa kulipa itauzwa upya.
* Kifaa/vitu vinauzwa kama vilivyo

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI KWA SIMU NAMBA 0754477982/ 0715477982**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALLY ABDALLAH KAHTAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 812 DMK** aina ya **MITSUBISHI- CANTER,** Chasis **No. FE652G540517,** Engine **No. 4D33Z415GT.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi **MWA/IGO/RB/461887/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALLY ABDALLAH KAHTAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 588 DME** aina ya **COMBINE HARVESTER,** Chasis **No.DC70HVN506981,** Engine **No. VZ403BHS2055.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi **MWA/IGO/RB/461895/2022.**

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 125 OF 2022**

**In Matter of the Estate of the Late TIMOTHY ROBERT KASELE**

**By 1. DIANA ALLY KASELE**
**2. ..................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grand should be field on or before the **19th** day of **December / 2022.**
Dated at **Morogoro**, this **22nd** day of **NOVEMBER 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA Mkoa TANGA**
**Usimamizi wa mirathi na 233|2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ABDALLAH HILALI**
**KATIKA SAHURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIOLETWA NA SOUD ABDALLAH HILALI**

### TANGAZO

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama zamwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa Hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 7 Mwezi 12 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehem anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetotewa leo tarehe 29 Mwezi 11 mwaka 2022**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**KEEWAY MOTOR TANZANIA LIMITED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA KEEYWAY CHASSIS NAMBA **IBBPEK9H01BB79781** ENGINE NAMBA **QJ162FMJ2B0239818.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/461537/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI

**SHINING LIGHT MINISTRIES OF TANZANIA** wanatangaza kupotea kwa Certificate of Registration yenye namba **6291.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/460377/2022**

# NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| UBUNGO | UYACODE VICOBA PROGRAM | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI KNDO 29299-KND/MBR/MWZ/10/2 | UYACODE VICOBA PROGRAM HQ | MAKUBURI UBUNGO | 16/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | LILIAN CLAUDY KANJE | NYUMBA YENYE HATI NAMBA 145001 | LILIAN CLAUDY KANJE | KIGOGO- MANISPAA YA KINONDONI | 15/12/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 16/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | JUMA NURU MUSHI | NYUMBA | JUMA NURU MUSHI | MBAGALA KUU | 16/12/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | SALMA HASSAN RAJAB | NYUMBA | SELEMAN KAFOKOMA | MBEZI MSAKUZI | 20/12/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | HAPPYNESS GEORGE MKOPI | NYUMBA YENYE HATI NAMBA 65739 | PATRICK SAMWEL NGAYIWA | MTONI KIJICHI | 15/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | NICE CHANDEMOHAMED | NYUMBA | ROSEMARY DESDELIUS HAULE | KWA AZIZI ALLY | 20/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | SASI SELEMANI KITUNDU | NYUMBA | MWAJUMA SELEMANI KITUNDU | GOBA KUNGURU | 19/12/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | MARYAN GENERAL SUPPLIES | NYUMBA | MARYAN KAPAMA | KIMARA TEMBONI | 21/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | ALLY NASSORO KIMBUGU | NYUMBA | NASSORO MOHAMED KIMBUGU | GOBA KINZUDI | 15/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | CHEX ENGINEERING LTD | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NAMBA 110 KITALU '15' NA HATI NAMBA 69065 | CHEDIEL GASPER MSHANA | BUNJU-KINONDONI | 16/12/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | MADALE KIDS PALACE | NYUMBA YA BIASHARA NYENYE HATI MILIKI | CRUCIAL INVESTMENT LIMITED | MADALE | 16/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | MAMU PHARMACY | 1.NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.151,KITALU 'Q10' HATI NAMBA 143195-KIBAMBA 2.1.NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.1123 KITALU 'L' HATI NAMBA 85726-MBAGALA 3.NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO-CHAMAZI DOVYA | AHMAD KASSIM OMARY | 1.KIBAMBA 2.MBAGALA 3.CHAMAZI DOVYA | 02/12/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA ( MARUDIO) |
| TEGETA | BUMERA LODGE AND CO. LTD | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | JOACHIM HERONIMUS MWINGIRA | MTAA WA KIGOGO KATI-KINONDONI | 21/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | MPOKI BROWN MWAIPASI | NYUMBA (2) | MPOKI BROWN MWAIPASI | 1.GONGOLAMBOTO 2. KILUNYA | 15/12/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 15/12/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | MWANJELWA , MBEYA MJINI | 16/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | JONATHAN ZAWADI MHANDO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JONATHAN ZAWADI MHANDO | MBEZI MSAKUZI | 15/12/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | OSCAR JOSSEY MUNIS | NYUMBA | VERAELI ELIYA KOMBE | MWANANYAMALA -KINONDONI | 16/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | FELIX BIRCKMAS ALOYS | NYUMBA (3) | 1.FELIX BIRCKMAS ALOYS 2.KASSIAN ANTHON NINDI 3.BOSCO ULIRICK TARIMO | 1. MBEZI KWA YUSUFU 2.TABATA KISUKULU 3.MANZESE | 19/12/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |


**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0714939933/0765999000/0712926881/0718038313/0752360133**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

17173402

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# SMITH AELEZA SABABU KUMPIGA KIBAO ROCK



NYOTA wa muvi na muziki wa Marekani, Will Smith, amesema hasira yake ndiyo iliyosababisha kumpiga kibao mchekeshaji, Chris Rock, kwenye jukwaa la tuzo za Oscar zilizofanyika Machi, mwaka huu, imefahamika.

Mwigizaji huyo amehojiwa kwa mara ya kwanza tangu tukio hilo, ambalo alilitaja kuwa "usiku wa kutisha".

Akiwa kwenye kipindi cha The Daily Show na Trevor Noah, alisema: "Nilikuwa nikipitia jambo fulani usiku huo, unajua?

"Si kwamba hiyo inahalalisha tabia yangu hata kidogo," alisema Smith.

"Kulikuwa na mambo mengi na matatizo yake na mimi tu."

Smith alivamia jukwaa kwenye hafla ya tuzo ya Hollywood baada ya Rock kufanya mzaha kuhusu kunyolewa kichwa kwa mke wa Smith, Jada Pinkett Smith.

Hapo awali alikuwa amesema mkewe hakumwomba amkabili Rock.

"Nadhani ningesema ni huwezi kujua mtu anapitia nini," alisema, bila kufafanua kile alichokuwa akirejelea.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Smith kuhojiwa hadharani kuhusu shambulio hilo.

"Ninaelewa jinsi hiyo ilivyokuwa ya kushangaza kwa watu … nilikuwa nimeenda. Hiyo ilikuwa hasira ambayo ilikuwa imebanwa kwa muda mrefu sana," alimwambia Noah.

"Huo ulikuwa usiku wa kutisha, kama unavyoweza kufikiria."

# NAVYKENZO KUACHIA NGOMA LEO



WASANII wa muziki wa Bongofleva Nahreel na Aika, Navy Kenzo, wanatarajia kuachia ngoma yao mpya leo.

Kwa mujibu wa taarifa yao, ngoma hiyo wamemshirikisha Fireboy DML kutoka Nigeria.

"Tunatangaza Alhamisi kundi la Navy Kenzo litaachia kolabo yetu na mwimbaji nyota toka Nigeria, Fireboy DML," ilisema taarifa yao.

Nahreel na Aika ambao ni wapenzi waliojaliwa watoto wawili hadi sasa, wanatamba na ngoma yao Manzese ambayo inaonekana kupokelewa vizuri sana.

Wimbo huo unaweza kuwa wakufungia mwaka huu.



# ROTIMI

## ANATAKA WATOTO WENGI NA VANESSA

MWIGIZAJI na mwanamuziki wa Marekani, Olurotimi Akinosho, almaarufu Rotimi amefichua sababu kwa nini anataka kuwa na watoto wengi.

Akizungumza kwenye video iliyochapishwa kwenye ukurasa wake wa Instagram, Rotimi alikiri yeye ni mtoto wa pekee katika familia yao na kumemfanya kutaka kuwa na watoto wengi.

Mume huyo wa malkia wa Bongofleva, Vanessa Mdee aliweka wazi hataki mwanawe awe peke yake.

Rotimi na Mdee wana mtoto wa kiume mwenye umri wa mwaka mmoja na wanatarajia mtoto wao wa pili, wa kike.

"Kwa hiyo nataka mwanangu (Seven Adeoluwa Akinosho) awe na mtu ambaye anaweza kumtegemea, ambaye anamwangalia," alieleza.

"Wanajua watakuwa pale kwa ajili yake. Binti yangu akiangalia upande wake wa kulia, anajua ana kaka mkubwa ambaye anapitia jambo lile lile katika umri huo huo."

Rotimi aliongeza hakutaka kusubiri muda mrefu sana kupata watoto.

"Unajua sikutaka lile pengo la miaka sita, saba ambapo kimsingi ni watoto tu, kwa hiyo nilitaka wawe karibu sana kiumri na Vanessa alielewa na yeye alitaka jambo hilo hilo."

# NTIBAZONKIZA AITAJA YANGA AKIWA TAYARI KUTUA SIMBA

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa Geita Gold FC, Saido Ntibazonkiza, amesema hashangazwi na taarifa kuhusiana na yeye kujiunga na Simba na kuongeza soka ni kazi yake na yuko tayari kucheza timu yeyote itakayomhitaji.

Ntibazonkiza ni miongoni mwa wachezaji wanaohusishwa kutakiwa na Simba katika usajili wa dirisha dogo linalotarajiwa kufunguliwa kuanzia Desemba 16, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, kiungo huyo alisema amesaini mkataba wa mwaka mmoja na Geita Gold FC na sasa umebaki wa miezi sita na kama kuna timu inamhitaji yuko tayari kwa sababu anatambua soka ni kazi yake.

Mrundi huyo alisema endapo Simba watahitaji huduma yake yuko tayari kwa sababu anaamini riziki yake ya kujiunga na klabu hiyo itakuwa imefika au kwenda katika timu nyingine ndani au nje ya Tanzania.

"Soka ni kazi yangu, wakinihitaji nitakuwa tayari kwa sababu itakuwa riziki yangu nimepangiwa na Mungu ambaye anajua kesho yetu, hayo mengine ni utashi wa mwanadamu, kikubwa tunafanya kwa mipango yake Mungu.

Sikuachwa kwa utovu wa nidhani, Je wameona hilo baada ya siku tano mkataba wangu kufikia tamati, siwezi kuzungumzia hicho kitu ambacho kimeshapita na sasa niko sehemu nyingine," alisema nyota huyo ambaye ilidaiwa ameachwa Yanga kwa kosa la utovu wa nidhamu.

Alisema ana imani kazi yake ni soka na hatachagua timu atakayochezea kwa sababu yuko kwa ajili ya kufanya kazi na si vinginevyo.

Ntibazonkiza amehusishwa kutua Simba kipindi cha dirisha dogo kwa sababu ya ubora wa kiwango chake na uzoefu mkubwa aliokuwa nao ili kuwasaidia Wekundu wa Msimbazi katika Ligi Kuu Tanzania Bara na katika hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Nyota huyo amekuwa na msimu mzuri tangu alipojiunga na Geita Gold ambayo katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara iko kwenye nafasi ya tano ikiwa na pointi 21 kibindoni.



Wachezaji wa Simba Queens wakifanya mazoezi kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania utakaofanyika kuanzia Desemba 6, mwaka huu. Simba Queens ndio mabingwa watetezi na watafungua pazia kwa kuikaribisha JKT Queens kwenye Uwanja wa Mo Arena, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA SC**

# Mamilioni yanukia kwa Prisons

**Na Saada Akida**

MDHAMINI wa Tanzania Prisons, Kampuni ya Silent Ocean imeahidi kutoa Sh. milioni 20 kwa timu hiyo endapo itafanikiwa kuifunga Yanga katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Prisons pia imeahidiwa kupata Sh. milioni 10 endapo watatoka sare katika mchezo huo.

Meneja Masoko wa Silent Ocean, Mohammed Kamilangwa, alisema anaimani Prisons inaweza kuifunga Yanga kutokana na ubora wa kikosi cha timu hiyo.

Naye Kocha Mkuu wa Prisons, Patrick Odhiambo, alisema mechi hiyo itakuwa ngumu na watajiandaa vizuri kwa kuzingatia ubora na udhaifu wa Yanga ambao wameubaini katika michezo yao iliyopita.

"Tutacheza kwa tahadhari kubwa na kuwaheshimu, tutashambulia tukiwa na mpira lakini tutazuia pale mpinzani wetu anapokuwa na mpira ili kutafuta pointi muhimu katika mchezo huo," alisema Odhiambo.

## Wanariadha walia na zawadi kiduchu

**Na Said Hamdani, LINDI**

WANARIADHA walioshiriki mbio za marathon maalumu kuchangia Afua za Ukimwi, zilizofanyika mkoani hapa wameiomba Tume ya Taifa ya kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), kuboresha viwango vya zawadi ili kuwapunguzia makali ikizingatiwa wengine wanasafiri kutoka maeneo ya mbalimbali hapa nchini.

Ombi hilo limetolewa na washiriki wanne kati ya waliofanikiwa kushinda mbio hizo mara baada ya kukabidhiwa zawadi za sh. milioni 5.7 na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Patrobasi Katambi.

"Mfano sisi tunaotokea Manyara, Dodoma na Arusha, nauli haipungui kati ya Sh. 200,000 na kuendela hapo hujala chakula na kulala," alisema mmoja wa washiriki wa mbio hizo.

Mratibu wa mbio hizo, Ally Ally, alisema amepokea ushauri huo na kuahidi kufikisha mawazo yao kwa wahusika na kuelezea hali hiyo imechangiwa na kiasi kidogo cha michango walichopokea kutoka kwa wadau.

Naye Katambi akizungumza baada ya kukabidhi zawadi kwa washindi aliwapongeza washiriki wote huku akiwataka wananchi kujenga tabia ya kufanya mazoezi ili kuiweka miili yao katika afya njema.

## Netiboli Daraja la 2 mambo yameiva

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya netiboli ya Ligi Daraja la Pili yanatarajiwa kufanyika kuanzia keshokutwa hadi Desemba 10, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ndani wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, imefahamika.

Katibu Mkuu wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), Rose Mkisi, alisema mashindano hayo yatashirikisha timu 15 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

Mkisi alizitaja timu ambazo zimethibitisha kushiriki mpaka sasa ni pamoja na Kagera Queens kutoka mkoani Kagera, Katumbi Queens (Tukuyu, Mbeya), NSSF, Upendo Queens, TPBC , Tanroad (Dar es Salaam), Benjamin Mkapa, Jiji na Chipukizi ya Dodoma.

"Mashindano ya mwaka huu yatakuwa na msisimko mkubwa kwa sababu timu nyingi za mashirika zimeonyesha nia ya kushiriki jambo ambalo limefanya mchezo huu uzidi kupiga hatua," alisema Mkisi.

Aliongeza maandalizi ya ligi hiyo yanaendelea vizuri na kuzitaka timu zote zijiandae kukutana na ushindani huku akiwaita mashabiki kwenda kushuhudia vipaji.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BAYERN YAMTAKA KANE

BAYERN Munich ipo katika harakati za kumnunua mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na Timu ya Taifa ya England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29 katika klabu hiyo kwa mkataba ambao unaweza kugharimu kati ya euro milioni 80 na milioni 100. ***(Sky Sports Germany)***

### DUMFRIES ANUKIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imefanya uchunguzi kwa Inter Milan kuhusu mlinzi wao wa pembeni wa kimataifa wa Uholanzi, Denzel Dumfries, mwenye umri wa miaka 26.***(90 min)***

### MENDY, KEPA NJIA PANDA

MUSTAKABALI wa baadaye wa mlinda mlango wa Senegal, Edouard Mendy mwenye umri wa miaka 30 na Mhispania, Kepa Arrizabalaga mwenye miaka 28 ndani ya Chelsea uko shakani, huku klabu hiyo ikifikiria kuleta kipa mpya ambaye atakuwa chaguo la kwanza msimu ujao wa joto. ***(Sun)***

### BAYERN YAMKATAA RONALDO

MKURUGENZI Mtendaji wa Bayern Munich, Oliver Kahn, amesema klabu yake haitamsajili fowadi wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 Januari baada ya kuondoka kwake Manchester United. ***(Sky Germany, via Mirror)***

### CHOUPO-MOTING SOKONI

OLIVER Kahn pia amesema klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, itakaa na fowadi wa Cameroon, Eric Maxim Choupo-Moting mwenye umri wa miaka 33, kujadili mkataba mpya baada ya Kombe la Dunia, kwani mkataba wake wa sasa unatarajiwa kumalizika msimu wa joto. ***(Fabrizio Romano)***

### ROMA KUMUUZA ABRAHAM

AS Roma ipo tayari kumuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Tammy Abraham, mwenye umri wa miaka 25 katika msimu wa joto. ***(Calciomercato)***

### MESSI KUBAKIA ULAYA

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain na Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 35 anatarajiwa kubakia katika soka la Ulaya angalau hadi mwaka 2024, licha ya ripoti kuwa anakaribia kukubali dili la kujiunga na klabu ya Inter Miami ya Marekani mwakani. ***(Sky Sports)***

### GAKPO AVUTIWA WENGI

KIUNGO wa kati wa zamani wa England, Joe Cole, amesema mshambuliaji wa Uholanzi na PSV, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 23, atakuwa "kwenye rada za klabu zote kubwa" baada ya kulisaidia taifa lake kwenye Kombe la Dunia. ***(ITV, Via TalkSPORT)***

### WILDER AITAKA SHEFFIELD

ALIYEKUWA Kocha wa Sheffield United, Chris Wilder, anavutiwa na kibarua kilichoachwa wazi katika kklabu ya Queens Park Rangers baada ya Michael Beale kuachia jukumu hilo. ***(Sun)***

### KESSIE ANUKIA INTER

INTER Milan inafikiria kuwasilisha ombi la kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Franck Kessie, mwenye umri wa miaka 25, msimu ujao. ***(Calciomercato)***

### COVENTRY ASAKA TIMU

WEST Ham imemwambia kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ireland, Conor Coventry mwenye umri wa miaka 22, yuko huru kupata klabu mpya kabla ya dirisha la uhamisho la Januari. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SOUTHGATE AFURAHIA KIWANGO CHA RASHFORD

●●●Afunguka mshambuliaji huyo amebadilika na tayari amefanikiwa rekodi...

**DOHA, Qatar**

GARETH Southgate amemsifia, Marcus Rashford kwenye Kombe la Dunia kama "mchezaji tofauti kabisa" na uchezaji wake wa wakati wa michuano ya Euro 2020.

Mshambuliaji huyo wa Manchester United alikosa mkwaju wa penalti katika fainali ya Euro dhidi ya Italia kabla ya kukumbana na ubaguzi mtandaoni wakilengwa yeye, Bukayo Saka na Jadon Sancho.

Rashford alionekana kutokuwa na kiwango baada ya Euro 2020, lakini kiwango cha kuvutia akiwa na United kabla ya mapumziko ya Novemba kilimfanya apate nafasi katika kikosi cha wachezaji 26 cha Southgate kuja Qatar.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 alifunga akitokea benchi katika ushindi wa mabao 6-2 dhidi ya Iran na kusherehekea mabao mawili baada ya kuanza katika ushindi wa magoli 3-0 Jumanne dhidi ya Wales na kuipeleka England kama washindi wa Kundi B kwenye hatua ya 16.

Hilo lilimfanya Rashford kuwa mchezaji wa kwanza wa United kufunga mabao matatu kwenye michuano mikubwa kwa England tangu Bobby Charlton kwenye Kombe la Dunia 1966, na kumfanya Southgate kushangilia mabadiliko ya mshambuliaji huyo.

"Imekuwa changamoto kwake. Nilienda kumwona kabla ya msimu na kufanya naye mazungumzo kwa muda mrefu, alikuwa na mawazo juu ya kile alichohitaji kufanya," alisema kocha huyo kuhusu Rashford.

"Akiwa na klabu yake, amefurahishwa na uchezaji wake mwaka huu.

"Tuna mchezaji tofauti kabisa hapa kuliko tulivyokuwa kwenye michuano ya Euro, angeweza kuwa na hat-trick kipindi cha kwanza kwani alikuwa anaingia kwenye maeneo sahihi. Alistahili mabao yake."

Hakuna mchezaji katika Uwanja wa Ahmad bin Ali aliyefurahia miguso mingi kwenye eneo la kisanduku cha wapinzani (nane), mikwaju (sita) - moja tu pungufu ya timu nzima ya Wales.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 412,

MECHI KALI

KMC
VERSUS
MBEYA CITY

1 | 2.20
X | 2.76
2 | 3.54

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CISSE AUTOA USHINDI WA SENEGAL KWA MANE



**DOHA, Qatar**

ALIOU Cisse alitoa pongezi kwa Sadio Mane ambaye hayupo baada ya Senegal kutinga hatua ya 16 bora ya Kombe la Dunia kwa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Ecuador, hapo juzi.

Simba wa Teranga hao walipaa hadi nafasi ya pili katika Kundi A huku mabao ya Ismaila Sarr na Kalidou Koulibaly yakiwafanya watinge hatua ya mtoano kwa mara ya kwanza tangu 2002.

Matokeo hayo pia yaliifanya Senegal kuwa taifa la kwanza la Afrika kuifunga timu ya Amerika Kusini kwenye Kombe la Dunia tangu Cameroon ilipofanya hivyo kwa Colombia mwaka 1990, na hivyo kumaliza msururu wa michezo 21 bila ushindi.

Nyota wa Senegal, Mane aliondolewa Qatar 2022 baada ya kupata jeraha la mguu akiwa na Bayern Munich, lakini mawazo ya Cisse yaligeuka haraka kwa fowadi huyo baada ya ushindi huo mkubwa wa timu yake.

"Ningependa kuukabidhi ushindi huu kwa mtu ambaye anaifanyia nchi mambo ya ajabu, kwa bahati mbaya hayupo leo (juzi), huyu anaitwa Sadio Mane," alisema.

Senegal itamenyana na mshindi wa Kundi B ambaye ni England hapo Jumapili, na Cisse amesema kikosi chake kitakuwa kimejiandaa vilivyo.

"Tunajua tutapambana na England katika hatua ya 16 bora - tupo tayari," aliongeza Cisse.

"Basi hiyo itakuwa hatua mpya kwetu, tunajua tunasonga mbele katika hatua ya mtoano, ambayo ni tofauti kabisa na tulivyozoea kucheza katika aina hizi za mechi za makundi.

"Sasa ni hali ya kushinda au kupoteza, hakuna nafasi ya pili - ukishinda, unapita, ukishindwa, unarudi nyumbani.

# Courtois: Hakuna mpasuko Ubelgiji

**DOHA, Qatar**

THIBAUT Courtois amesisitiza "uongo mwingi unaenezwa" huku kipa huyo wa Ubelgiji akipuuza ripoti za mpasuko katika kambi ya Mashetani Wekundu hao.

Kombe la Dunia la 2022 linachukuliwa kuwa la mwisho kwa 'kizazi cha dhahabu' cha Ubelgiji ambacho lazima kiepuke kupoteza dhidi ya Croatia ili kupata nafasi yoyote ya kutinga hatua ya 16 bora, leo Alhamisi.

Baada ya kichapo chao cha mabao 2-0 kutoka kwa Morocco, Jan Vertonghen alionekana kutokuwa sawa na Kevin De Bruyne, ambaye alisema Mashetani Wekundu hao walikuwa "wazee sana" kuanzisha changamoto ya kweli nchini Qatar.

Wakati huo huo, Eden Hazard alieleza imani yake kikosi hicho cha kocha Roberto Martinez kina "nafasi kubwa" ya kurudia utukufu wa nchini Urusi miaka minne iliyopita, walipochapwa 1-0 na Ufaransa katika nusu fainali.

"Nadhani tunashambulia vibaya kwa sababu sisi pia ni wazee sana mbele," alisema Vertonghen aliwaambia waandishi wa habari baada ya kupoteza dhidi ya Morocco akionekana kumjibu Bruyne.

Courtois, ambaye atacheza mechi yake ya 100 leo iwapo atachakuguliwa dhidi ya Croatia, alifichua kumekuwa na mjadala miongoni mwa kundi siku ya Jumatatu, na kwamba uvumi huo umewachochea wachezaji wenzake.

"Tatizo ni uwongo mwingi unaenezwa," alisema. "Hali inaelezewa ambayo haipo. Kama kikundi, tunapaswa kuepusha hali hiyo hasi.



,613,570

# JACKPOT MECHI WIKI HII

## BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/12/22 | 02:30 | Deportivo Pasto vs Independiente Medellin | 3.01 | 2.92 | 2.35 |
| 02. 01/12/22 | 02:30 | America De Cali vs Rionegro Aguilas | 2.90 | 2.80 | 2.51 |
| 03. 01/12/22 | 04:35 | Independiente Santa Fe vs Millonarios FC | 3.35 | 3.00 | 2.29 |
| 04. 01/12/22 | 11:30 | Sreenidi Deccan FC vs Mohammedan SC | 2.76 | 3.20 | 2.35 |
| 05. 01/12/22 | 14:30 | Meizhou Kejia vs Shanghai Shenhua | 2.38 | 3.26 | 2.68 |
| 06. 01/12/22 | 15:45 | Viseu vs GD Estoril | 2.68 | 3.07 | 2.49 |
| 07. 01/12/22 | 18:00 | Croatia vs Belgium | 2.66 | 3.31 | 2.56 |
| 08. 01/12/22 | 20:00 | Maritimo vs Rio Ave | 2.75 | 3.25 | 2.50 |
| 09. 02/12/22 | 15:45 | Arab Contractors vs Ceramica Cleopatra | 2.60 | 2.75 | 3.05 |
| 10. 02/12/22 | 15:45 | Ismaily SC vs Smouha Club | 2.49 | 2.89 | 3.04 |
| 11. 02/12/22 | 22:00 | Serbia vs Switzerland | 2.55 | 3.19 | 2.75 |
| 12. 02/12/22 | 22:45 | Crewe vs Newport | 2.82 | 3.12 | 2.47 |
| 13. 02/12/22 | 22:45 | Doncaster vs Walsall | 2.63 | 3.13 | 2.63 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 01/12/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:30 | 1817 | Real Kashmir vs Tiddim Road Athlectic Club | 1.78 | 3.35 | 4.18 |
| 11:30 | 1899 | Sreenidi Deccan FC vs Mohammedan SC | 2.77 | 3.21 | 2.34 |
| 14:00 | 4674 | Zorya Lugansk vs Kolos Kovalivka | 1.62 | 3.71 | 4.69 |
| 14:30 | 3530 | Chengdu Qianbao vs Guangzhou Evergrande | 1.35 | 4.58 | 7.01 |
| 14:30 | 4560 | Meizhou Kejia vs Shanghai Shenhua | 2.01 | 3.50 | 3.16 |
| 15:35 | 2952 | Al Oruba vs Sohar Club | 4.48 | 3.31 | 1.74 |
| 15:45 | 1797 | Viseu vs GD Estoril | 2.72 | 3.05 | 2.47 |
| 15:45 | 5930 | El Daklyeh vs Coca Cola | 3.45 | 3.15 | 2.17 |
| 16:00 | 2817 | CSA Steaua Bucuresti vs Gloria Buzau | 2.02 | 3.22 | 3.41 |
| 16:00 | 3467 | Legetafo Legedadi vs Ethiopia Bunna SC | 5.25 | 3.40 | 1.62 |
| 16:00 | 3966 | KMC vs Mbeya City | 2.20 | 2.76 | 3.54 |
| 17:00 | 2422 | Mumbai City FC vs FC Goa | 1.71 | 3.79 | 3.98 |
| 17:30 | 5259 | AL Badii vs Riffa Club | 5.64 | 3.74 | 1.53 |
| 18:00 | 2494 | Croatia vs Belgium | 2.60 | 3.25 | 2.65 |
| 18:00 | 5118 | Canada vs Morocco | 3.45 | 3.30 | 2.10 |
| 18:30 | 3019 | SOL FC vs ASEC Mimosas | 5.84 | 3.31 | 1.60 |
| 18:30 | 5032 | Bahrain Club vs Muharraq SC | 5.45 | 3.36 | 1.62 |
| 19:00 | 5066 | Arba Minch Kenema vs Adama City FC | 2.14 | 3.31 | 3.02 |
| 20:00 | 1058 | Arzignanochiampo vs Pro Vercelli | 2.44 | 3.05 | 3.00 |
| 20:00 | 1461 | Olimpija Ljubljana vs NK Celje | 1.73 | 3.61 | 4.10 |
| 20:00 | 3648 | Zamalek vs Al Masry Club | 1.84 | 3.38 | 4.27 |
| 20:00 | 3859 | Maritimo vs Rio Ave | 2.61 | 3.21 | 2.66 |
| 20:00 | 4167 | Omonia Nicosia vs Karmiotissa | 1.43 | 4.37 | 5.83 |
| 20:00 | 5006 | Botosani vs Steaua Bucuresti | 4.05 | 3.46 | 1.84 |
| 20:30 | 1303 | Sitra Club vs Al Hidd Club | 2.72 | 2.91 | 2.57 |
| 21:30 | 1125 | KAA Gent W vs Sporting Charleroi W | 1.14 | 7.39 | 11.67 |
| 22:00 | 2006 | Japan vs Spain | 8.02 | 4.71 | 1.36 |
| 22:00 | 2123 | Trento Calcio 1921 vs Vicenza | 3.35 | 3.25 | 2.15 |
| 22:00 | 5475 | Costa Rica vs Germany | 16.89 | 7.61 | 1.14 |
| 23:45 | 5430 | Vitoria Guimaraes vs Belenenses | 1.33 | 4.58 | 7.59 |
| 00:00 | 5711 | CD Marathon vs CD Olimpia | 2.93 | 2.97 | 2.37 |

### IJUMAA - 02/12/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3632 | Churchill Brothers vs Aizawl FC | 2.17 | 3.25 | 3.01 |
| 14:00 | 5293 | Chernomorets Odessa vs FC Kryvbas Kriviy Rih | 2.52 | 3.05 | 2.66 |
| 15:45 | 1653 | Arab Contractors vs Ceramica Cleopatra | 2.74 | 2.84 | 2.79 |
| 15:45 | 5914 | Ismaily SC vs Smouha Club | 2.45 | 2.90 | 3.10 |
| 16:30 | 3062 | UTA Arad vs Sepsi Osk | 3.77 | 3.03 | 2.06 |
| 17:30 | 1033 | Al Ahli Manama vs Al Hala Muharraq | 2.33 | 3.10 | 3.10 |
| 18:00 | 1130 | Ghana vs Uruguay | 4.52 | 3.66 | 1.74 |
| 18:00 | 5680 | South Korea vs Portugal | 4.82 | 4.11 | 1.62 |
| 18:30 | 2154 | Al Shabbab vs Manama Club | 4.27 | 3.35 | 1.76 |
| 20:00 | 2672 | Doxa Katokopia vs Akritas Chlorakas | 2.09 | 3.40 | 3.35 |
| 20:00 | 3591 | EN Paralimni vs AEK Larnaca | 4.82 | 3.76 | 1.68 |
| 20:00 | 4379 | Eyupspor vs Tuzlaspor | 1.40 | 4.37 | 6.41 |
| 20:00 | 5310 | Neftchi Baku vs Karabakh | 4.49 | 3.61 | 1.67 |
| 20:30 | 5826 | AL Khalidiyah vs East Riffa | 1.90 | 3.05 | 4.07 |
| 22:00 | 1170 | Cameroon vs Brazil | 9.61 | 5.40 | 1.28 |
| 22:45 | 2514 | Glenavon vs Larne | 5.25 | 4.28 | 1.48 |
| 22:45 | 2554 | Charlton vs Cheltenham | 1.72 | 3.57 | 4.56 |
| 22:45 | 2834 | Ipswich vs Fleetwood Town | 1.34 | 4.75 | 8.31 |
| 22:45 | 2910 | Plymouth vs Port Vale | 2.06 | 3.47 | 3.27 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# FUNDI RANGI ALAMBA BONUS YA SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Kipunguni, jijini Dar es Salaam, Bilal Kambwande amechomoka na kitita cha Sh. milioni 6.3 kama bonus ya ushindi katika Supa Jackpot ya Sportpesa wikiendi iliyopita.

Akizungumza katika ofisi za Sportpesa Oysterbay jijini, Bilal alisema alianza kucheza na Sportpesa miaka mitano iliyopita, hii ni baada ya yeye kuona washindi mbalimbali waliokuwa wanatangazwa baada ya kushinda.

''Mimi nilianza kucheza mwaka 2017 ambapo niliwaona na kusikia washindi mbalimbali waliopita ambapo walikuwa wakitangazwa kwenye magazeti na TV''.

Bilal alisema tangu ameanza kucheza na Sportpesa anashukuru Mungu ameshawahi kushinda Sh. 900,000/ Sh. 600,000 na Sh. 200,000 kabla ya ushindi huu wa Supa Jackpot bonus alioupata wikiendi hii.

''Kama kuna bahati ambayo ninayo basi hii ya kuwahi kushinda siku za nyuma na sasa ambapo leo nimekuja kwa ajili ya utambulisho na uhakiki wa Supa Jackpot bunus yangu niliyoshinda''.

Kuhusu mkeka ulioshinda Bilal alisema mara nyingi yeye huchukua siku mbili hadi tatu akitathmini mikeka kabla hajaiweka.

Aliongeza fedha aliyoipata atanunua kwanza boda boda na nyingine ataangalia afanyie nini. ''Mimi ndoto yangu ilikuwa kumiliki pikipiki almaarufu bodaboda hivyo nashukuru nimetimiza ndoto yangu ya kumiliki mali hiyo''.

Aliongeza anawaasa Watanzania wasiache kujaribu bahati zao kwani Sportpesa haina longolongo kwenye malipo. ''Mimi ni shuhuda kama ambavyo nilikuwa nasikia kwa wengine na sikuwahi kata tamaa juu ya kuja kushinda''.

Naye Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Sportpesa, Sabrina Msuya, alimpongeza mshindi huyo na kumtaka akawe mfano mzuri kwa wengine.

'Nampongeza Bilal kwa ushindi wake na kupitia ushindi huu akawe mfano bora kwa wengine kwa kuendelea kuwapa ushuhuda na elimu ya namna ya kujisajili, kuweka pesa na kucheza,'' alisema Sabrina.

Jackpot yetu ya katikati ya wiki imesimamia Sh. 412,613,570 na Supa Jackpot ni zaidi ya bilioni moja.




Fundi rangi kutoka Kipunguni, Ilala jijini Dar es Salaam, Bilal Kalambwande, akiwa ameshikilia hundi ya mfano ya Sh. milioni 6.3 kama bonus ya ushindi wa Supa Jackpot ya Sportpesa baada ya kuibuka mshindi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Mgunda: Simba

INATOKA UK. 32

Coastal Union haitapelekea mchezo uwe rahisi," Mgunda alisema.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kikosi cha timu hiyo kinatarajia kuondoka jijini leo kuelekea Tanga kwa ajili ya kuendeleza mapambano ya kuwania ubingwa.

Wakati huo huo, katika mbio za kuwania Kombe la FA, Azam FC imepangwa kuanza na Malimao FC kutoka mkoani Katavi na ratiba inaonyesha timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu zitaanzia nyumbani, mechi za raundi ya pili zikitarajiwa kuchezwa kati ya Desemba 5 hadi 15, mwaka huu.

Yanga ndio mabingwa watetezi wa michuano hiyo ambao waliwafunga Coastal Union penalti 4-1 baada ya kupata sare ya mabao 3-3 katika dakika 120, fainali ikichezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha.

# YANGA YAELEZA ILIPOANGUKIA

INATOKA UK. 32

zoefu.

Mwambusi alisema kwa kufahamu hivyo, aliwatengeneza vijana wake namna ya kukabiliana nao na anashukuru Mungu mipango yake ilikwenda vyema.

"Tulienda na 'plani' ya kuwaheshimu Yanga lakini siyo kuwaogopa. Niliwaambia vijana wangu twendeni tukacheze mpira, tuwaheshimu lakini tusiwaogope, tucheze mpira wetu mzuri ambao unaweza kutupatia nafasi chache tukazitumia na kweli wachezaji wangu wakalichukulia kwa umakini jambo nililowaambia," alisema Mwambusi. Kocha huyo wa zamani wa Yanga alisema kwa ushindi walioupata umewapa wachezaji wake ari zaidi ya kupambana na kushinda katika mechi zinazofuata kwa ajili ya kuhakikisha wanaibakisha timu hiyo kwenye Ligi Kuu.

"Tulicheza kwa kujiamini hasa kipindi cha pili, tulitengeneza mipango ambayo ingetuhakikishia tunatoka na matokeo mazuri na tulipopata bao la pili nikaingiza wachezaji wenye uwezo wa kuzuia zaidi, kusema kweli mechi ilikuwa ngumu, hatukutaka kupiga mipira mirefu, tulitaka tumiliki ndiyo njia ya kupoteza muda na kweli tukafanikiwa. Kwa sasa timu inanipa mwelekeo, lengo langu kubwa ni kuhakikisha timu inabaki ligi kuu, sina haja ya ubingwa wala nne bora," Mwambusi alisema.

Aliongeza mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ni ngumu kwa sababu kila timu inapoingia uwanjani inasaka ushindi na si kusindikiza.

"Ligi ni ngumu sana, tunaendelea kupambana katika kila mechi, bado ni mapema kusema nani atashuka, nani atachukua ubingwa, timu zote zinapambana," aliongeza kocha huyo ambaye pia aliwahi kuifundisha Mbeya City.

Ligi hiyo inatarajia kuendelea tena kesho kwa Singida Big Stars kuikaribisha Namungo FC wakati Kagera Sugar yenyewe itawavaa Ihefu kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba.

# Michezo

Alhamisi Desemba 1, 2022

Nipashe




UKURASA 29

## Southgate afurahia kiwango cha Rashford



Straika wa Timu ya Taifa ya Marekani, Christian Pulisic (jezi ya bluu), akifunga bao pekee dhidi ya Iran katika mechi ya Kundi B ya mashindano ya Kombe la Dunia iliyochezwa kwenye Uwanja wa Al Thumama Doha, Qatar juzi usiku. Marekani itakutana na Uholanzi keshokutwa katika hatua ya 16-bora. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YAELEZA ILIPOANGUKIA

●●● Yakiri imecheza chini ya kiwango, kuanza na Kurugenzi Kombe la FA...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupoteza mechi ya kwanza msimu huu na kusitisha rekodi yake ya 'Unbeaten', Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema wachezaji wake walikuwa na uchovu wa kucheza mechi nyingi mfululizo bila ya kupata muda wa kupumzika.

Ikitokea nyuma, Ihefu SC ambayo kabla ya mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Highland Estates uliopo Mbarali, Mbeya ilikuwa inaburuza mkia, ilipata ushindi wa mabao 2-1 na kupanda hadi katika nafasi ya 13 katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kufikisha pointi 11.

Akizungumza na gazeti hili, Kaze, alisema viwango vya wachezaji wao vilikuwa chini na hii inatokana na ratiba ngumu waliyonayo kwenye ligi hiyo licha ya kuendelea kukaa kileleni katika msimamo.

"Nyinyi wenyewe mmeona wachezaji wote viwango vyao havikuwa vizuri hata kidogo, imefika wakati watu wanashindwa hata kukimbia. Hii ratiba ni ngumu sana, lakini tayari limeshatokea, tumepoteza, tuwape hongera tuliocheza nao kwa sababu wamepambana, unajua kuna wakati ukipoteza inakupa wakati mzuri wa kukaa chini kujitathmini na kujipanga vizuri kuliko kila siku ukiwa unashinda tu.

Ninawambia mashabiki wa Yanga hakuna timu inayocheza inataka kushindwa, lakini tumeshindwa, tumecheza mechi 49 bila kupoteza, leo (juzi) tumepoteza, tunaenda nyumbani kujirekebisha, tunaahidi tutakuja vizuri zaidi," alisema Kaze.

Aliongeza wameshafunga ukurasa kuhusiana na mchezo huo na sasa akili yao inaelekea kujiandaa kuwakaribisha Tanzania Prisons hapo Jumapili.

Juma Mwambusi, Kocha Mkuu wa Ihefu SC, alisema alijipanga vyema kuwakabili Yanga kwa sababu anaifahamu vizuri, anajua jinsi gani huwa wanacheza, anafahamu ni timu kubwa nchini na yenye wachezaji wazuri wenye viwango vikubwa na wa-

INAENDELEA UK. 31

## Mgunda: Simba, Coastal joto juu

**Na Saada Akida**

HUKU ikipangwa kuanza kuwania taji la mashindano ya Kombe la FA kwa kuivaa Eagle FC ya Dar es Salaam, Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amesema anaendelea kufanyia kazi madhaifu yaliyopo kwenye kikosi chake ili ajihakikishe kuvuna pointi tatu kila watakaposhuka dimbani.

Simba itaifuata Coastal Union katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuchezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga.

Mgunda alisema kuelekea mchezo huo, amempa jukumu la kuongoza 'mauaji' kiungo, Clatous Chama katika kazi ya kupika mabao kwa washambuliaji wa timu hiyo wanaoongozwa na Mosses Phiri, ambaye ni kinara wa kufumania nyavu ndani ya klabu hiyo.

Kocha huyo alisema pia ametoa majukumu mengine kwa kiungo mkabaji, Sadio Kanoute na mabeki kuhakikisha wanawabana washambuliaji wa Coastal Union kutovuka kwenda kufanya mashambuluzi katika eneo la Wekundu wa Msimbazi.

Aliongeza licha ya kupata ushindi dhidi ya Polisi Tanzania, Maafande hao waliwapa upinzani mkubwa kitu ambacho anategemea pia kitatokea katika mchezo dhidi ya Coastal Union.

"Mechi dhidi ya Polisi imemalizika na sasa tunajianda na mchezo ujao, ule ulikuwa mchezo mzuri wenye upinzani mkubwa na tunashukuru Mungu tumefanikiwa kupata ushindi mnono ugenini. Pamoja na ushindi tuliopata lakini kuna mapungufu yameonekana na mimi kama mwalimu na benchi langu la ufundi tutayafanyia kazi mazoezini ili yasiwepo katika mchezo ujao," alisema Mgunda.

Aliongeza mechi dhidi ya Coastal Union itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu ya maandalizi ya kila timu na kuwafamu wachezaji wa timu hiyo ni jambo lingine litakalomwongezea changamoto.

"Kila mechi tunajiandaa vizuri, kila mchezaji anatambua ugumu na umuhimu wa kutafuta pointi tatu, tutaingia kwa tahadhari kubwa, sababu ya kuwahi kufundisha

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002